

Makusudio 23 Adhimu
ya
Ujenzi wa Baitullah

Na

Hadhrat Mirza Nasir Ahmad^{rh}
Khalifatul Masihi wa Tatu

Makusudio 23 Adhimu ya Ujenzi wa Baitullah

Tafsiri ya Kiswahili ya:

Tameer Baitullah ke Te-ees Azeemush-Shaan Maqaasid
(Kiurdu)

Tameer Baitullah kei Ta'ees Azeemush-Shaan Maqaasid
(Swahili Translation)

Hotuba zilizotolewa na:

Hadhrat Mirza Nasir Ahmadth Khalifatul Masihi wa Tatu

Mfasiri

Jamil R. Rafiq

Chapa ya Kwanza (Kiurdu): 1968

Chapa ya Kwanza (Kiswahili): 2021

© **Islam International Publications Ltd.**

Kwa Maelezo Zaidi:

Tanzania:

Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, Tanzania
Mtaa wa Bibi Titi Mohamed S.L.P. 376, Dar es Salaam.
Simu: +255222110473 Fax: +255222121744

Kenya:

E.A. Ahmadiyya Muslim Mission
P.O. Box 40554 Nairobi Kenya Simu: +254222111031

Kimechapwa na Ahmadiyya Printing Press
Dar es Salaam, Tanzania / Nairobi, Kenya

ISBN: 978-1-84880-782-2

10 9 8 7 6 5 4 3 2 1

MAELEZO YA MWENEZI

Dawati la Kiswahili linaweka mbele ya wasomaji tafsiri ya hotuba 10 za Ijumaa za Hadhrat Khalifa wa Tatu^{rh} alizozitoa kuhusiana na ‘Makusudio 23 Adhimu ya Ujenzi wa Baitullah’ mnamo mwaka 1967 ndani ya Masjid Mubarak, Rabwah, Pakistan.

Amefafanua hekima za ndani sana za ujenzi wa Kaaba ambazo mtu akizielewa kwa kuzisoma kwa makini hotuba hizi atachangamka sana kiroho, kwani kwa njia hii hayajapata kuelezwa makusudio ya kujenga upya Kaaba kupitia Hadhrat Ibrahim^{as} na Hadhrat Ismail^{as}. Umuhimu wa hotuba hizi zajulikana vizuri mkijua Ufunuo mmoja wa Seyidna Ahmad^{as} uliomo ndani ya Tadhkira, uk. 80, kwamba:

“Yule mtu anayeufahamu msingi wa Kaaba kuwa suala la hekima ya Mungu, huyo ndiye mwenye lubu sana kwani anayo hadhi katika siri za ulimwengu wa malaika.”

Baadhi ya sehemu za hotuba hizi zapaswa kusomwa mara mbili tatu ili kuzingatia barabara muradi wake.

Mwenyezi Mungu Awajaalie wasomaji watukufu kupata maarifa ya ndani sana ya shabaha ya Mwenyezi Mungu kujenga upya Kaaba kupitia Hadhrat Ibrahim^{as} na mwanaye Hadhrat Ismail^{as}.

Sheikh Ansar Hussain ametia bidii kupanga herufi zake
kwa kompyuta na kufanya kazi ya fomati; yuastahili
kushukuriwa.

Jamil R. Rafiq

Wakilut-Tasnif

Tahrike Jadid

Rabwah, Pakistan.

31 Desemba 2020

①

**Makusudio 23 Adhimu
ya Kujengwa Upya Baitullah
Kupitia Hadhrat Ibrahimu^{as}**

Hotuba ya Ijumaa, 31 Machi 1967,
Masjid Mubarak, Rabwah, Pakistan.

“Mwenyezi Mungu Alijenga upya Baitullah kupitia Hadhrat Ibrahim^{as}, na Akachukua ahadi kutoka kwa Hadhrat Ibrahim^{as} kuwa yeye na kizazi chake wakijitolea wakfu maisha yao katika njia ya Mwenyezi Mungu wataendelea kutekeleza majukumu yao yahusianayo na ujenzi wa Baitullah. Na watajibidiisha kwa tadbiri na dua ya kwamba Nabii wa mwisho wa kuleta sheria atakapotumwa na Mwenyezi Mungu duniani, wazao wake wajaaliwe na Mwenyezi Mungu kumpokea. Na baada ya kusilimu watoe dhabihu ya hali ya juu watakayotakiwa kutoa kwa kutukuza jina la Mwenyezi Mungu.

Shabaha nyingi na makusudio mengi yanahusiana na Baitullah ambayo tunakuta yametajwa ndani ya Kurani Tukufu ambayo kwa hakika yanahusiana na kutumwa kwa Nabii Mtukufu^{saw}.”

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

تَحْمِيدًا وَنُصَلِّيَ عَلَى رَسُولِهِ الْكَرِيمِ²

Baada ya kutoa Shahada mbili na A'udhu na kusoma Sura Al-Faatiha, Hudhurth akasoma aya zifuatazo za Kurani Tukufu:

إِنَّ أَوَّلَ بَيْتٍ وُضِعَ لِلنَّاسِ لَلَّذِي بِبَكَّةَ مُبْرَكًا وَهُدًى لِلْعَالَمِينَ ﴿١﴾ فِيهِ آيَاتٌ بَيِّنَاتٌ مِّمَّا قَامَ إِبْرَاهِيمُ ۖ وَمَنْ دَخَلَهُ كَانَ آمِنًا ۗ وَلِلَّهِ عَلَى النَّاسِ حِجُّ الْبَيْتِ حَيْثُ أَشَاءَ ۗ لِلَّهِ سَبِيلًا ۗ وَمَنْ كَفَرَ فَإِنَّ اللَّهَ غَنِيٌّ عَنِ الْعَالَمِينَ ﴿٢﴾
(Aali 'Imraan, 3:97-98)

وَإِذْ جَعَلْنَا الْبَيْتَ مَثَابَةً لِّلنَّاسِ وَأَمْنًا ۗ وَاتَّخِذُوا مِنْ مَّقَامِ إِبْرَاهِيمَ مُصَلًّى ۖ وَعَهِدْنَا إِلَىٰ إِبْرَاهِيمَ وَإِسْحَاقَ أَن طَهِّرَا بَيْتِيَ لِلطَّائِفِينَ وَالْقَائِمِينَ وَالرُّكَّعِ السُّجُودِ ﴿١﴾ وَإِذْ قَالَ إِبْرَاهِيمُ رَبِّ اجْعَلْ هَذَا بَلَدًا آمِنًا وَارْزُقْ أَهْلَهُ مِنَ الثَّمَرَاتِ ۖ مَنْ الثَّمَرَاتِ مَنْ آمَنَ مِنْهُمْ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ ۗ قَالَ وَمَنْ كَفَرَ فَأُمَتِّعُهُ قَلِيلًا ثُمَّ أَضْطَرُّهُ إِلَىٰ عَذَابِ النَّارِ ۗ وَبِئْسَ الْمَصِيرُ ﴿٢﴾ وَإِذْ يَرْفَعُ إِبْرَاهِيمُ الْقَوَاعِدَ مِنَ الْبَيْتِ وَإِسْحَاقُ ۖ رَبَّنَا تَقَبَّلْ مِنَّا ۖ إِنَّكَ أَنْتَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ ﴿٣﴾ رَبَّنَا وَاجْعَلْنَا مُسْلِمِينَ لَكَ وَمِنْ دُونِنَا أُمَّةٌ مُّسْلِمَةٌ لَّكَ ۗ وَارِنَا مَنَاسِكَنَا وَتُبْ عَلَيْنَا ۖ إِنَّكَ أَنْتَ التَّوَّابُ الرَّحِيمُ ﴿٤﴾ رَبَّنَا وَابْعَثْ فِيهِمْ رَسُولًا مِنْهُمْ يَتْلُو عَلَيْهِمْ آيَاتِكَ وَيُعَلِّمُهُمُ الْكِتَابَ وَالْحِكْمَةَ وَيُزَكِّيهِمْ ۗ إِنَّكَ أَنْتَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿٥﴾

(Al-Baqara, 2:126-130)

Baadaye akasema:

Nilianzia madhumuni yangu haya siku ya Idul-Haji na kusema kwamba Mwenyezi Mungu Alijenga upya Baitullah kupitia Hadhrat Ibrahim^{as} na kuchukua ahadi kutoka kwa Hadhrat Ibrahim^{as} kuwa yeye na kizazi chake wakijitolea wakfu maisha yao katika njia ya

¹ Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwingi wa na Ukarimu.

² Twamhimidia Yeye na kumsalia Mtume Wake mhashamu.

Makusudio 23 Adhimu ya Ujenzi wa Baitullah

Mwenyezi Mungu, wataendelea kutekeleza majukumu yao yahusianayo na ujenzi wa Baitullah. Na watajibidiisha kwa tadbiri na dua ya kwamba Nabii wa mwisho wa kuleta sheria atakapotumwa na Mwenyezi Mungu duniani, wazao wake wajaliwe kumpokea. Na baada ya kusilimu watoe dhabihu ya hali ya juu watakatwa kutoa kwa kutukuza Jina la Mwenyezi Mungu.

Nilisema kwamba shabaha nyingi na makusudio mengi yanahusiana na Baitullah, ambayo twaona yametajwa ndani ya Kurani Tukufu, na ambayo kwa hakika yanahusiana na kutumwa kwa Nabii Mtukufu^{saw}. Aya hizi nilizosoma sasa hivi, zisomwapo kwa makini, makusudio yafuatayo twayakuta ambayo kwa ajili yake Mwenyezi Mungu Alijengesha upya Baitullah na Akadumu kufanya vizazi vyake waendeleo kutoa dhabihu kwa miaka elfu mbili na mia tano.

Shabaha ya kwanza imeelezwa katika *'Wudhi'a linnaasi'* – iliyowekwa kwa watu; na ya pili ndani ya *'Mubarakan'* – yenye baraka. Shabaha ya tatu imeelezwa ndani ya *Hudan lil-'alamiin* – mwongozo kwa walimwengu; ya nne *Ayaatun bayyinaat* – ishara bayana; ya tano *Makamu Ibrahim* – mahali aliposimama Ibrahim; ya sita *man dakhlahu kaana Aaminaa* – atakayeingia humo atakuwa salama; ya saba *wa lillah 'alannasi hijjul baiti manis-tataa'a ilaihi sabiila* – na kwa ajili ya Mwenyezi Mungu watu wafanye hija kwenye Nyumba hiyo – awezaye kufunga safari ya huko; ya nane *Ja'alnal baita mathabatan linnasi* –

Tuliifanya Nyumba iwe mahali ya kuendewa na watu; ya tisa *wa amnaa* – na pa salama; ya kumi *Wattakhidhuu min makami Ibrahima musalla* – na mpafanye mahali aliposimama pawe pa kusalia. Shabaha ya kumi na moja imeelezwa katika *Tahhiraai baitiya* – mwitakase Nyumba yangu. Shabaha ya kumi na mbili imo ndani ya neno *Taaifiina* – waizungukao. Shabaha ya kumi na tatu imeelezwa katika neno *'Aakifiina* – kwa wakaao. Shabaha ya kumi na nne imeelezwa ndani ya *Warruka'is Sujuud* – na kwa wanaorukuu na kusujudu. Shabaha ya kumi na tano imeelezwa katika *Rabbij'al haadhaa baladan Aaminan* – Mola wangu, uufanye mji huu uwe wa salama. Shabaha ya kumi na sita imeelezwa ndani ya *Warzuk Ahlahuu minath Thamaraati* – Uwape wenyeji wake matunda. Shabaha ya kumi na saba imeelezwa ndani ya *Rabbanaa Takabbal minnaa* – Ee Mola wetu, Utupokelee. Shabaha ya kumi na nane imeelezwa ndani ya *Assamii'* – Asikiaye sana. Shabaha ya kumi na tisa imeelezwa katika *Al-'Aliim* – Mjuzi sana. Shabaha ya ishirini imeelezwa katika *wa min dhurriyyatinaa Ummatan Muslimatan laka* – na uwafanye wazao wetu kuwa wajitupao kwako. Shabaha ya ishirini na moja imeelezwa katika *wa arinaa manaasikanaa* – na Utuonyeshe njia za ibada yetu. Ya ishirini na mbili imeelezwa katika *wa tub 'alainaa* – na Utuelekee. Na shabaha ya ishirini na tatu imeelezwa katika *Rabbanaa Wab'ath fiihim Rasulan minhum* – Mola wetu, na mwinue ndani yao Mtume kutoka miongoni mwao.

Mwenyezi Mungu Anasema; *Inna awwala baitin wudhi'a Linnasi*, nyumba ile iliyofanywa, iliyojengwa, kwa ajili ya watu wote imo ndani ya Makka. Kutokana na riwaya mbalimbali na aya za Kurani Tukufu zilizoelezwa katika sehemu mbalimbali nimefahamu kwamba Adamu^{as} wetu alipoumbwa na kutumwa (Nimetumia neno Adamu wetu, kwani Nabii Mtukufu^{saw} amesema kuwa ma-Adamu wapatao laki moja waliumbwa katika dunia hii waliopita kabla ya Adamu^{as}. Mawalii wa Kiislamu wamewahi kuona katika hali ya kashfi baadhi ya wazao wa ma-Adama wa zamani, na wamewataja katika vitabu vyao), wakati huo dunia ilikaliwa katika sehemu ndogo sana, na hapo Mwenyezi Mungu kwa hekima yake kamilifu Akimfunulia wahyi Adamu na kujengesha Baitullah, Akajengesha Nyumba moja, na Akaihusisha Nyumba hii kwa wazao wa Adamu huyo. Lakini baadaye kizazi hiki kilipozidi na kuenea na kusakinia maeneo mbalimbali ya dunia, hapo Mwenyezi Mungu kwa kuona ukuaji wao wa ruhania na akili, Akaanza kuwatuma manabii mbalimbali ndani ya kila kaumu na kila sehemu tofauti, ili hao manabii wajaribu kuwaongoza watu kwenye njia ambazo kwa kuzifuata hizo mja wa Mwenyezi Mungu anaweza kutekeleza majukumu yake ya kuwa mtumishi wa Mungu. Na kutokana na Hadithi inajulikana kwamba manabii zaidi ya laki moja wameisha pita duniani. Basi yule Adamu ambaye wazao wake walikuwa wametawanyika namna ambavyo wakawa kaumu mbalimblai tofauti ambao kila

kaumu yao ilikuwa na nabii wake, nao wakaacha kuitunza Nyumba ile iliyokuwa Nyumba ya Mungu iliyowekwa kwa wanadamu wote. Basi kwa sababu ya kutokutunzwa, hata alama zake zikafutika kwa maafa ya asilia na kutokarabatiwa na kukosekana wakazi sehemu hiyo. Lakini ulipowadia wakati wa kutimia matakwa ya Mwenyezi Mungu kwamba dunia mara nyingine ikusanywe katika dini moja, Mwenyezi Mungu Akaamua kuijenga upya Nyumba hii, na kwa kuitunza Akaamua kwamba Hadhrat Ibrahim^{as} na kizazi chake wajitolee wakfu ili izalike kaumu moja watakaohusikana na Nyumba ya Allah, ambao watakuwa na vipawa vyote vinavyopaswa kuwapo katika kaumu watakaokuwa wa kwanza kuongozwa na Muhammad^{saw} Mtume wa Mungu na Kurani Tukufu. Basi, kwa maombi na kujitoa wakfu, kaumu moja ikawa tayari katika miaka elfu mbili na mia tano. Kama hao wawe wa Mwenyezi Mungu, basi vipawa walikuwa navyo vyote vile ambavyo kwavyo waweze kuwaongoza wanadamu katika nyanja za ruhania. Na kwa kuwa vipawa hivyo na nguvu hizo zilikuwa zimekwishafikia upeo wake, fitina kubwa ingeweza kuzuka kwa kutumia nguvu hizo vibaya, hivyo maadamu walipokuwa wapotevu, wakampinga vikali sana Nabii Mtukufu^{saw}, na kumtesa sana jinsi hata umati wowote wa hapo kabla usivyomtesa nabii wake. Ilmuradi walikuwa na vipaji vingi, vikaendelea kufichika kwa mwia, shetani akawatawala kwa muda. Lakini vipawa hivyo vilivyokuwa ‘vimelala’ vilipozinduka na hao wakamtambua Mola wao,

hapo dunia ikaona mandhari ya kujitoa dhabihu katika njia ya Mwenyezi Mungu isiyoonna hapo kabla. Kwa kifupi, hii ilikuwa ni kaumu iliyozalika kwa sababu ya dhabihu za Hadhrat Ibrahim^{as} na dua zake na dhabihu za wazao wake na dua zao.

Kwa ufupi, muradi wa kweli wa *wudhi'a linnaasi* unahusiana na Mtume^{saw}. Lakini, Mwenyezi Mungu alikuwa Amemuambia Hadhrat Ibrahim^{as} kwamba mimi Naijengesha upya Nyumba hii iliyo Nyumba Yangu kwa shabaha hizo, hivyo hutakuwa na budi kutoa dhabihu kwa ajili ya hizo.

Almuradi, shabaha ya kwanza ihusikanayo na Baitullah ndiyo hii kwamba Baitullah ni Nyumba ile ya kwanza kabisa ambamo Mwenyezi Mungu Ameyaweka manufaa ya dini na ya dunia kwa wanadamu wote. *Wudhi'a linnaasi*, yaani hii imejengwa kwa ajili ya wema wa wanadamu wote. Kutoka humo mataifa yote ya dunia bila ubaguzi wa rangi na kimbari, na pasipo kujali mambo yawatenganishayo baadhi yao na wengine, yatapata manufaa ya kidunia pia na ya dini vilevile. Hili ndilo kusudio la kwanza la kujenga upya Nyumba hii.

Kusudio la pili la ujenzi wa Baitullah ni kwamba Sisi Twataka kuifanya Nyumba hii (Baitullah) kuwa *Mubarakan*. Na *mubarakan* humaanisha nyanda za chini; kama ikinyesha mvua, maji ya pande zote nne hukusanyika hapo. Kwa kuwa Mwenyezi Mungu katika sehemu hii Haongei kuhusu mvua, bali habari za

Makusudio 23 Adhimu ya Ujenzi wa Baitullah

ustawi na maendeleo ya kidini na ya kidunia yanazungumzwa, hivyo neno *Mubarakan* hapa lina maana mbili. Mosi, wawakilishi wa mataifa yote ya dunia watadumu kujumuika hapo. Ya pili ni kwamba Sisi Tumeijengsha Baitullah na kuamua iwe inazuriwa kwa lengo la kuimarisha hapa sheria, kumwinua hapa Nabii mwenye kuleta sheria ya mwisho, ambayo ndani mwake miongozo yote na kweli zote za kiroho zijumuishwe zilizokuwa zimekwepo katika sheria tofauti za mataifa mbalimbali, hata kwamba usibaki ukweli wowote nje ya sheria hii.

Basi, Akasema, Twataka kuifanya Baitullah hii *Mubarakan* kwa njia ya Kiroho. Na lengo letu ni kuwa hii itakuwa ni mahali pa kuzalika kwa sheria ambamo miongozo yote ipatikanayo katika sheria mbalimbali za manabii wote itakusanywa ndani mwake. Isitoshe, ndani mwake mtakuwa na baraka hii pia kwamba mambo mengine yote vilevile yatakwemo humo ambayo hayakuwa ya lazima kwa watu wa zamani, kwani hawakuwa na uwezo wa kuyavumilia; kweli hizo zote pia zaelezwa humo, nayo itakuwa ni sheria kamilifu timilifu itakayoimarishwa kwa manufaa ya mataifa yote. Na Nyumba hii, Baitullah hii, itakuwa *Ummul Kuraa* – kwa ajili ya sheria hii ya kudumu iliyo kamilifu timilifu.

Kusudio la tatu la ujenzi wa Baitullah limeelezwa katika *hudan lil'alamiin* – mwongozo kwa walimwengu. Kumbukeni kwamba mwanzoni mwa aya hizi ilielezwa

wudhi'a linnasi, yaani Twaijenga Nyumba hii kwa dunia nzima, mataifa yote na zama zote. Uhusiano wake na mataifa yote Ameukariri mara kwa mara ndani ya aya hizi. Mwenyezi Mungu Anasema kuwa kusudio la tatu la ujenzi wa Nyumba hii ni *Hudan lil'alamiin*, yaani iwe ni njia ya mwongozo kwa walimwengu wote. Neno *Hudan* pia laashiria '*Alamiin*' kwani akili na busara, elimu na maarifa ambamo wanadamu wote wanashirikiana, huitwa mwongozo. Minghairi yake elimu za ruhania haziwezi kuendelea kwani, kwa mfano, yule asiye na akili atakuwa punguani, hawajibiki, sheria haimhukumu. Kwa kifupi, akili ni msingi wa sheria na wa zile maana zilizomo ndani ya neno 'mwongozo'. Hivyo, Mwenyezi Mungu Amesema hapa kuwa Sisi Tutathibitisha kupitia Nyumba hii kwamba mataifa yote kiakili, kibusara, kimaarifa na kielimu yana vipaji vya aina moja; taifa moja halina ubora kuliko jingine kwa njia hii.

Ndani mwake mmeashiriwa pia kwamba katika zama ambamo utukufu wa *mwongozo kwa walimwengu* utadhihiri, yaani baada ya Nabii Mtukufu^{saw} kutumwa, wakati huo yatazalika duniani baadhi ya mataifa yatakayosema kwamba sisi tunayo akili nyingi na tunacho kipawa zaidi cha busara na cha kuelimika na kwamba yapo mataifa mengine ambayo Mwenyezi Mungu Ameyaumba kwa shabaha hii tu kuwa yatawaliwe nasi. Hivyo, Mwenyezi Mungu Anasema kwamba Sisi Tutahakikisha kupitia Nyumba hii kwamba taifa moja haliwezi kutofautishwa na taifa jingine

kuhusiana na akili, busara na elimu za kimsingi. Mwenyezi Mungu Amewaumba wanadamu wote kumwabudu Yeye. Na ili kupata lengo hili, ile akili, busara, maarifa na elimu vinavyohitajika vimetolewa kwa mataifa yote kwa usawa, yaani yote hayo yana vipawa hivyo barabara; tofauti ya vipawa yaweza kuwa baina ya mtu mmoja na mwingine, lakini taifa lolote halina ubora kulinganishwa na taifa jingine.

Maana ya pili ya *Hudan lil 'alamiin* ni kwamba Mwenyezi Mungu Ataanzisha Kurani Tukufu kuteremka kutoka mahali pa Baitullah hii, kwani ndani ya *mufradaat Raghīb* imo kwamba maana moja ya *hidaya* ndio ule mwongozo ambao Mwenyezi Mungu Amewaita kwao wanadamu kupitia manabii na tena kwa kuteremka Kurani Tukufu; yaani Akasema, 'Njoooni hapa, hizi ndizo njia za mwongozo, mkizifuata hizi mtaweza kunifikia. Hivyo, katika maana ya 'mwongozo', Mtume^{saw} na manabii wote wanashirikiana. Lakini 'mwongozo kwa walimwengu' huhusiana na Mtume^{saw} pekee, kwani manabii wengine wote walitumwa kwa ajili ya zama zao na mataifa yao tu. Basi, Mwenyezi Mungu Amenena hapa kwamba Baitullah hii ni sehemu ya Kurani Tukufu kushuka, toka hapa Kurani Tukufu itaanza kuteremka, na kwa sababu hii Twaihifadhi na kuandaa njia za kuitakasa.

Maana ya tatu ya *hudan lil 'alamiin* ni kuwa Mwenyezi Mungu Amesema kwamba Baitullah ni mahali itakapoanzia sheria ile itakayomfungulia binadamu

milango ya maendeleo yasiyo na kikomo. Kwani maana ya tatu sawa na Imam Raghīb ni hii kwamba mtu anapozifuata njia za mwongozo na kutenda amali njema, basi Mwenyezi Mungu Humjaalia mwongozo mwingine zaidi. Hivyo, kwa sababu ya kila amali njema, mtu anajaaliwa amali njema zaidi Anayoipenda zaidi Mwenyezi Mungu. Yaani, mwongozo huu utaendelea kumpandisha mtu hatua kwa hatua daraja za maendeleo ya ruhania, na umati huu utafunguliwa milango ya maendeleo yasiyofikia ukomo. Kisha Akasema kusudio la kuweka Baitullah ni hili kwamba kwa njia ya *hudan lil-'alamiin* (kutokanan a maana yake ya nne) utaletwa umati wa Kiislamu utakaoneemeshwa kwa neema usizozipata umati wowote wa hapo kabla, na mpaka Kiama binadamu wataendelea kupata thawabu za aina hii zilizokamilika na kutimilika na fadhili na rehema za Mwenyezi Mungu, maana, Imam Raghīb ameandika *Al-Hidayatu fil Akhirati ilal jannati*. Maneno *fil Akhirati* (sawa na rai yangu) yeye ameongeza kwa sababu ya itikadi yake hii kwamba pepo inapatikana katika Akhera tu, waila katika lugha maana yake ni *Al-Hidayatu ilal Jannah* tu. Yaani, mtu atapata kusudio lile aliloambiwa kulipata. Hivyo, Mwenyezi Mungu Alisema ndani ya Kurani Tukufu kwamba pepo hii siyo katika maisha ya Akhera tu, bali hupewa katika maisha haya ya kidunia pia. Mwenyezi Mungu alikuwa Amesema sehemu hii kwamba Twaiimarisha Baitullah na Twaziandaa njia za kuihifadhi, kwani sehemu hii umati mmoja utapata

kuzalika ambao utapata thawabu na ujira na kujaaliwa radhi ya Mwenyezi Mungu wasiyopata watu wa mataifa ya zamani. Yaani, natija bora zaidi inayoweza kuwa za amali njema za mtu, natija hii hii itakuwa ya amali za umati huu, kwani sheria walipopewa ni kamilifu timilifu kwa kila jiha. Sheria walizopewa watu wa zamani, zilikuwa pungufu kwa kulinganishwa na sheria hii, hivyo hata kama zingetekezwa kikamilifu, natija yake, kiakili, haingeweza kuwa sawa na amali ifanywayo chini ya sheria iliyo kamilifu kwa kila jiha. Basi, Mwenyezi Mungu Amesema sehemu hii *Hudan lil'alamiin*. Chemchem ya sheria ya duniani kote itakayobubujika kutoka katika Nyumba hii, kwa kuitekeleza mtu atapata *Al-jannah*, pepo kamilifu ndani ya dunia hii pia na huko Akhera vilevile. Basi, kusudko la tatu (linalogawanyika tena katika shabaha zingine) la kujenga Baitullah ni mwongozo kwa walimwengu.

Kusudio la nne la ujenzi wa Nyumba hii lililoelezwa ni hili kwamba hii ndiyo *Aayaat Bayyinaat*. Kwa kutalii Kurani Tukufu inajulikana kuwa Kurani Tukufu inamwahidi binadamu aina mahususi ya ishara bayana, au inatoa matabiri kuhusiana nazo. Kwangu mimi, ishara bayana katika sehemu hii haina maana ya kawaida, bali sehemu hii muradi wake ni zile ishara bayana zihusianazo na Nyumba hii ya kwanza iliyowekwa kwa watu wote, iliyo *Mubarakan*, nayo ni *Hudan lil'alamiin*. Baada ya kueleza hayo, Mwenyezi Mungu Akasema *Aayaatun Bayyinaatun*, iliyomaanisha sehemu hii kwamba zitakuwa

ishara bayana zitakazohusiana na Nyumba hii, na Nyumba hii itakuwa chanzo cha ishara na misaada ya kimbingu zitakazodumu milele. Zile ishara bayana walizopewa manabii wa zamani au wafuasi wao ziliisha kwa nyakati zao.

Kila umati, kati ya nyimati za zamani, kwa kuitafuta dalili ya kimantiki na isiyotuliza, ukadai kuwa haiwezekani kwamba mtu apate ukaribu Wake, wahyi Wake, ruya za kweli na kashfi Zake na bishara kuhusu siku zijazo. Hivyo, kila umati wa zamani ulijifungia milango ya ukaribu Wake. Mwenyezi Mungu Anasema kuwa lengo lenyewe ni kuimarisha umati wa Kiislamu kwa njia ya ujenzi wa Baitullah, ili kupitia umati huu ishara za Mwenyezi Mungu zidumu kudhihiri. Nao kwa kupata katika dunia matunda ya ishara zao na kupokelewa dua zao na kwa kutoa dhabihu zao, umati huu utaendlea kuithibitisha dunia kwamba Yupo Mungu Aliye hai Aleyiumba dunia hii; Yu Mungu Mwenye nguvu, Mungu Mrehemevu, Mwenye upendo. Yeye Hawapotezi waja wake wanaoinama mbele yake, bali Anaimarisha nao uhusiano. Ili kuimarisha heshima yao duniani na kuiambia dunia kuwa hawa ni waja wangu wapendwa, Anawafunulia Wahyi, Huwaonyesha ruya na kashfi, Huwapokelea dua zao. Na watu kama hao watadumu kuzaliwa katika umati huu wataoendelea kuthibitisha kwamba Mungu wetu Yu Mungu Hai, na wanaokuwa na uhusiano Naye wanapata ishara zilizo bayana.

Kusudio la tano lihusianalo na Baitullah ambalo Mwenyezi Mungu Amelieleza ni *Makami Ibrahim*. Hapa Mwenyezi Mungu Amesema kwamba tazameni, mja Wetu Ibrahim na wengi miongoni mwa wazao wake wakitengana na nafsi zao na kuzama ndani ya huba ya Mungu na mapenzi ya Mwabudiwa, kaulimbiu yao ilikuwa *Aslamtu Lirabbil 'alamiin* – nimejitupa kwa Mola wa walimwengu – na kuiwekea dunia mfano. Tumefanya mpango wa kusakiniwa kwa Baitullah ili kwa njia hii jamii ya wampendao Mungu iendelee kuzalika ambao wawe wenye kujipatia daraja ya kujipoteza ndani ya Mungu kwa kuondolea mbali mapazia yote na kutengana na mahusiano yote ya kidunia na kutupilia mbali matakawa yao yote na kutoa dhabihu ya matamania yao yote. Na wawe wenye kufanya ibada hii kwa njia bora sana na kwa ukamilifu, ambayo inahusiana na huba na kutokuwa na ubinafsi. Hadhrat Masihi Mau'udi^{as} amefafanua jambo hili akisema kuwa ibada ni ya aina mbili. Ibadat moja ni ile inayoimarika juu ya misingi ya unyenyekevu, na ibada nyingine ndiyo ile iimarikayo juu ya misingi ya mahaba na kutokuwa na ubinafsi. Sala yetu ndiyo ibada ya aina hii iliyoimarika juu ya unyenyekevu, kwani Nabii Mtukufu^{saw} amesema kwamba sala ndiyo dua, na kwa kuomba dua mtu analazimika kujinyenyekeza sana mno. Yule aliye na kiburi hata sawa na chembe mbele ya Mola Wake, dua yake haiwezi abadan kupokelewa. Basi sala zetu zinakuwa ibada hapo tu ambapo zinaimarika

kikweli juu ya unyenyekevu. Na kuna ibada nyingine isimamayo juu ya misingi ya mahaba na kutokuwa na ubinafsi. Ibada hii ya Hadhrat Ibrahim^{as} inayohusiana na ujenzi wa Kaaba, ihusikanayo na kuhifadhi Kaaba, ihusianayo na kuijitoa wakfu na wazao wake kwa Baitullah na kuiombea, hii ndiyo ibada yenye mahaba. Mahaba ya Mwenyezi Mungu na mapenzi yake aliyodhihirisha Hadhrat Ibrahim^{as} yalikuwa ni mfano ulioadimika. Mwenyezi Mungu Anasema kwamba hii ndiyo *makami Ibrahim*. Kutoka hapa Tutaumba umati wa malaki ya watu watakaopatikana katika kila zama. Na mkilinganisha dhabihu ya umati huu na dhabihu ya Hadhrat Ibrahim^{as}, hamtaikuta pungufu.

Kwa nguvu takatifu ya Nabii Mtukufu^{saw} kulikuwa hakuna budi kuzalika kaumu hii, lakini ili kuzagaza duniani athari za nguvu hii takatifu, msingi wa Kaaba uliwekwa upya tangu miaka elfu mbili na miaka mia tano. Sehemu hii Amesema sura ya kidhahiri ya vitendo vifanywayo katika hija, sura ya ibada hii yenyewe ndiyo ya namna ambayo inahusiana na mapenzi. Kwa mfano, kuna kuizunguka Kaaba. Sasa fikiria hii inapatikana katika mataifa yote kwamba ikiwa dhabihu ya uhai inapaswa kutolewa kwa mtu fulani, basi watu huwa wanamzunguka. Imeelezwa kuwahusu baadhi ya wafalme wetu ya kwamba mwanaye mfalme fulani alipougua, hapo bababke akamzunguka na kuomba dua kwamba umri wangu apewe mwanangu. Hivyo, kujitolea uhai huhusikana sana na kuzunguka. Kwa

Makusudio 23 Adhimu ya Ujenzi wa Baitullah

ufupi, Mwenyezi Mungu Anasema hapa kwamba kutoka katika sehemu hii itaumbwa kaumu itakayodumu kumzunguka Mpendwa wake na kubusu kizingiti Chake. Upande mmoja kaumu hii itadumisha kumbukumbu ya Hadhrat Ibrahim^{as}, na upande wa pili itadhihirisha nguvu takatifu ya Mtume^{saw} kwa shani kubwa. Basi Mwenyezi Mungu Akaiumba kaumu hii, si tu katika zama za awali, si tu katika waishio Bara Arabu, bali katika kila sehemu ya dunia, na ndani ya kila zama mpaka siku ya Kiama watakaokuwa na huba na mapenzi ya Ki-Ibrahim^{as} kwa ajili ya Mola wao nao wataendelea kutoa dhabihu za kila aina katika njia Yake.

②

**Uhusiano Wenye Uketo
wa
Makusudio ya Ujenzi wa Baitullah
na
Kutumwa kwa Mtume^{saw}**

Hotuba ya Ijumaa, 7 Aprili 1967,
Masjid Mubarak, Rabwah, Pakistan.

“Mwenyezi Mungu Akajengsha Nyumba moja kwa manufaa ya wanadamu wote, lakini hawa hawakutambua adhama yake. Matokeo yake, Nyumba hii ikatiliifika, hata alama zake zikafutika. Kisha Mwenyezi Mungu kwa kumfunulia wahyi Hadhrat Ibarahim^{as} akaainisha ile sehemu na kwa njia yake akajengsha upya, na ili kuihifadhi na kuiimarisha adhama yake Akafanya mpango huu kwamba Hadhrat Ibarahim^{as} awatoe wakfu wazao wake. Hivyo, wazao wake wakaendelea kwa muda mrefu kuihudumia. Na kwa huduma ya miaka elfu mbili na mia tano na kwa dua zao ikapatikana kaumu iliyokuwa na nguvu na vipaji vya kubeba majukumu mazito ya sheria kamilifu timilifu iliyokuwa kwa ajili ya dunia nzima.”

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ³

تَحْمُداً وَنُصَلِّيَ عَلَى رَسُولِهِ الْكَرِيمِ⁴

Baada ya kutoa Shahada mbili na A'udhu na kusoma Sura Al-Faatiha, Hudhurth akasoma aya zifuatazo za Kurani Tukufu:

إِنَّ أَوَّلَ بَيْتٍ وُضِعَ لِلنَّاسِ لَلَّذِي بِبَكَّةَ مُبْرَكًا وَهُدًى لِلْعَالَمِينَ ﴿١﴾ فِيهِ آيَاتٌ بَيِّنَاتٌ مِّمَّا قَامَ إِبْرَاهِيمُ ۖ وَمَنْ دَخَلَهُ كَانَ آمِنًا ۗ وَلِلَّهِ عَلَى النَّاسِ حِجُّ الْبَيْتِ حَيْثُ أَشْرَطَ إِلَيْهِ سَبِيلًا ۗ وَمَنْ كَفَرَ فَإِنَّ اللَّهَ غَنِيٌّ عَنِ الْعَالَمِينَ ﴿٢﴾
(Aali 'Imraan, 3:97-98)

وَإِذْ جَعَلْنَا الْبَيْتَ مَثَابَةً لِّلنَّاسِ وَأَمْنًا ۗ وَاتَّخِذُوا مِن مَّقَامِ إِبْرَاهِيمَ مُصَلًّى ۖ وَعَهِدْنَا إِلَىٰ إِبْرَاهِيمَ وَإِسْحَاقَ أَن طَهِّرَا بَيْتِيَ لِلطَّائِفِينَ وَالْقَائِمِينَ وَالرُّكَّعِ السُّجُودِ ﴿١٢٦﴾ وَإِذْ قَالَ إِبْرَاهِيمُ رَبِّ اجْعَلْ هَذَا بَلَدًا آمِنًا وَارْدُ قَوْمِي آهْلَهُ مِنَ الشُّرَكَاتِ مَنْ آمَنَ مِنْهُمْ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ ۗ قَالَ وَمَنْ كَفَرَ فَأُمَتِّعُهُ قَلِيلًا ثُمَّ أَضْطَرُّهُ إِلَىٰ عَذَابِ النَّارِ ۖ وَ يَأْسُ الْبَصِيرِ ﴿١٢٧﴾ وَإِذْ يَرْفَعُ إِبْرَاهِيمُ الْقَوَاعِدَ مِنَ الْبَيْتِ وَإِسْحَاقُ ۖ رَبَّنَا تَقَبَّلْ مِنَّا ۗ إِنَّكَ أَنْتَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ ﴿١٢٨﴾ رَبَّنَا وَاجْعَلْنَا مُسْلِمِينَ لَكَ وَمِن ذُرِّيَّتِنَا أُمَّةٌ مُّسْلِمَةٌ لَّكَ ۗ وَارِنَا مَنَاسِكَنَا ۗ وَتُبَّ عَلَيْنَا ۗ إِنَّكَ أَنْتَ التَّوَّابُ الرَّحِيمُ ﴿١٢٩﴾ رَبَّنَا وَابْعَثْ فِيهِمْ رَسُولًا مِنْهُمْ يَتْلُو عَلَيْهِمْ آيَاتِكَ وَيُعَلِّمُهُمُ الْكِتَابَ وَالْحِكْمَةَ وَيُزَكِّيهِمْ ۗ إِنَّكَ أَنْتَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿١٣٠﴾

(Al-Baqara, 2:126-130)

Kisha akasema:

Nimeishatoa hotuba kadhaa juu ya maudhui fulani ya muhimu ambayo kwa ufupi ni kwamba Mwenyezi Mungu Akajengesha Nyumba moja kwa manufaa ya wanadamu wote, lakini hawa hawakutambua adhama yake. Matokeo yake, Nyumba hii ikatilifika, hata alama zake zikafutika. Kisha Mwenyezi Mungu kwa

³ Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwingi wa na Ukarimu.

⁴ Twamhimidi Yeye na kumsalia Mtume Wake mhashamu.

kumfunulia wahyi Hadhrat Ibarahim^{as} akaainisha ile sehemu na kwa njia yake akaijengsha upya, na ili kuihifadhi na kuiimarisha adhama yake Akafanya mpango huu kwamba Hadhrat Ibrahim^{as} awatoe wakfu wazao wake. Hivyo, wazao wake wakaendelea kwa muda mrefu kuihudumia. Na kwa huduma ya miaka elfu mbili na mia tano na kwa dua zao ikapatikana kaumu iliyokuwa na nguvu na vipaji vya kubeba majukumu mazito ya sheria kamilifu timilifu iliyokuwa kwa ajili ya dunia nzima.

Kisha niliwaambia kwamba ndani ya aya nilizosoma, Mwenyezi Mungu Ametaja shabaha na makusudio ishirini na matatu yanayohusiana na ujenzi wa Baitullah, na kupata makusudio haya yote kuhusiana na kutumwa kwa Nabii^{saw}. Miongoni mwa makusudio haya, niliwaeleza ndugu makusudio matano katika hotuba iliyopita. Mosi, Nyumba hii *Wudhi'a Linnasi*, imejengwa kwa manufaa ya wanadamu wote. Pili, *Mubarkan*, ndani yake mna sifa ya kuwa yenye baraka, kidunia pia na kiroho vilevile. Ya tatu, *Hudan lil'alamiin*, Twataka kuifanya kuwa njia ya mwongozo kwa walimwengu wote. Na katika maana zote nne za mwongozo, Mwenyezi Mungu akaifanya kuwa makao makuu ya mwongozo kwa walimwengu. Ya nne, *fih Aayaatun bayyinatun*, yaani kutoka hapa ishara za kimbingu zitaanza kufululiza zitakazobaki salama hadi Kiama, na toka hapa itabubujika chemchem ya msaada wa kimbingu ambayo haitakauka abadan. Ya tano, ndani ya

maneno *Makamu Ibrahim* imehabarishwa ya kwamba ile ibada iliyoimarishwa juu ya msingi wa mahaba na kutokuwa na ubinafsi, hii – *Makamu Ibrahim* – itakuwa ni kitovu chake, na kutakuwa na kaumu moja itakayowakilisha mataifa yote, itapatikana katika zama zote, ambayo itakuwa imejaa kabisa, kama Hadhrat Ibrahim^{as}, mapenzi ya Mwenyezi Mungu yaunguzayo dhambi zote, na njia za kumkaribia Mwenyezi Mungu zitadumu kufunguliwa kwake.

Hayo ndiyo makusudio matano niliyoeleza kwa kirefu katika hotuba ya Ijumaa iliyopita. Kwa kuwa nitalirejea kila moja katika hayo matano kwa kuthibitisha kwamba kila mojawapo linahusiana na kutumwa kwa Mtume^{saw} na kwamba hilo likapatikana kwa njia na sura gani, hivyo nimenuia leo kuyaeleza makusudio hayo kwa kifupi sana. Nitajaribu kuyaeleza katika hotuba ya leo yote yaliyosalia miongoni mwa makusudio ishirini na matatu, lakini itakuwa Atakayopenda Mungu.

Mwenyezi Mungu Anasema *man dakhalahuu kaana Aaminan*. Kusudio la sita la ujenzi wa Baitullah ni hili kwamba yeyote atakayeingia, yaani kila mmoja atakayefanya zile ibada zihusianazo na Baitullah, mtu huyo atakuja ndani ya hifadhi ya Mungu, atakingwa na jahanamu ya dunia na Akhera, na dhambi zake zote zilizopita zitasamehewa. Hivyo, kusudio la sita la ujenzi wa Baitullah ni kwamba Nyumba moja ya Mungu ijengwe ambayo baadhi ya ibada zihusiane nayo. Na

Makusudio 23 Adhimu ya Ujenzi wa Baitullah

mtu yeyote atakayetokeleza ibada hizi kwa nia halisi na kwa ukamilifu utimilifu, huyo anaahidiwa na Mwenyezi Mungu kusamehewa dhambi zake zote za zamani na atakingwa na moto wa jahanamu.

Kusudio la saba la ujenzi wa Baitullah Aliloeleza Mwenyezi Mungu ni *wa lillahi 'alannaasi hijjul Baiti*. Sio faradhi ya wazao wa Ibrahimu^{as} au Waarabu tu kufanya hija ya Baitullah, bali kusudio hasa ni kwamba mataifa yote ya dunia yajumuike sehemu hii kwa hija. (Nafikiri kuwa shabaha hizi na makusudio haya yote alikwisha ambiwa Hadhrat Ibrahimu^{as} wakati wa ujenzi wa Baitullah, kwani karina nyingi madhubuti zipo kuhusu jambo hili ndani ya Kurani Tukufu). Almuradi, Hadhrat Ibrahimu^{as} aliambiwa kwamba hii ndiyo Nyumba ya Mwenyezi Mungu ambayo mataifa yote ya dunia yatakayoniadini Mimi na Mtume^{saw} Wangu na kwa kufanya Baiati kwa mkono wa Khatamun Nabiyyina^{saw} yataweka nira ya utii Wangu shingoni mwao, wote hao watafaradhishwa kufanya hija ya Baitullah, na kwa njia hii sehemu hii itafanywa kuwa mahali pa kuendewa na mahulukuku na ulimwengu.

Shabaha ya nane, au kusudio la nane la ujenzi wa Baitullah lililoelezwa ni *mathaabatan*. Ndani ya neno hili imeashiriwa kwamba mataifa ya dunia yamegawanyika makundi kwa makundi, na wakati mfarakano huu utakapofikia upeo wake ndipo atatumwa Mtume atakayekuwa mwenye kutimiza kusudio hili la Baitullah

na kuyajumuisha mataifa haya mbalimbali kwenye makao makuu, na atawaleta katika dini moja. Hivyo, hapa imesemwa kwamba ingawaje mifarakano itafikia kilele chake wakati fulani, lakini ni utashi wa Mwenyezi Mungu kumtuma wakati ule Mtume atakayeyafanya mataifa yote kuwa umati mmoja.

Kusudio la tisa lililoelezwa hapa ni *Amnan*. Yaani, Nyumba hii ni amani kwa watu. Sehemu hii, neno hili lamaanisha kwamba Sisi Tumetaka kuifanya Nyumba hii kwamba kwa njia yake, na kwa njia yake tu, dunia itapata amani. Kwani, itakuwa ni Nyumba hii pekee inayoweza kuitwa Baitullah. Kwa kutengana nayo na kutojali mafundisho yake, chama chochote cha dunia kikijaribu kuimarisha amani duniani kitajikuta kimeshindwa. Dunia yaweza kupata amani ya kweli kwa kutekeleza mafundisho yale tu atakayoitolea dunia yule Nabii atakayeinuliwa kutoka katika Kaaba.

Kwa kulingana na maana ya pili ya *Amn*, neno *Amnan linnasi* pia lamaanisha kwamba dunia itaweza kupata kiruhania utulivu wa moyo kwa kuungana na ile sheria ya mwisho itakayodhihiri huko Makka na itakuwa inayaita mataifa yote ya ulimwengu kwenye Mola wao. Na kwa kuwa mtu hupata utulivu wa moyo hapo tu ambapo mafundisho yawe yenye kutimiza mahitaji yake ya asili, na yawe yaongozayo na kuzikua nguvu zote na vipawa vyote Alivyomjaalia Mwenyezi Mungu, basi Amesema hapa kwamba Makka itakwa ni nyumba ya

mafundiho yatakayokuwa yenye kuipatia dunia kikweli utulivu wa moyo. Maana hizi zote mbili zinafaa hapa. Kwanza, kama dunia yaweza kubahatika kupata amani, hiyo ni kupitia Makka. Pili, roho za dunia kama zikiweza kupata utulivu wa moyo, akili za dunia kama zikipata utulivu, basi ni kwa njia ya mafundiho yale yatakayoteremka Makka.

Shabaha ya kumi na kusudio la kumi la Kaaba Aliloeleza Mwenyezi Mungu katika aya hizo ni *Ittakhidhuu min makami Ibrahim Musalla*. Katika aya iliyotangulia *Makami Ibrahim* ilitajwa. Hii ilimaanisha kwamba mahali hapa ni Nyumba ambapo msingi umewekwa wa ile ibada ya kweli itiririkayo kutoka ndani ya chemchem ya mapenzi, kutokuwa na ubinafsi, na upendo wa Mungu. Na katika *ittakhidhuu min makami Ibrahim musalla* imetajwa ile ibada inayobubujika kutoka katika chemchem ya unyenyekevu.

Kwa ufupi, Mwenyezi Mungu Amesema sehemu hii kwamba shabaha moja ya ujenzi wa Baitullah ni hii kwamba iumbwe kaumu ambayo iwe inafanya ibada ya Mola wake kwa kujinyenyekeza sana na iimarisha duniani kote vivuli vya daraja ya Hadhrat Ibrahimu^{as} kwa ajili ya ibada yenye unyenyekevu na iimarisha vituo vya kuzagaza Islam.

Kusudio la kumi na moja la ujenzi wa Baitullah lililoelezwa ni *Tahhiraai Baitiya*. Ndani yake tumeambiwa kwamba utashi wa Mwenyezi Mungu ni kwamba kwa

kujifunza kuweka usafi wa dhahiri na batini, Kaaba ifanywe kuwa chuo kikuu na makao makuu.

Kusudio la kumi na mbili limeelezwa kuwa ni *Littaaifiina*, yaani wawakilishi wa mataifa yote ya ulimwengu watajumuika hapa mara kwa mara. Hadhrat Ibrahim^{as} alikwishaambiwa na Mwenyezi Mungu tangu miaka 2500 kwamba wajumbe wa mataifa yote ya ulimwengu wataendelea kufika hapa mara kwa mara kwa kuizunguka Kaaba na kutimizi shabaha zile pia zihusianazo na Kaaba.

Kusudio la kumi na tatu lililoelezwa ni *Wal'akifiina*. Kaaba inajengeshwa kwa shabaha hii kwamba kupitia hii izalike kaumu ya watu watakojitolea wakfu maisha yao katika njia ya Mwenyezi Mungu na kwa njia hii watakuwa wenye kutimiza makusudio ya Baitullah.

Kusudilo la kumi na nne ni kwamba Mwenyezi Mungu Anataka *war-rukka'is-sujuud*, yaani iumbwe kaumu ambayo iimarike katika imani ya Umoja wa Mungu, ambayo ipitishwe maisha yake katika kumtii Mwenyezi Mungu na kujitupa Kwake.

Kusudio la kumi na tano ndilo *Baladan Aaminan*. Neno *Amn* limetumika katika aya hizi kwa kueleza shabaha tatu mbalimbali. Katika sehemu hii Mwenyezi Mungu Anasema kuwa Sisi Tutaihifadhi Nyumba hii na mashambulizi ya kidhuluma ya dunia. Shambulio lolote litakalofanywa kuifutilia mbali Kaaba halitafaulu, bali washambulizi wataangamizwa ili dunia itambue kuwa

yule Nabii Tunayetaka kumtuma toka hapa, huyo naye atakuwa katika hifadhi ya Mwenyezi Mungu, na nguvu yoyote haitaweza kumhilikisha au kuifanya misheni yake ishindwe, na ili dunia itambue pia kuwa ile sheria atakayopewa Nabii huyo maasumu itadumu milele, na Mwenyezi Mungu Mwenyewe Ataihifadhi.

Kusudio la kumi na sita linaloambatana na Kaaba ni *warzuk Ahlahu minath Thamaarati*. Ndani yake Mwenyezi Mungu Ametuambia kwamba Ninaijengesha Baitullah upya kwa shabaha hii pia kwamba dunia ikishuhudia Baitullah na baraka zake itambue kwamba wale watu wanaojifia katika njia ya Mwenyezi Mungu na wakiwa Wake wanajitolea mhanga katika njia yake na kwa kutengana na dunia wanakuwa Wake, amali zao hazipotei bure, bali wanapata matunda matamu na natija bora sana za amali zao za kujinyenyekeza na za upendo wa Mungu zinakadiriwa kwa ajili yao.

Kusudio la kumi na saba la kuimarisha Baitullah ni *Rabbanaa Takabbal minnaa*. Yaani, shabaha moja ya ujenzi wa Baitullah ni kwamba ili dunia ielewe na kutambua kwamba njia ya kujipatia daraja za juu za ruhaniania ni dua pekee. Katika kuomba dua, mtu anapofikia upeo wa kujinyenyekeza na kutiririsha machozi, na hali ya mauti inazalike, ndipo fadhili ya Mungu huteremka toka mbinguni na mja anafunguliwa njia za maarifa.

Ilmuradi, hapa Mwenyezi Mungu Ameeleza shabaha ya kuimarisha Baitullah ni kwamba hapo itazalika kaumu ambayo itaomba dua pamwe na masharti yake yote, na katika dua itawafikia hali ya mauti na uwepo wake utatoweka fika na ukigeuka kuwa maji utatiririka kizingitini pa Mola. Nao watakuwa wamefahamu kuwa hatuwezi kujipatia kitu kwa sababu ya amali zetu (amali tupu) hadi tuvute fadhili ya Mwenyezi Mungu kwa njia ya dua. Hivyo, baada ya kutoa dhabihu zote wataziona dhabihu zao si chochote wala lolote. Saa zote wataendelea kumcha Mungu na kutetemeka. Na juu ya dhabihu zote zile, dua yao itakuwa ni hii kwamba yale tunayopeleka mbele Yako ni hedaya hakiri mno. Shani Yako imetukuka sana, nasi twafahamu kuwa hedaya yetu hii haifai kukubalika. Lakini U Mola Mrehemevu sana, tupokelee hedaya yetu hii duni na Uiangalie mighafala yetu na juhudi zetu hakiri kwa jicho la maghufira, na tuandaalie njia ya kupata rehema zako ili jitihada na bidii zote zipokelewe nawe. Ilmuradi, kwa kuiumba kaumu ya aina hii, Mwenyezi Mungu Akaweka msingi wa Kaaba.

Mwenyezi Mungu Anasema kwamba kusudio la kumi na nane la kujenga upya Kaaba ni hili kwamba dunia itambue ya kuwa wale watu wanaomwomba Mwenyezi Mungu kwa njia hii ndio wanaoshuhudia maonyesho ya sifa *Samii'* ya Mola wao. Kisha dunia inaona kuwa Mola wetu ndiye Asikiaye. Yuasikia dua zetu na Anasema, Nimesikia maombi yenu. Basi natija ya kuimarisha

Kaaba ni kwamba dunia itapata utambuzi wa Mungu Aliye *Samii'*.

Kusudio la kumi na tisa ni kwamba dunia ipate maarifa ya Mungu Aliye Mjuzi – *'Aliim*. Haitakuwa kwamba mtu kwa kupungukiwa ujuzi ameomba dua fulani na Mwenyezi Mungu Akakubali; sivyo, bali mtu atakapomba dua na ataifikisha hadi upeo wake, basi Mwenyezi Mungu Ataipokea lakini sawa na muktadha wa elimu Yake ya ghaibu, yaani Ataikubali namna inavyotakikana kukubali. Kutokubalika kwa baadhi ya dua, au kutokukubalika kwa sura iliyoombwa hakutathibitisha kuwa Mungu siye *Samii'* au si Mweza, bali kutahakikisha kuwa Mwenyezi Mungu ndiye *'Allaamul Ghuyuub* – Mjuzi wa mambo ya ghaibu. Hivyo, msingi wa Kaaba umewekwa ili waja wa Mungu wamtambue Mungu Mjuzi na kumjua na kumwelewa.

Kusudio la ishirini limeelezwa kwamba ni *wamin dhurriyyatinaa ummatan Muslimatan laka*, yaani Uujaalie *ummatan Muslimatan* uwe kutoka katika dhuria zetu. Mwenyezi Mungu Amesema sehemu hii kwamba kusudio letu ni kuwa Muhammad^{saw} atakapotumwa kwa dunia, kaumu yake iwe na kipawa cha kuwa *ummatan muslimatan* – umati unaojitupa kwa Mungu – na kwa sababu ya dua za Ibrahimu^{as} itakuwa *ummatan Muslimantan*. Hii pia inamaanisha kuwa Yule Nabii aliyehidiwa atazaliwa ndani ya Makka, lakini endeleeni kuomba kwamba kwa sababu ya mghafala au kasoro

yetu isije Yule Nabii akatokea miongoni mwa kaumu nyingine kwa sababu ya sisi kutostahili machoni Mwako kutimiziwa ahadi hii. Hivyo, akasema hapa kwamba Uwajaalie wazao wangu kuwa *ummatan Muslimatan*, wawe wa kwanza kuhubiriwa, nao wote wawe wenye kumpokea pia.

Basi, imesemwa sehemu hii kwamba ule umati utakaozaliwa kutokana na dhuria za Hadhrat Ibrahim^{as} na Hadhrat Ismaili^{as}, huo uwe umati *Muslima*, usimkatae Nabii Yule, bali ukimwamini uwe na nguvu na uwezo wa kutekeleza majukumu utakayotwishwa. Mwenyezi Mungu Anasema kuwa Sisi Twataka kuwafanya wawe kaumu ya aina hii, na ndiyo maana Tumejengsha upya Kaaba.

Kusudio la ishirini na moja lililoelezwa sehemu hii ni *Arinaa manaasikanaa*. Ndani yake imeashiriwa kwamba atazaliwa Mtume ndani ya Makka atakayetumwa kwa dunia nzima wakati dunia baada ya ukuaji wake wa ruhania na akili itakapokuwa imefikia daraja ya kuibeba sheria kamilifu timilifu, sheria ambayo ikilinganishwa na sheria za zamani inafaa katika mazingira yote, sheria ifundishayo kutenda matendo yafaayo na hali, sheria itimizayo mahitaji ya mataifa yote na zama zote. *Arinaa manasikanaa* yamaanisha kwamba mambo yafaayo, ibada na majukumu yetu, Utuonyeshe na kutufundisha, yaani Ututeremshie sheria ya Kurani.

Hivyo, tumeambiwa katika *Arinaa manaasikanaa* kwamba yule Mtume^{saw} atakapowasili, atahusikana na mataifa yote ya dunia na zama zote. Basi, mwendelee kuomba: Ee Mola wetu, kwa sababu ya mahitaji na tabia tofauti za mataifa mbalimbali na matatizo tofauti ya zama mbalimbali Utuletee sheria kamilifu timilifu itakayotimiza mahitaji ya kitabia ya kila kaumu, na iwe ya kuyatatua matatizo ya kila zama na ibaki hai mpaka Kiama, ili litimie kusudio lile lililosababisha kuweka msingi wa Kaaba.

Kusudio la ishirini na mbili Alilolieleza Mwenyezi Mungu ni *Tub 'alaina*. Ndani yake imeelezwa kwamba sheria ile ya mwisho itakayoteremshwa hapa itahusiana sana na Mola Aliye *Tawwaab*. Wafuasi wa sheria hii watatambua kweli hii kwamba pasipo toba na maghufira haiwezekani kupata maarifa. Hivyo, watakuwa wanatoa pia mara kwa mara dhabihu katika njia hii na vilevile wataelekea Kwake na kusema, 'Ee Mungu, tusamehe makosa yetu.' Hao watakuwa ni watu ambao baada ya kufanya wema pia wataendelea na hofu isije ikabaki kasoro katika wema wetu na kumkasirisha Mola wetu; hivyo hawa watadumu kuomba ghofira na kutubu daima dawamu.

Kusudio la ishirni na tatu, Amesema Mwenyezi Mungu, ni *Rabbanaa wab'ath fihim Rasulan minhum*, yaani Sisi Twataka kuifanya sehemu hii kuwa mahali pa kuzaliwa Muhammad (Mtume^{saw} wa Mungu). Twataka kupafanaya

mahali ambapo Tutamtuma mja wetu mmoja na kumpa daraja ya kusifiwa sana – daraja ya Ki-Muhammad – ikiwa ni natija ya maombi yaliyofanywa katika mazingira yake kwa unyenyekevu na kutiririsha machozi kwa huba na mapenzi. Na kwa njia yake sheria moja itaimarishwa na kuumbwa umati utakaokuwa na ishara zilizo hai. *Yatluu ‘alaihim Aayaatika*, na watajihusisha na Mungu Aliye Mzima na Nabii aliye hai na sheria iliyo hai. Na watafundishwa sheria kamilifu. Lakini hawataambiwa waambiwavyo watoto wasiofahamu kwamba ‘Tunasema, basi mkubali tu’, bali Mwenyezi Mungu kwa kuona lubu na busara yao Atawaambia hekima za maamrishi Yake kupitia Nabii huyo. Nao watajaliwa utakaso jinsi ambavyo kaumu yoyote hapo kabla haikupata utakaso kama huo. Na hii ndiyo hakika hata akili yetu pia hukubali. Kwani, kama nyimati za hapo kabla ziliteremshiwa sheria pungufu, na kwa sababu ya mwongozo mpungufu zilipata utakaso, basi utakaso huo si mkamilifu. Utakaso waliopata wa hapo kabla ingawaje ulilingana na tabia yao na vipawa vyao na uwezo wao, lakini sio mkamilifu, kwani mafundisho waliyopewa hayakuwa kamili kwa sababu uwezo wao ulikuwa bado haujakamilika. Kisha ilipopatikana kaumu iliyokuwa na uwezo wa kubeba sheria kamili, basi mionogni mwao waliopitisha maisha yao kwa kutoa dhabihu kubwa kabisa na kwa kumcha Mwenyezi Mungu wakitekeleza maamrishi yake yote na kuepukana na makatazo yote watapata utakaso wa nafsi

Makusudio 23 Adhimu ya Ujenzi wa Baitullah

(kwa fadhili za Mungu na si kwa sababu ya amali zao) ambao utakuwa ni usafi kamili na utakaso kamili, na furaha na radhi ya Mwenyezi Mungu wasiyoipata radhi kama hii watu wa mataifa ya zamani.

Basi, Mwenyezi Mungu Anasema sehemu hii kwamba kusudio la ishirini na tatu la kuimarisha Baitullah ni kwamba atumwe duniani Mbora^{saw} wa Mitume, na tena apatiwe binadamu daraja ya juu ambayo aliumbwa kuipata.

Twamwomba Mwenyezi Mungu Atujumishe kwa fadhili yake na waja hao, kwani sisi tu wanyonge mno na vinyangarika, wenye makosa na wenye dhambi, tusiofahamu tumenasa katika matamania ya nafsi. Lakini Akipenda Yeye na tukiteremkiwa na fadhili Yake, Yeye Aweza kutuondoa katika uchafu na kutufikishia daraja zile za juu za utakaso Alizouahidia umati wa Mtume^{saw}.

Katika hatuba zijazo, Mungu Akijalia, nitaeleza kwa kirefu shabaha na makusudio haya 23 jinsi yalivyotimia kwa njia ya Nabii Mtukukufu^{saw}. Ninawasogeza asteaste kwenye upande nilioashiria kwao hapo kabla pia kwamba Mwenyezi Mungu Amenielekeza kwenye jambo moja la muhimu, na mkakati ule ni wa muhimu kwa ulezi wa Jumuiya.

Kwa vyovyote, naendelea kujaribu kuwatayarisheni kifikira. Lakini, ni nani miye, na athari gani unayo mdomo wangu, mpaka Mwenyezi Mungu Atie athari

Makusudio 23 Adhimu ya Ujenzi wa Baitullah

katika usemi wangu na kuzijalia nyoyo zenu kupokea athari hiyo! Hivyo endeleeni kuomba dua. Mimi nami naendelea kuomba. Mwenyezi Mungu Aijalie Jumuiya yetu, kwa fadhili zake, kufanya ile kazi Ambayo Aliimarisha Jumuiya kuitekeleza.

(Gazeti la Al-Fadhl, 30 Aprili 1967)

③

**Manufaa ya Kidini na Kidunia
ya
Mataifa Yote ya Ulimwengu
Yameambatanishwa na Baitullah**

Hotuba ya Ijumaa, 21 Aprili 1967,
Masjid Mubarak, Rabwah, Pakistan

“Kusudio la kwanza la kuimarisha Baitullah Amelieleza Mwenyezi Mungu katika maneno *Wudhi’a Linnasi*. Yaani, Nyumba hii ya Mungu inajengeshwa upya kwa mkono wa Hadhrat Ibrahimu^{as}, ili manufaa ya kidini na ya kidunia ya mataifa yote ya ulimwengu yaambatanishwe na Baitullah.”

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ⁵ تَحْمَدُهُ وَنُصَلِّي عَلَى رَسُولِهِ الْكَرِيمِ⁶

Baada ya kutoa Shahada mbili na A‘udhu na kusoma Sura Al-Faatiha, Hudhur^{rh} akasoma aya zifuatazo za Kurani Tukufu:

إِنَّ أَوَّلَ بَيْتٍ وُضِعَ لِلنَّاسِ لَلَّذِي بِبَكَّةَ مُبَارَكًا وَهُدًى لِّلْعَالَمِينَ ﴿٥﴾ فِيهِ آيَاتٌ بَيِّنَاتٌ مَّقَامُ إِبْرَاهِيمَ ۖ وَمَنْ دَخَلَهُ كَانَ آمِنًا ۗ وَلِلَّهِ عَلَى النَّاسِ حِجُّ الْبَيْتِ حَيْثُ أُبَيِّنَ مَن اسْتَطَاعَ إِلَيْهِ سَبِيلًا ۗ وَمَن كَفَرَ فَإِنَّ اللَّهَ غَنِيٌّ عَنِ الْعَالَمِينَ ﴿٦﴾
(Aali‘ Imraan, 3:97-98)

وَإِذْ جَعَلْنَا الْبَيْتَ مَثَابَةً لِّلنَّاسِ وَأَمْنًا ۗ وَاتَّخِذُوا مِن مَّقَامِ إِبْرَاهِيمَ مُصَلًّى ۖ وَعَهِدْنَا إِلَىٰ إِبْرَاهِيمَ وَإِسْمَاعِيلَ أَنَّ طَهِّرَا بَيْتِيَ لِلطَّائِفِينَ وَالْقَائِمِينَ وَالرُّكَّعِ السُّجُودِ ﴿١٠﴾ وَإِذْ قَالَ إِبْرَاهِيمُ رَبِّ اجْعَلْ هَذَا بَلَدًا آمِنًا وَارْدُ قُرْبَىٰ أَهْلَهُ مِنَ التُّهَّاتِ ۖ مَنْ آمَنَ مِنهُم بِاللهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ ۖ قَالَ وَمَن كَفَرَ فَأُمَتِّعُهُ قَلِيلًا ثُمَّ أَضْطَرُّهُ إِلَىٰ عَذَابِ النَّارِ ۖ وَبِئْسَ الْمَصِيرُ ﴿١١﴾ وَإِذْ يَرْفَعُ إِبْرَاهِيمُ الْقَوَاعِدَ مِنَ الْبَيْتِ وَإِسْمَاعِيلُ ۖ رَبَّنَا تَقَبَّلْ مِنَّا ۖ إِنَّكَ أَنْتَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ ﴿١٢﴾ رَبَّنَا وَاجْعَلْنَا مُسْلِمِينَ لَكَ وَمِن دُونِنَا أُمَّةٌ مُّسْلِمَةٌ لَّكَ ۗ وَارِنَا مِن مَّناسِكَنا وَتُبْ عَلَيْنَا ۖ إِنَّكَ أَنْتَ التَّوَّابُ الرَّحِيمُ ﴿١٣﴾ رَبَّنَا وَابْعَثْ فِيهِم رُسُلًا فَمَنَّهُم بَيَّنُّوا عَلَيْهِمُ الْبَيِّنَاتِ وَيُعَلِّمُهُمُ الْكِتَابَ وَالْحِكْمَةَ وَيُزَكِّيهِمْ ۗ إِنَّكَ أَنْتَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿١٤﴾

(Al-Baqara, 2:126-130)

Kisha akasema:

Niliwaambia katika hotuba mbili zilizopita kwamba ndani ya aya nilizosoma kabla ya hotuba hizo, na leo pia nimezisoma, Mwenyezi Mungu Ametaja makusudio 23 yanayohusiana na Baitullah, na ambayo kupata haya makusudio huhusikana na kutumwa kwa Mtume^{saw}. Ingawaje ahadi hizi zote Alipewa Hadhrat Ibrahimu^{as} miaka karibu 2500 kabla ya Mtume^{saw} kutumwa, lakini

⁵ Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwingi wa na Ukarimu.

⁶ Twamhimidia Yeye na kumsalia Mtume Wake mhashamu.

habari hizi, ahadi hizi, bishara hizi, kwa hakika zilitimia na makusudio haya yote yalipatikana wakati Nabii Mtukufu^{saw} alipotumwa kwa dunia na sheria ya Kurani Tukufu ikateremka toka mbinguni.

Kusudio la kwanza la kuimarisha Baitullah Aliloeleza Mwenyezi Mungu katika aya hizi, kama nilivyosema katika hotuba ya kwanza, ni *wudhi'a linnaasi*. Nyumba hii ya Mungu inajengeshwa upya kwa mkono wa Hadhrat Ibrahimu^{as} ili manufaa ya mataifa yote ya kidini na ya kidunia ya ulimwengu yahusishwe na Baitullah. Ni dhahiri kwamba zama za miaka 2500 zilizopita baina ya Hadhrat Ibrahimu^{as} na Mtume^{saw} kuhusu hizo ilikuwa haiwezi kusemwa kwamba mataifa yote ya ulimwengu yananufaika kidini na kidunia kutoka katika Baitullah. Kulikuwa na mataifa mengi wakati huo yasiyojua Baitullah au jiografia ya Makka. Mataifa mengi hayakuwa na upendo moyoni mwao kwa Baitullah, hayakuvutika kwake. Hayakuiheshimu wala kuitukuza. Hayakuyakini kwamba baadhi ya baraka na neema zinahusiana na Baitullah ambazo tukizijua na kuzitambua twaweza kujipatia sehemu za baraka hizo na neema hizo. Lakini alipodhihiri Mtume^{saw}, hapo Nyumba hii hii, iliyoisahau dunia, ikaitambua dunia na kuelewa baraka zake, na moyoni mwa dunia, kifuni mwa mataifa, mkazalika mapenzi yake, na zikaanza kutimia ahadi zote ambazo Mola wa Hadhrat Ibrahimu^{as}, Mola wa Muhammad^{saw}, Mtume wa Mungu, Mola wetu, Alikuwa Amemwahidi Hadhrat Ibrahimu^{as}.

Sasa nitawaambia namna gani ahadi hii (*wudhi'a linnaasi*) ilitimia kupitia Nabii Mtukufu^{saw} na kwa sura ipi. Kwa kuwa ahadi hii ilikuwa kwa ajili ya mataifa yote, na ahadi yenyewe ilikuwa kwamba wanadamu wote watapata baraka toka kwa Makka, basi ni dhahiri kwamba kiakili haiwezekani kutimia ahadi hii pasipo kuteremka sheria kamilifu, hivyo kulikuwa hakuna budi kuteremka sheria kamili ya Kurani Tukufu kabla ya ahadi hii kutimia. Kurani Tukufu imedai kuwa *Dhaalikal Kitabu* (Sura Al-Baqara 2:3), yaani Kurani hii ni sheria kamilifu timilifu. Na kuhakikisha madai haya ikalta dalili kwamba *la raiba fihi* – hamna shaka ndani yake. Nomino *Raib* inazo maana nne zinazohusikana na sehemu hii. Kutokana na maana hizi, tumeambiwa hoja nne za kuthibitisha kwamba kwa kweli Kurani hii, na Kitabu hiki, kimekamilika na kutimilika kwa kila jiha.

Kutokana na maana moja ya *raib*, sifa ya Kurani Tukufu ndiyo kwamba hiki ni Kitabu pekee kikamilifu kitimizacho mahitaji ya binadamu ya kiruhania na kimwili, ya jamii na huluka, ya iktisadi na siasa, na hiki ndicho Kitabu kitimizacho haja zote za kweli za tabia ya asili ya binadamu, kwani hii inathibitisha haja yake na ukweli wake kwa sifa zake kamilifu na fadhila zake na mafundisho yake yasiyo na kifani. Kama niichukulie dalili hii tena kuwa dai moja na kuanza kufafanua hoja zake, hii itachukua muda mrefu. Waifahamuo Kurani Tukufu kiasi fulani pia wanajua kwamba dalili za Kurani Tukufu na fadhila zake na mafundisho yake

yasiyo na kifani vinathibitisha ubora wake juu ya Vitabu vyote vya zamani.

Hadhrat Masihi Mau'udi^{as} alipoulizwa kuhusu Vitabu vilivyofunuliwa vya Bani Israeli kwamba maadamu hivi vipo kulikuwa na haja gani ya Kurani Tukufu, akajibu: Msiitaje Kurani Tukufu nzima; hiki ndicho Kitabu chenye wasaa mwingi, ndani mwake mna elimu nyingi. Mwanzoni mwake kuna Sura Al-Faatiha, ndani yake mna maarifa mengi na dalili za haki. Kama mkituonyesha maarifa na dalili kwa mkabala wa maarifa na dalili za Sura Al-Faatiha, tutafahamu kwamba Vitabu vyenu vinaweza kuthubutu kuikabili Kurani Tukufu. Muda mrefu umeishapita tangu mwito huu ulipotolewa. Katika dini ya Katoliki Papa wengi wamepita, mmoja baada ya mwingine, nao walikuwa ni viongozi wa Kanisa la Katoliki, kadhalika yapo madhehebu mengine ya Wakristo, lakini Kiongozi yeyote miongoni mwao hakuweza kutoa dalili kama hizo kutoka katika Vitabu vyao vya kimbingu kuikabili Sura Al-Faatiha, ambazo Hadhrat Masihi Mau'udi^{as} alidai kwamba sisi tutazitoa kutoka ndani ya Sura hii kuwaonyesheni.

Basi, *La raiba fihi* maana yake moja ni kuwa hiki ni Kitabu kiwezacho kuthibitisha haja yake na ukweli wake kwa sifa zake kamilifu na fadhila zake na mafundiho yake yasiyo na kifani. Na alipoulizwa kuwa kulikuwa na haja gani ya Kurani Tukufu, likatolewa lile jawabu, na katika jawabu hilo mwito uliotolewa ili kuamua swala

hili, hadi leo viongozi wa madhehebu ya Wakristo hawajakubali. Kwa hiyo, imehakikika kuwa hawawezi kutoa madhumuni kutoka ndani ya Vitabu vyao vya kimbingu kuyakabili madhumuni yaliyomo ndani ya Sura Al-Faatihah.

Al-Kitab, dalili ya pili ya Kurani Tukufu kuwa Kitabu kamili Aliyoitoa Mwenyezi Mungu ndani ya *La raiba fiihi* ni hii kwamba mafundiho ya Kurani Tukufu yakimwondoa binadamu katika majangwa ya dhana humfikisha kwenye daraja za juu za yakini kwa dalili na ishara bayana. Na sifa hii njema itadumu daima dawamu ndani yake, kwani Mwenyezi Mungu Ameihifadhi. Sawa na maana moja ya *Raib*, muradi huu pia upo ndani yake kwamba Kitabu hiki kipo katika hifadhi ya Mwenyezi Mungu; ulaghai wa kishetani hauwezi kukiingilia. Hivyo, jinsi kinavyoathiri roho ya binadamu leo, ndivyo kitakavyoendelea kuiathiri roho ya mtu mpaka Kiama. Basi, hiki Al-Kitab ni Kitabu kilichokamilika. Muradi mmoja wa *La raiba fiihi* pia ni kwamba mwongozo au ukweli wowote unaolazimika kuwemo ndani ya Kitabu kikamilifu haukosekani ndani yake. Kuhusiana na jambo hili pia Hadhrat Masihi Mau'udi^{as} amezitupia mwito dini nyingine katika sehemu nyingi kwa ajili ya uamuzi. Akasema kwamba dalili yoyote ya kweli kuhusu uwepo wa Mungu nionyesheni kutoka katika Vitabu vyenu, ambayo nisiweze kuwaonyesheni nikiitoa kutoka ndani ya Kurani Tukufu. Basi kila kweli ambayo Kitabu chochote kingine kinaweza kudai, imo ndani yake, na

pia zimo ndani yake kweli nyingine nyingi zisizomo ndani ya Vitabu vingine, kwa hiyo hiki Al-Kitab ni Kitabu kilichokamilika.

Sawa na maana ya nne ya *La raiba fihi*, hapa pameelezwa dalili hii kwamba jaribuni kwa kutekeleza mafundiho haya, mtajikuta mmesalimika na misiba na maafa ya kila namna, na mtakuwa chini ya hifadhi ya Mungu, kisha ulaghai wowote wa dunia na nguvu yoyote ya ulimwengu au njama yake yoyote haiwezi kuwahasirisha kikweli, kwani hasara hupatikana iwapo kitu fulani kipotee kweli. Lakini kama Rupia tano za mtu zipotee, na hapo babake ampe Rupia tano badala yake na tena amwongezee Rupia kumi nyingine kwa kumfariji na tashwishi aliyopata na kwa hivyo sasa akawa na Rupia kumi na tano, hapo hakuna mwenye lubu atakayesema kuwa huyo amepata hasara ya Rupia tano. Hivyo, Mwenyezi Mungu Amedai sehemu hii kwamba hamtapata hasara au taabu, Hakusema kuwa hamtapata udhia. Kwani mwaminio hana budi kutoa dhabihu katika njia ya Mwenyezi Mungu, lakini kile inachokifahamu dunia kuwa taabu, mwaminio hukiona ni raha. Na Mungu wake, Mola wake na Mmiliki wake, Ambaye kwa ajili yake mja huyo anaendela kuvumilia taabu hii na shida, Anamwandalia mambo ya kumfurahisha, kumchangamsha na kumstarehesha mpaka anafahamu kwamba mwenye kuniudhi ameniudhi kidogo tu, na anayakini kuwa kama angeniudhi zaidi, ningepata mapenzi zaidi ya Mola

wangu. Basi, kwa kuwa hiki ni Kitabu ambacho mwaminio wa kweli anayetokeleza mafundisho yake hahasiriki katu, na kinyume chake Vitabu vingine havina hali hii, basi imethibitika kuwa hiki ndicho Kitabu kilicho Al-Kitab, na kwa hiyo Mwenyezi Mungu Alisema ndani ya Sura An-Nisaa (4:171):

يَا أَيُّهَا النَّاسُ قَدْ جَاءَكُمْ الرَّسُولُ بِالْحَقِّ مِنْ رَبِّكُمْ فَأَنْوُوا خَيْرًا لَكُمْ

Enyi wanadamu wote, sikilizeni kwamba mtu mmoja mkamilifu amekwishawajieni kwa ukweli mkamilifu toka kwa Mola wenu. Mola wenu Aliyekuwa Amewaumbeni kwa shabaha mahususi, Amewaleteni, kwa kuwapitisha katika daraja tofauti za ukuaji na uendeleaji, kwenye daraja ile ya kuwaingizeni ndani ya pepo zake kamilifu. Sikilizeni kwamba Mtume huyu amekwishafika *Fa aminuu*, aminini ayasemaye. Mwaminini kwa ulimi wenu pia na kwa moyo vilevile na kadhalika kwa viungo vyenu. Na kama mkitekeleza mafundisho yake na kumwamini Mtume huyu mkamilifu na kupitisha maisha yenu kulingana na sheria yake kamilifu, mtakuwa umati bora. Nanyi mtakapokuwa umati bora – na mtakuwa umati bora hapo tu mtakapoweza kuwanufaisha wanadamu wote – hapo kutoka kwenu watu wa mataifa yote na wa zama zote watajipatia manufaa kidini na kidunia. Na maadamu hampati daraja hii, dunia nzima na watu na mataifa yote waishio katika kila sehemu ya dunia hawawezi kujinufaisha kwenu, na madhali mataifa yote ya ulimwengu hayawezi kunufaika kwenu, hamwezi mpaka wakati huo kuitwa kuwa

Ukhrijat Linnaasi, mmeumbwa kwa kuifaa dunia nzima. Na mpaka iweze kusemwa kuwahusu nyinyi kwamba mmeumbwa kwa kuifaa dunia nzima, hadi wakati huo ahadi ya *inna awwala Baitin wudhi'a linnaasi* haitatimia. Hivyo, 'aaminuu, itikieni labeka anapowaiteni na kuiamini sheria ya Kurani, ishini kulingana nayo, mtakuwa umati bora.

Basi, kupitia ushukaji wa Kurani, kusudio la *wudhi'a Linnaasi* likapatikana. Mwenyezi Mungu Anasema katika Sura Aali 'Imraan 3:111, kwamba:

كُنْتُمْ خَيْرَ أُمَّةٍ أُخْرِجَتْ لِلنَّاسِ تَأْمُرُونَ بِالْمَعْرُوفِ وَتَنْهَوْنَ عَنِ الْمُنْكَرِ وَتُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ ۗ وَكَوَلَّيْنَا أَهْلَ
الْكِتَابِ لَكُمْ خَيْرًا لَّئِنْ

Ndani ya aya hii kwa hakika imedaiwa kwamba umati wa Muhammad^{saw} umeumbwa sawa na bishara na ahadi ya Hadhrat Ibrahimu^{as} kwa faida ya wanadamu. Ndiyo kusema kwamba umati mmoja umekwisha kujiandaa ulio *Ukhrijat Linnaasi*. Huo umeumbwa kwa manufaa ya binadamu wote. Dalili yake iliyotolewa hapa ni kwamba huu ni umati bora, kutokana na jambo hili inathibitika kwamba huu ndio *Ukhrijat linnaasi*, yaani huu umeumbwa kwa ustawi wa wanadamu wote. Dalili hii ni hivi kwamba kama mkizizingatia sheria zote za dunia, mtafikia natija hii kwamba sheria zote ziliendelea kuteremka kuafikiana na vipaji vya kaumu mbalimblai. Kutokana na sheria iliyopewa kwa kaumu ya Hadhrat Nuhu^{as} twaelewa vipawa vya ruhania vya kaumu ya Hadhrat Nuhu^{as} vilikuwa ni vipi. Kutokana na sheria

iliyomteremkia Hadhrat Musa, twapata kujua vipaja na vipawa vya ruhania vya kaumu ya Hadhrat Musa^{as}, Bani Israeli, vilikuwa vipi. Kadhalika ilikuwa ni hali ya kaumu za manabii wengine. Kwa vyovyote sheria yoyote inayoiteremkia kaumu yoyote toka kwa Mwenyezi Mungu huwa kwa kuangalia vipawa na vipaji vyake, kwani Mwenyezi Mungu Hamtwishi mtu au kaumu yoyote mzigo isioweza kuvumilia.

Uhakika wa pili ulio bayana sana ni huu kwamba sheria ya Kurani, kwa kulinganishwa na sheria zote za awali, ni kamilifu timilifu sana. Kama mkiweka maamrisha na makatazo ya sheria za zamani kukabiliana na hukumu za Kurani Tukufu, mtatambua kuwa ndani ya Kurani Tukufu kuna maamrisha na makatazo zaidi ya mia sita saba kwa ajili ya umati huu, ilhali Hadhrat Musa^{as} aliteremkiwa na hukumu chache sana. Tena ndani ya Kurani Tukufu mna mamia ya hukumu zisizoonekana katika sheria yoyote ya hapo kabla. Hii inahakikisha kuwa hukumu (maamrisha na makatazo) za sheria za zamani zilikuwa chache, kwa sababu vipaji vya kaumu ile iliyoteremkiwa na sheria hizo vilikuwa vichache. Na Kurani Tukufu ikiwa sheria kamilifu timilifu huthibitisha kwamba wanadamu wa zama ilipoteremka Kurani Tukufu, walikuwa na vipawa kamili vya ruhania; la sivyo, Kurani isingewashukia.

Hivyo basi, sifa kamilifu mahususi za mafundisho ya Kurani zinashuhudia vipawa vikamilifu vya umati huu.

Kwa kuona ukamilifu wa mafundisho ya Kurani Tukufu, na wasaa wake mwingi wa ukamilifu wake na shani yake, tunafikia natija hii kwamba wale ambao Kurani Tukufu inasema nao ndio wenye fadhila na ubora na utukufu katika vipawa na vipaji vyao kuliko nyimati za zamani. Kisha vipawa na vipaji hivyo vilipolelewa na Kurani Tukufu, hapo kwa maarifa ya Roho mtakatifu na nguvu takatifu ya Mtume^{saw} wakazaliwa – kwa baraka ya kumfuata yeye^{saw} – waja wa kiroho waliokuwa katika idadi, ubora, mwenendo na hali, wakamilifu watimilifu kuliko watoto wa kiroho wa manabii wa zamani. Na kama usingezalika umati bora ambao umati wowote wa hapo kabla usingeweza kuthubutu kukabiliana nao, na huu usingezitangulia nyimati zote, na baadaye pia usingeweza kuzalika umati wowote ambao ungeupita umati huu – yaani umati huu uwe umefikia upeo wake na kilele chake – ahadi ya *wudhi'a linnaasi* isingepata kutimia. Kwani, kwa sababu ya sheria pungufu na kwa ulezi mpungufu haitarajiwi kuwa umati ule utakuwa wenye kuzinufaisha sehemu zote za ulimwengu. Almuradi hakukuwa na umati wowote uliokabiliana hadi leo na umati wa Muhammad^{saw} katika kutoa heri, wala uamti wowote ule hauwezi kuzalika mpaka Kiama utakaokabiliana na umati wa Kiislamu. Hivyo, Mwenyezi Mungu Anasema:

كُنْتُمْ خَيْرَ أُمَّةٍ أُخْرِجَتْ لِلنَّاسِ

Sawa na ahadi hii hii ya Ibrahimu^{as} mmeumbwa kwa manufaa ya watu wote. Dunia nzima itajipatia faida

kwenu, itapata baraka kwenu. Uthibitisho wake ni kwamba m umati bora kwa jiha zote mbili. Kwa jiha ya vipaji pia na jinsi mlivyoiga mfano mwema wa Mtume^{saw} na khulka zake njema pia kwa sababu ya ulezi bora. Na mwaweza nyie tu ambao dunia nzima yaweza kufaidika nanyi. Basi, kuwa kwenu uamti bora na kufikia vipawa vyenu na vipaji vyenu ukamilifu wake, kisha ulezi wa vipawa na vipaji vyenu kufikia upeo wake, vyahakikisha kwamba ahadi ile imekwisha timia kwamba Baitullah imeimarishwa kwa manufaa na heri ya mataifa yote ya ulimwengu.

Pia ikumbukwe kwamba mtu anaweza kuwanufaisha wanadamu wote hapo tu ambapo yeye aimarishe baina ya wanadamu wote udugu na usawa, na asihalalishe ubaguzi na tofauti yoyote ile iwayo. Basi mambo yote yenye kuimarisha heshima na taadhima ya binadamu yamo ndani ya sheria ya umati wa Kiislamu, Kurani Tukufu au mfano mwema wa Mtume^{saw} au Hadithi. Islam imefutulia mbali kila ubaguzi na tofauti baina ya mtu na mtu, na hivyo ikaimarisha heshima na adhama ya binadamu.

Hotuba aliyotoa Mtume Mtukufu^{saw} kwenye *Hajjatul wadaa'* – hija ya kuagana – ndani yake pia alisema:

Habedari! Zindukeni! Tegeni masikio kwamba Mola wenu ni Mmoja. Ndiye Yeye Ambaye kwa ulezi wake mataifa yote yakisafiri umbali tofauti yamefikia mahala ambapo vipawa na vipaji vya kiroho na vya khulka vya

mataifa yote vimekuwa vya namna moja na sasa yako tayari kuipokea sheria ya mwisho. Muumbaji wenu ni Mmoja. Yeye Amewaumbieni vipawa vyenu vya kimwili na kiruhania kwa usawa; Hakutofautisha baina ya kaumu moja na nyingine. Ni sahihi kwamba kila mmoja analo eneo la maendeleo yake, lakini haiwezekani kuleta tofauti baina ya kaumu na kaumu. Sio kwamba kaumu moja ndiyo dhalili na hakiri au umbile lake ni namna ambavyo haiwezi kupata maendeleo ya kimwili au kiroho, kielimu au kihulka, kijamii au kiiktisadi. Basi, akasema, jihadharini. Sikilizeni kwa uangalifu kwamba Mola wenu aliyewaumbeni nyinyi na nguvu zenu, vipawa vyenu na vipaji vyenu, kisha akavitunza, na akawapitisheni katika daraja za maendeleo na kuufikisha ulezi na ustawi wenu kwenye ukamilifu, Huyu Mtukufu ndiye Mmoja. Nanyi mkumbuke vilevile kuwa baba yenu pia ni mmoja, yaani nyote m katika wazao wa Adamu. Kwa kifupi, Mola wenu Muumbaji ni Mmoja, na baba yenu Adamu ni mmoja. Kama mngekuwa wazao wa mababa tofauti, mngesema tumerithi kwa mababa zetu daraja hizi, na baba yetu alikuwa mtukufu na bora sana, hivyo tumerithi cheo hiki kikubwa. Lakini kauli hii ni batili, kwani baba ni mmoja. Tena kama miungu wangukuwa tofauti, hapo kaumu moja ingeweza kusema kwamba yule Mola Aliyetuumba Alikuwa Mwenye nguvu zaidi na elimu nyingi na Mweza sana na Mwenye upendo na rehema nyingi zaidi; Huyu Ametupatia mengi. Mungu Aliyewaumba wengine

hakuwa na elimu nyingi wala uwezo mwingi wala hakuwa mrehemevu zaidi, hakuwa na upendo kwa viumbe vyake sana jinsi Mola wetu Alivyokuwa nao kwa ajili yetu. Hivyo, watu wengine wakapatiwa vitu vichache na wakawa duni. Lakini kama Mola wenu ni Mmoja na baba mmoja, basi tambueni kuwa Mwarabu yeyote hana fadhila juu ya Mwajemi yeyote, wala mweusi hana fadhila juu ya mwekundu, wala mwekundu juu ya mweusi. Sehemu nyingine akasema pia kwamba mwekundu hana fadhila juu ya mweupe, wala mweupe juu ya mwekundu. Kipimo cha ubora machoni mwa Mola wenu na kwa sababu ya vipawa Alivyoviumba ndani mwenu ni kimoja tu, ncho ni Takwa. Machoni mwa Mwenyezi Mungu mkubwa zaidi ni yule aliye mcha Mungu zaidi. Lakini hamjui mtazamo wa Mungu. لَا تُؤْتُوا الْأَنْفُسَ كَمَا هِيَ أَعْلَمُ بِمَنْ أَنْتَ Basi msijitakase nafsi zenu; Yeye Anamjua sana aliyetakasika (Sura An-Najm 53:33). Ikiwa kipimo cha ubora chautegemea mtazamo wa Mungu, nasi hatuna habari kwamba Anatuangalia kwa jicho la upendo au ghaidhi, basi msitangazane ubora baina yenu. Huu ni mfano mmoja tu, waila mafundisho ya Kiislamu yamejaa maamrisha na mafunzo ya aina hii. Mathalani, Islam haitambui ubora wa iktisadi ya mtu yeyote. Bali yamwambia tajiri kwamba madhali umaskini upo, wewe huna haki juu ya mali yako. Akasema Mwenyezi Mungu: وَفِي أَمْوَالِهِمْ حَقٌّ لِّلسَّائِلِ وَالْمَحْرُورِ ‘Na katika mali zao imo haki ya aombaye na ajizuiaye’ (Sura Adh-Dhaariyat 51:20). Kwangu mimi, aya hii inamaanisha

kwamba mpaka kila mmoja apate mahitaji yake ya lazima, tajiri yeyote hana haki juu ya mali yake. Mahitaji ya lazima yatimiapo, hapo zinazosalia, hizi ni fadhili za Mwenyezi Mungu, Islam haimzuii mtu kuzitumia katika njia iliyo halali. Lakini, kama jirani ana kikomba cha njaa nawe uvile vyakula vya aina tano au saba, basi Islam hairuhusu jambo hili. Hivyo, kwa jiha yoyote taifa lolote halina ubora juu ya taifa jingine.

Mathalani, katika uwanja wa elimu, akili zote ni za namna mmoja. Katika kila kaumu wapo wenye ustadi mzuri na vipaji, na ndani ya kila kaumu kuna vichwamaji pia. Wote wanavyo vipawa vyao mbalimbali. Lakini, si sawa kwamba kaumu moja nzima iwe kichwamaji na kaumu nyingine nzima iwe yenye kipaji katika uwanja wa elimu. Hii ni kweli kwamba mataifa yanayotawala yanawapandisha hata majuha wao kwenye daraja ya juu sana. Mathalani, katika Oxford kulikuwa na mwanafunzi mwenzangu. Huko desturi ni hii kwamba mwanafunzi asiyeweza kuendelea na masomo yake, hawataki apoteze fedha zake bure, bali baada ya muhula mmoja aendapo kwao na matokeo ya muhula ule unapotolewa, huyo mwanafunzi anapelekwa barua kwamba huna haja ya kurejea masomoni, ufanye kazi yoyote pale ulipo. Kwa Kiingereza anaitwa ‘Sent home’ – amepolekwa nyumbani. Sasa yule mwanafunzi wa kikundi changu hakurejea kwa ajili ya muhula wa pili – nami nilikuwa sielewi desturi ya ‘kupelekwa nyumbani’ – basi nikawauliza marafiki zangu kumhusu

mwanafunzi huyo kwamba kwa nini hakurudi. Kwani nilifikiria kwamba wakati mwingine vifo vinatokea au pengine ajali, sielewei kwa sababu gani hakurejea. Hapo, rafiki mmoja akaniarifu kwamba ‘amepelekwa nyumbani’, ameondolewa chuoni. Mnamo mwaka 1944 nilipokwenda Delhi, kwa bahati nikawahi kumwona mtu na nikajua kuwa huyu ndiye yule yule mwanafunzi. Sasa yeye alikuwa afisa mkubwa katika serikali ya Kiingereza. Yeye akanitambua, nami nikamtambua pia. Tukaonana. Nikasema moyoni kwamba kwa kuwa taifa hili lina madaraka ya kidunia, hivyo, sawa na nahau nchini kwetu *‘wanawafanya mapunda wao pia kuwa maofisa’*, tena maofisa juu yetu. Ilmuradi, katika kila taifa kuna wenye lubu bora na lubu mbovu pia. Hakuna taifa lolote zima lisilo na hali hii. Hakuna taifa la watu walio wote wenye akili bora, na hakuna taifa lenye watu wote wenye akili mbovu. Wenye akili bora, ya wastani na mbovu, wote wanapatikana ndani ya kila taifa. Kwa ufupi, Islam haipendi ubaguzi, bali inaimarisha usawa. Kwa mfano, tazameni uwanja wa elimu. Islam inasisitiza sana kujifunza elimu, yaani kiasi mtu anachoweza. Kila mtu anapaswa kufundishwa sawa na uwezo wake na kipaji chake. Hii pia inamaanisha kwamba mwanafunzi mwenye uwezo hafifu anayepasi mtihani kwa kuhurumiwa, hapaswi kupewa msaada wa masomo, kwani huku ni kupoteza mali. Lakini yule mwanafunzi aliye hodari, kupoteza bongo lake ni utovu wa shukurani kwa Mwenyezi Mungu, na ni kulihasiri taifa.

Kwa kifupi, Islam imeimarisha usawa baina ya wanadamu na baada yake udugu; imeondolea mbali inda na bughudha zote za moyoni na imesema mpendane kama ndugu nyinyi kwa nyinyi. Kisha ikaimarisha mafundisho yake ya kimsingi juu ya nguzo kubwa tatu, na nguzo hizi tatu ni adili, hisani na *iita'i dhilkurbaa*.⁷ Kila kaumu ambayo ina hadhi ya kimataifa, ama mahusiano yale yaliyo ya kimataifa, yakiimarika juu ya msingi wa adili na kisha kusonga mbele na kuimarika juu ya hisani na kisha juu ya *iita'i dhilkurbaa*, basi matatizo yote ya dunia yanafutika leo hii, na watu wote wa duniani wanaanza kunufaikana wao kwa wao, badala ya kufikiria namna ya kuwahasirisha wengine. Hivyo, Mwenyezi Mungu Akitupa amri ya kimsingi Ametuambia kuwa baadhi ya watu kitabia hawataweza kujisogeza mbele zaidi ya adili, Twawaambia nyinyi msiachane na daraja ya adili na kuanguka chini, waila hamtabaki kuwa Waislamu. Wengine watakuwa na tabia ya kusonga mbele na kufikia daraja ya hisani, lakini hawatakwenda mbele zaidi. Hawa Twawaambia kama juu ya kuwa na uwezo, mkiachana na daraja ya hisani na kuteremeka hadi adili, mtajinyima neema nyingi sana ambazo mngeweza kupata kwa kuimarika juu ya daraja yenu ile; na hii siyo hasara ya kawaida, bali ni hasara kubwa fika. Kisha kati yenu wapo wengine ambao wakipanda juu ya daraja hizi mbili,

⁷ Uwape watu (kama uwapavyo ndugu).

wanafikia daraja ya *iitai dhilkurbaa*, na wanaweza kuifikia. Hawa Twawaambia kwamba msiridhike na daraja ya hisani, la sivyo mtanyimwa neema, fadhili na baraka nyingi zisizo na kifani. Almuradi, Islam imeimarisha usawa baina ya wanadamu na udugu na kupendana juu ya nguzo hizo tatu.

Hivi sasa, saa nyingi imeishapita, lakini nilipenda kueleza kwa marefu na mapana kusudio hili, kwani miongoni mwa makusudio haya 23 kusudio hili ni la kimsingi; kusudio la mwisho pia ni la muhimu kama hili; yaliyo baina ya hayo tutapita haraka. Kuhusiana na jambo hili ndugu mmoja ameona ruya pia. (yeye hakuelewa maana yake). Siku chache zimepita aliniandikia kwamba nipo (pamoja na marafiki zangu kadha) katika njiapanda ile ya Qadian iliyoongezwa baadaye ambapo ngazi za sehemu ile ya Masjid Mubarak zinateremkia. Hapa patakuwa na watoto wengi wasioiona Qadian, hawa hawawezi kufahamu, lakini walioiona Qadian wanaweza kufahamu kwamba ngazi za ile sehemu mpya ya Masjid Mubarak iliyokuwa imeongezwa zilikuwa zinateremkia kwenye njiapanda moja. Ndugu huyo aliandika kuwa sisi tumesimama katika njiapanda hiyo, nawe umefika haraka sana, uso wako ulikuwa na bashasha na uchangamfu. Unapanda vidaraja kadha vya ngazi, kisha unatutazama. Tena unapanda vidaraja kadha vya ngazi na unatutazama. Ulifanya hivyo mara mbili, kisha ukapanda vidaraja vyote, na ulitoa adhana. Tunafikiri kwamba ni wakati wa

sala ya Alasiri, hivyo utatusalisha. Lakini adhana uliyotoa kabla ya sala tulihisi ni ndefu kuliko kawadia. Na sehemu hii niielezayo ni kama kuwaiteni kwenye mkakati mahususi, ili nitakapowaiteni kwenye mkakati huo mwanze kufahamu majukumu yenu mkiishaelewa mandharinyuma yake barabara. (Adhana kuwa ndefu kuliko kawaida yaashria kwenye jambo hili hili)

Kwa ufupi, *Wudhi'a linnasi* ilikuwa ni kusudio moja la ujenzi wa Baitullah. Na kwa kuwa hili ni la muhimu sana kwa sababu makusudio mengine yote yanahusiana na kusudio hili la kwanza, au yanahusiana na kusudio la mwisho lililoelezwa katika *رَبَّنَا وَابْعَثْ فِيهِمْ رَسُولًا مِنْهُمْ يَتْلُو عَلَيْهِمْ آيَاتِكَ...*, nilipenda kulieleza kwa kirefu ili mpate kufahamu kwamba bishara ya *wudhi'a linnasi* haingeweza kutimia pasipo kuzalika duniani umati ule ulio bora wa nyimati. Na umati huo usingeweza kuzalika mpaka ingepata kuteremka sheria ya Kurani Tukufu iliyo kamilifu timilifu. Kila sheria huteremka kuafikiana na uwezo wa kaumu. Kwa kuwa sheria ya Kurani Tukufu imekamilika fika kwa kila jiha, hivyo twafikia natija hii (na hatuweza kufikia natija nyingine) kwamba mataifa yale yaliyohubiriwa hiyo katika zama hizo na tena mpaka Kiama yataendelea kuhubiriwa, hayo kwa vipaw na vipaji vyao yaliweza kuibeba Kurani Tukufu. Na baada ya kupokea malezi ya Kurani Tukufu na kupata hadhi katika tajamala na baraka za Mtume^{saw}, sura zao zikabadilika namna ambavyo machoni mwa wenye busara wakawa wanadamu wapya, yaani sura zao

iliyokuwa hapo kabla na nakshi zao za zamani hazikubaki hata kidogo, bali nakshi mpya zikaibuka. Mfano wao ni kama mfano wa nondo wa hariri ambaye anapokuwa ameishatengeneza hariri, hapo kama binadamu ampatie nafasi, naye atoke nje ya kifukofuko chake alichokuwa amekitengeneza pembezoni mwake, huyo hawi tena mdudu yule wa kwanza, bali kichwa chake cha kwanza, macho yake ya kwanza na sura yake hugeuka fika. Kwanza huwa hana mabawa, lakini ndani ya masaa 24 au 48 mabawa yake yanajitokeza, kichwa kipya kuinazalika na macho mapya. Huu huu ndio mfano wa wale watu waliomwamini Mtume^{saw}; kwanza walikuwa wadudu wa ardhini, baadaye Mwenyezi Mungu Akawajaalia busara mpya, macho mapya, akili mpya, nguvu mpya ya kuruka, kisha wakaanza kuruka maangani mwa mbingu. Na ilipozalika kaumu hii, ahadi ya *wudhi'a Linnaasi* nayo ikatimia.

Kutokana na hii, inajulikna kwamba kaumu ile ambayo Kurani Tukufu inaiita kuwa umati bora, huwa na majukumu ya aina gani ili kuitumikia dunia. Mwenyezi Mungu Atujaalie sisi sote uwezo wa kutekeleza majukumu yetu. (Amin)

(Gazeti la Alfadhl, Rabwah, 7 Mei 1967)

④

**Kudhihiri kwa Baraka za Kaaba
kwa Dunia Nzima
kwa Kutumwa
kwa Mtume Mtukufu^{saw}**

Hotuba ya Ijumaa, 5 Mei 1967,
Masjid Mubarak, Rabwah, Pakistan.

“Mwenyezi Mungu Alitaka kuifanya Kaaba kuwa yenye baraka. Kwa kutumwa Mtume^{saw}, Baitullah ikawa *mubarak*... Na Mwenyezi Mungu Alitaka kupeleka sehemu hii mwongozo ulio Mwongozo kwa walimwengu wote kwa sababu ya ukamilifu wa sheria pia na kwa kuwanufaisha watu pia. Na ahadi hii pia ikatimia kwa njia ya Kurani Tukufu.”

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ⁸

تَحْمِيْدًا وَتُصَلِّيٰ عَلَىٰ رَسُوْلِهِ الْكَرِيْمِ⁹

Baada ya kutamka Shahada mbili na A‘udhu na kusoma Sura Al-Faatiha, Hudhur alisoma aya hii:

اِنَّ اَوَّلَ بَيْتٍ وُضِعَ لِلنَّاسِ لَلَّذِيْ بِبَكَّةَ مُبْرَكًا وَهُدًىٰ لِّلْعٰلَمِيْنَ ۗ

(Aali ‘Imraan, 3:97)

Naendelea kuwaambia jinsi makusudio 23 ya ujenzi wa Baitullah yalivoelezwa ndani ya aya hizi yalivyotimia kwa kutumwa Mtume^{saw}. Ndani ya hotuba iliyopita nilitoa maelezo ya *wudhi‘a Linnasi* katika mandharinyuma hii.

Kusudio la pili lililoelezwa ndani ya aya hizi ni hili kwamba Kaaba ni *mubarak*. Nilieleza kuwa neno *mubarak* hapa laweza kuchukuliwa katika maana mbili. Mosi, Kaaba itakuwa ni makazi ya wawakilishi wa Mataifa yote ya ulimwengu, na kutoka mataifa yote wataendelea kujumuika hapa watu watakaokuwa ‘simba’ wa nyanja za ruhania. Hapa patakuwa ni mahali pa kukaa watu shujaa wenye kukaa imara kwa ushupavu. Historia inashuhudia kwamba katika maana hii Baitullah haikuwahi kuwa *mubarak* kwa dunia nzima kabla hajatumwa Mtume^{saw}. Yaani, kabla ya Mtume^{saw} kutumwa hayakuzalika nyoyoni mwa mataifa ya dunia mahaba ya Baitullah kiasi hiki kwamba watu wangevutika kwake na kuikimbilia. Tena haikuwa

⁸ Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwingi wa na Ukarimu.

⁹ Twamhimidia Yeye na kumsalia Mtume Wake mhashamu.

sababu yoyote ndani ya Kaaba ambayo ingekuwa ya kuwapa utulivu wajumbe wa mataifa ya dunia nzima kama wangepata kufika huko.

Baada ya Mtume^{saw} kutumwa hali ya dunia kwa jiha hii ikabadilika. Upande mmoja mapenzi yalizalika nyoyoni mwa mataifa ya dunia, na upande mwingine sababu zilipatikana kwa watu kuiendea ili kujifunza elimu za ruhania au ya maandiko au ya kimantiki au ya kidini – elimu ziwezazo kuwanufaisha watu wa mataifa yote katika kila zama kidini na kidunia. Historia inahakikisha kwa uwazi sana kwamba shabaha hii ilitimizwa kwa kutumwa kwa Mtume^{saw}, kwa hiyo haina haja kuieleza zaidi.

Maana ya pili ya *Mubarak* inayofaa hapa ni hii kwamba Makka itafanywa kuwa mahali pa kuzalika sheria moja ambamo zitajumuishwa kweli zote za kimsingi na miongozo vinavyopatikana katika sheria mbalimbali za manabii wa zamani. Kurani Tukufu ndiyo sheria ya pekee iliyodai kujijumuishia kweli zote za zamani. Kabla ya Kurani Tukufu hakuna sheria yoyote iwayo iliyodai jambo hili wala zisingeweza kutoa madai kama haya, kwani Mungu Mwenye kuziteremsha Alijua kuwa sheria hizo zinateremshwa kwa ajili ya mataifa maalum na kwa zama mahususi.

Kurani Tukufu imetoa dai hili ndani ya aya mbalimbali ambazo baadhi yake napenda kuwaambia marafiki zangu wakati huu. Mwenyezi Mungu Anasema katika Sura Al-

An'aam 6:156 kwamba **وَ هَذَا كِتَابٌ أَنْزَلْنَاهُ مُبَارَكٌ فَاتَّبِعُوهُ وَ اتَّقُوا لَعَلَّكُمْ تُرْحَمُونَ**
Yaani Kurani hii ni Kitabu, ni Sheria iliyo *Mubarak*, kana kwamba mambo mazuri ya Vitabu vya mbingu na kweli zao za kimsingi zimetiririka ndani yake. Sasa kifuateni kikamilifu Kitabu hiki kilichobarikiwa **إِتِّبِعُوهُ** , mtapata faida mbili kwayo. Mosi, mtaingia katika hifadhi ya Mungu; Mungu Atakuwa ni ngao yenu, naye Atawakingeni na wasiwasi wote wa kishetani. Kwani, pasipo kukifuata Kitabu hiki kilichobarikiwa, maarifa ya njia zilizo sawa za Takwa hayapatikani, na mtu hawezi kuingia katika ulinzi wa Mwenyezi Mungu bila kuzifuata njia hizo. Natija yake ya pili itakuwa kwamba mtastahili kurehemiwa na Mwenyezi Mungu na kwa sababu ya neema zake zisizo na mipaka mtapata ustawi wa kimwili na kiroho.

Kadhalika, mahali pengine (ndani ya Srua Al-An'aam 6:93), Mwenyezi Mungu alisema:

وَ هَذَا كِتَابٌ أَنْزَلْنَاهُ مُبَارَكٌ فَصَبِّحْهُ الَّذِي بَيْنَ يَدَيْهِ وَ لَتُنذِرَ أُمَّ الْقُرَىٰ وَ مَنْ حَوْلَهَا
Yaani, Kurani hii ni Kitabu chenye shani adhimu Tulichokiteremsha kijumuishacho baraka za kila namna za nyimati zote za zamani (**مُبَارَكٌ**) . Na kimeteremka kuafikiana na bishara na matabiri yaliyomo ndani ya Vitabu vya zamani kuhusiana na Kitabu hiki, tena kinahakikisha ukweli wa kweli za kimsingi na miongozo ya sheria zote za hapo awali (na zimejumuishwa ndani mwake). Kadhalika, hiki ni tunda la dhabihu na dua za Hadhrat Ibrahimu^{as}. Hivyo, uwahabarishe wenyeji wa

Makka na waishio Bara Arabu kwamba ile sheria mliyokuwa mmeahidiwa, ahadi hiyo imetimia na sheria iliyoahidiwa imeisha wateremkieni. Kama mkikengeuka, basi mtaangukiwa na ghadhabu ya Mwenyezi Mungu na mtaburutwa kwenye adhabu ya Moto jinsi mlivyoarifiwa kupitia Hadhrat Ibrahimu^{as}.

Ndani ya aya hii لِيُنذِرَ أُمَّ الْقُرَىٰ وَمَنْ حَوْلَهَا , imeelezwa bayana kwamba 'Mubarak' huhusiana na dhati ya Mtume Mtukufu^{saw} na bishara za Hadhrat Ibrahimu^{as}.

Hivyo, kwa jiha ya maana zote mbili, Nyumba hii ya Mungu ikawa *mubarak* wakati alipotumwa Mtume^{saw}. Mapenzi ya Makka yalizalishwa moyoni mwa dunia, na kwa kutimiza mahitaji ya dunia, sheria ya Kiislamu ilishuka Makka.

Kusudio la tatu la ujenzi wa Kaaba aliloeleza Mwenyezi Mungu ni *Hudan Lil'aalamiin*. Hii itafanywa kuwa makao makuu ya mwongozo kwa walimwengu wote. Yaani, hapa sheria moja itateremka isiyohusikana na taifa moja tu au zama moja tu, bali itahusiana na 'Aalamiin, mataifa yote, sehemu zote za dunia, walimwengu wote na zama zote.

Kuhusiana na habari hii, jambo la kwanza lifaalo kukumbukwa ni kwamba katika zama za kuteremka Vitabu vya kimbingu, vipawa dhaifu vya binadamu havikufaa kustahili kutwisha sheria iliyokamilika, kwa hiyo hata Kitabu kimojawapo hakikudai kuwa kwa ajili ya mataifa yote ya ulimwengu na kwa zama zote. Kwa

hiyo dai la kuwa لِلْعَالَمِينَ (katika maana hii) haikulifanya sheria yoyote kabla ya Kurani. Kurani Tukufu peke yake imetoa dai hili, Mtume Muhammad^{saw} pekee aliitangazia dunia kuwa mimi ni Mtume kwenu nyote. Ndani ya Kurani Tukufu mna aya chungu nzima kuhusiana na madhumuni haya. Nitazieleza hapa aya chache tu kama mfano. Mwenyezi Mungu Anasmea: وَكُنَّا عَلَيْكَ تَنبِيئًا مُبِينًا (Sura Al-Nahl, 16:90). Yaani, tumekuteremshia Kitabu kile ambamo kila kitu na kila fundisho limeelezwa tulilotaka kueleza kwa maendeleo ya juu sana ya ruhania ya binadamu. Yaani, katika elimu yetu kamilifu, mafundisho yaliyokuwa ya lazima kwa maendeleo ya juu sana ya ruhania tumeishayaeleza ndani ya Kitabu hiki. Sehemu nyigine Akanena: مَا فَزَّطْنَا فِي الْكِتَابِ مِنْ شَيْءٍ (Sura Al-An‘aam, 6:39). Yaani, kwa ukuaji sahihi wa vipaji kamili wa binadamu, chochote kilichohitajika kimeishaelezwa ndani yake, hakuna mafundisho yoyote yaliyokosekana humo. Kwa sababu hii hii Mwenyezi Mungu Amedai ndani ya Kurani Tukufu: الْيَوْمَ اكْمَلْتُ لَكُمْ دِينَكُمْ وَأَتَمَمْتُ عَلَيْكُمْ نِعْمَتِي وَرَضِيتُ لَكُمُ الْإِسْلَامَ دِينًا (Sura Al-Maa’ida, 5:4) Yaani, kwa njia ya Kurani Tukufu, dini imefikia ukamilifu wake, na neema za ruhania upeo wake. Sasa kwa kupitia Islam tu mtu anaweza kupata radhi ya Mwenyezi Mungu.

Hadhrat Masihi Mau‘udi^{as} akieleza aya hii anasema kwamba kutokana na aya hii inabainika kuwa:

“Kurani Tukufu ndiyo tu iliyotoa mafundisho kamili, na zama za Kurani Tukufu tu zilifaa kwa

kutolewa mafundisho yaliyokamilika. Hivyo basi, dai hili la mafundisho kamili ililotoa Kurani Tukufu ilikuwa ni haki yake tu. Pasipo Kurani Tukufu hakuna Kitabu chochote cha kimbingu kilichotoa dai kama hili, jinsi ilivyo dhahiri kwa watazamao kwamba Torati na Injili zote mbili hazina madai haya.”

(Dibacha Baraahine Ahmadiyya, J. 5, uk. 5).

Yeye, Hadhrat Maishi Mau‘udi^{as}, akafafanua kuhusu madai haya kwamba Torati ilisema Mtume atainuliwa kutoka ndani na ndugu zenu, naye atawasomeeni Neno kamili la Mungu, na asiyemsikiliza na kumfuata, Mwenyezi Mungu Atalitaka kwake. Kama Torati ingekuwa kamilifu, usingekuwa uwezakano wa kuteremka sheria yoyote baada ya Torati, ambayo kwa kuikana mtu angeghadhibikiwa na Mwenyezi Mungu.

Na Injili ikajitoa katika jambo hili ikitangaza kwamba kuna mengi yafaayo kuelezwa, lakini nyinyi hivi sasa hamwezi kuyavumilia, kwani vipaji vyenu bado havijakamilika.

Basi, Hadhrat Masihi Mau‘udi^{as} anasema:

‘Ni dalili kubwa fika kwa kuthibitisha ukweli wa Islam kwamba kwa njia ya mafundisho yake huishinda kila dini na hakuna dini yoyote iwayo

izezayo kuikabili kwa jiha ya mafundisho yaliyokamilika.”

(Dibacha Baraahine Ahmadiyya, J. 5, uk. 4).

Kwa kuwa Kurani Tukufu na Islam inaishinda kila dini, hivyo Mwenyezi Mungu Akaitangazia dunia وَقُلْ جَاءَ الْحَقُّ وَزَهَقَ الْبَاطِلُ إِنَّ الْبَاطِلَ كَانَ زَهُوقًا (Sura Banii Israaiil, 17:82) Hadhrat Masihi Mau'udi^{as} akiieleza anasema kuwa hapa muradi wa الْحَقُّ ni Dhati ya Mwenyezi Mungu pia na vilevile Mtume^{saw} na Kurani Tukufu.

Hivyo basi, aya hii imemaanisha kwamba kupitia Kurani Tukufu na Mtume^{saw} onyesho la kijalali la Mwenyezi Mungu likadhihiri, na kwa sababu ya onyesho hili la kijalali, shetani pamwe na majeshi yake akakimbia, na mafunzo yake yakathibitika kuwa dhalili na hakiri, na uchafu wa mila zake mbovu na wa bidaa mbaya alizoimarisha ukadhihirika, na kundi hili likapatwa na ushinde mkubwa fika.

Hivyo, hili ni dai la Kurani Tukufu kwamba kwa shabaha hii hii ikadhihiri Kurani Tukufu na Mtume^{saw}. Ndani ya Sura At-Tauba 9:33, Mwenyezi Mungu Ananena: هُوَ الَّذِي أَرْسَلَ رَسُولَهُ بِالْهُدَىٰ وَدِينِ الْحَقِّ لِيُظْهِرَهُ عَلَى الدِّينِ كُلِّهِ ۗ وَ لَوْ كَرِهَ الْمُشْرِكُونَ . Yaani, Yeye ndiye Aliyemtuma Mtume Wake ili Aishindishe juu ya dini zote, ijapokuwa washirikina wachukie.

Hebu, nieleze kuwa ndani ya aya hii, kipande chake mpaka عَلَى الدِّينِ كُلِّهِ kimo ndani ya Kurani Tukufu mahali

patatu mbalimbali, na katika kila mahali muradi wake na madhumuni yake ni tofauti. Katika sehemu hii Mwenyezi Mungu Amesema kwamba ni Mungu tu Aliye kamili katika Dhati yake na sifa zake, Yeye ndiye Aliyemtuma Mtume huyu kwa mwongozo na dini ya haki. Na shabaha ya kutumwa kwake na kudhihiri kwake ni kwa kuthibitisha ubora wa sheria hii na wa Mtume huyu juu ya dini zote. Ubora wa dini ya kweli utakapothibitika, basi na ubora wa aliyeleta dini utathibitika wenyewe. Hapa imesemwa **لِيُظْهِرَ عَلَى الدِّينِ كُلِّهِ** ambayo yamaanisha kwamba dini zote zile zilizokuwepo duniani kabla ya Mtume^{saw} kutumwa, lakini hali zao na sura zao zilikuwa zimevurugika, zitashindwa kila zitakapokuja kuikabili Islam; ndani ya Kurani Tukufu Amekwishaweka Mwenyezi Mungu sababu za jambo hili. Pia imeelezwa ndani yake kwamba ikiwa baada ya sheria ya Kiislamu itatokea dini ya uongo, Islam itaishinda hiyo vilevile, kwani hapa hamna sharti yoyote kwa dini kuwa iwe ya zamani. Mathalani, wapo Mabhai ambao wamebuni dini yao mpya kuikabili Kurani Tukufu; ni madai ya Kurani Tukufu kwamba zile dini zitakazozalika baada ya sheria ya Kiislam, Kurani Tukufu inayo nguvu ya kuponda kichwa chake. Kwani, hili ni Neno la Mungu Aliye Mjuzi wa mambo ya ghaibu, Ayajuaye yote yale yatakayotokea baadaye. Basi, dini ya Kiislamu ndiyo dini ya pekee ambayo dini yoyote ya kabla yake wala ya baada yake haiwezi kuikabili. Hii inayo nguvu ya kuzishinda kwa dalili zake

za kiakili, kweli zake za ruhania, miongozo yake na misaada ya Kimbingu.

Basi, madai ya kuwa هُدَىٰ لِلْغَالِبِينَ – mwongozo kwa walimwengu wote – imetoa Kurani Tukufu pekee, na imeyathibitisha pia kwa kitendo.

Niliwaambia kuwa neno *Hidayat* – mwongozo – lina maana nne katika lugha. Kuhusu maana ya kwanza iliyochapishwa katika hotuba ya kwanza si wazi sana, ningependa kuifafanua maana hii. Maana ya kwanza ya هدايت ni ule mwongozo ambao lubu na busara inauhitaji. Yaani, zile nguvu alizojaaliwa binadamu za akili na busara na za kujipatia elimu na kufanya utafiti wake, nguvu hizi pekee hazitoshi, bali hizo nazo zahitaji mwongozo kutoka mbinguni.

Hivyo, *hidayat* hii ni jinsi iliyo sawa kwa watu wote, haihusiani na dini yoyote iwayo. Kurani inasema kwamba jinsi hii iliyo sawa baina ya wanadamu wote nayo inaongozwa na Kurani Tukufu. Akili yenyewe ni kipofu tu kama hakuna jua la ufunuo. Na ili kumwambia binadamu kwamba uwezo wa kimwili na vipawa vya ruhania havitoshi mpaka kwa fadhili ya Mwenyezi Mungu sababu zake zizalike toka mbinguni. Mungu Ametoa ndani ya Kurani Tukufu mifano mingi sana. Mathalani, Ametoa mfano huu mmoja kwamba Twamfunulia nyuki. Na hili si dai tu ililofanya Kurani Tukufu, bali kwa kuwezesha na Mungu, utafiti wa kina wa binadamu umethibitisha kwa njia nyepesi ukweli wa

madai haya ya Kurani Tukufu. Basi, ndani ya utafiti mpya uliofanywa kuhusu nyuki, jambo hili limebainika kwamba malkia wa nyuki anapokuwa anataga mayai, wakati wa kutaga kila yai anafunuliwa kwamba kutokana na yai fulani mtoto wa kiume atazaliwa au wa kike. Ndani ya sega sehemu mbalimbali zimeteuliwa kwa shabaha maalum. Ndani ya sehemu fulani mama anaweka yale mayai wanamozaliwa watoto wa kiume, na katika sehemu nyingine ya sega anaweka yale mayai wanamozaliwa watoto wa kike. Hivyo, yule nyuki aitwaye malkia anataga mayai mamia na maelfu, na kila atagapo yai huambiwa ndani mwake mtatoka mtoto wa kiume au wa kike.

Basi, kwa mifano ya aina hii Mwenyezi Mungu Amemfahamisha binadamu kuwa msizitegemee nguvu zenu na uwezo wenu, akili zenu na busara zenu, elimu zenu na utafiti wenu pekee; hamwezi kufaulu kikweli katika uwanja wowote mpaka uwateremkieni mwongozo toka mbinguni. Na kwa kuwa Mwenyezi Mungu Amewajaalia wanadamu wote akili, na wale wanaotekeleza kanuni alizoeleza Mwenyezi Mungu, basi Mwenyezi Mungu Anawafunulia na Anawatilia akilini mwao elimu mpya mpya katika uwanja wa akili na uwanja wa ujuzi, bila kutofautisha kuwa mtu huyo ni Mwislamu au Mkristo au mwenye dini nyingine yoyote au mwenye dini mbovu au asiye na dini. Kwani, Mwenyezi Mungu Ameifanya akili kuwa urithi wa watu wote kwa usawa. Kurani inasema kuwa zaidi ya

miongozo mingine inayoteremka toka mbinguni, Sisi Tunaiongoza akili vilevile. Kuhusiana na habari hii, Hadhrat Masihi Mau‘udi^{as} amefafanua madhumuni haya kwa njia nyepesi sana kwamba Mwenyezi Mungu kupitia wahyi na ufunuo Ananoa lubu za binadamu, tena zile elimu zinazopata kukuzwa na ubongo bora, Kurani Tukufu inazitumikisha kama mahadimu. Hadhrat Masihi Mau‘udi^{as} anasema:

“Kwa kutambua uwepo wa Mwenyezi Mungu na sifa zake za uumbaji na Tauhid yake na kudura, rehema, *Ukayyumi* – kuwa Mhifadhi wa milele – na sifa zake za majazi na kadhalika, kiasi ambacho elimu za kiakili zahusika, Kurani imetumia njia ya mahojiano kikamilifu. Na kuhusiana na mahojiano haya... elimu zote zimefafanuliwa kwa njia nyepesi na ifaayo sana... na... imezitumikisha elimu zilizotajwa kwa njia inayostahili namna asivyotumikisha binadamu yeyote.”

(Surma Chashme Aria, uk. 24-25, maelezo ya pembeni)

Na huu ndio ubora wa Kurani Tukufu kwamba dini nyingine zinashindwa mbele ya elimu za kisasa, lakini Islam pekee ni dini na Kurani peke yake ni Kitabu kisichoshindwa mbele ya elimu yoyote ya kimantiki, bali kinaichukulia kama hadimu na kinaitumikisha.

Maana ya pili ya *hidayat* ni sheria iteremkayo toka kwa Mwenyezi Mungu. Hivyo, هُدًى لِلْغَالِبِينَ itamaanisha ile sheria iliyo kwa ajili ya *‘Alamiin*, kwa walimwengu wote

na kwa zama zote. Na Kurani Tukufu peke yake ndiyo هُدًى لِّلْعَالَمِينَ, ndiyo sababu Mtume Mtukufu^{saw} aliitangazia dunia kwamba: اِنِّي رَسُولُ اللّٰهِ اِلَيْكُمْ جَمِيعًا — mimi ni Mtume wa Mungu kwenu nyote, (Sura Al-A‘raaf 7:159) Kurani Tukufu imejaa madhumuni haya kwamba hii ndiyo kwa walimwengu wote na zama zote. Hili si dai tu, bali ni ukweli usiokatalika ambao kwa kuufafanua Hadhrat Masihi Mau‘udi^{as} anasema – sikilizeni katika maneno yake mwenyewe:

“Maarifa yote ya hali ya juu, na kweli zote tukufu zilizopo, na nukta zote na elimu za kina za Mungu zinazohitajika duniani kwa kuikamilisha nafsi, kadhalika magonjwa yote ya *nafsi ammaara* na jazba zake na maafa yake yatokaeyo kwa vipindi ama ya kudumu, au njia zao za kuyatibu au kuyarekebisha, na njia zote za kuitakasa na kuisafisha nafsi, na alama zote na sifa bainishi na mambo ya lazima ya kuzidhihiri fika khulka njema, hivyo vyote vimejaa ndani ya Kurani Tukufu kikamilifu kitimiifu. Na mtu yeyote hawezi kuleta ukweli wowote au ujuzi wa keto kuhusu Mungu au njia ya kumfikia Mungu au njia yoyote ya nadra au takatifu ya kujibidiisha kwa kumpata Mungu na ya kumwabudu Yeye isiyopatikana ndani ya Neno hili Tukufu.”

(Surma Chashme Aria, uk. 26, maelezo ya pembeni).

Mbele, Hudhur^{as} ametoa maelezo yake. Hivyo, ni dai la Kurani Tukufu pekee kwamba kila mwongozo na ukweli iliohitaji nafsi ya mtu kufikia ukamilifu wa ruhania, wote huo umo ndani yangu. Mkinifuata mtasalimika na kufunguliwa milango ya maendeleo ya ruhania, nanyi mtajipatia ukamilifu wa nafsi yenu. Kila sheria inayodai – na yaipasa kuidai – ya kwamba nawafungulieni milango ya maendeleo yasiyo na kikomo, na Kurani Tukufu imedai hii pia, maana mwanzoni tu ikasema هُدًى لِّلْمُتَّقِينَ (Sura Al-Baqara, 2:3), yaani mtu akifikia hata daraja gani ya Takwa, bado Kurani Tukufu inamfungulia njia nyingi zaidi za Takwa. Kisha mja huyo anafikia daraja nyingine za juu zaidi. Hapo daraja nyingine za juu sana zaonekana mbele yake, na jazba ya kuzipata hizi yazalika moyoni mwake, ndipo Kurani Tukufu yamwambia nifuate nitakupeleka kwenye daraja zingine za juu zaidi, na mfululizo huu unaendelea usio na kikomo.

Hadhrat Maishi Mau'udi^{as} ameeleza madhumuni haya kwa njia mbili. Mosi, neema na baraka nyingi zisizo na kikomo za Mwenyezi Mungu zipo juu ya Mtume^{saw}; neema hizi haziwezi kuwekewa mipaka. Na kwa kuwa neema za Mungu zisizo na kikomo zipo juu ya Mtume^{saw} kwa hiyo wenye kumsalia Mtume^{saw} wanaomtikia yeye baraka kwa mapenzi ya dhati huwa wanapata hadhi yao katika baraka hizi kadiri ya jazba yao. Kuhusiana na jambo hili, Hadhrat Masihi Mau'udi^{as} anasema mahali pengine:

“Naona baraka za Mwenyezi Mungu zamwendea Mtume^{saw} kwa sura ya ajabu ya nuru, na zikimfikia zinaingia kifuani mwa Mtume^{saw}, na kisha kwa kujitokeza toka humo zinakuwa na mifereji mingi isiyo na kikomo na kumfikia kila mwenye haki sawa na haki yake.”

(Al-Hakam, 28 Februari 1903, uk. 7)

Hivyo, madai ya Kurani Tukufu kuwa mimi ni هُدَى الْمُسْلِمِينَ, naifikisha nafsi ya mtu kwenye ukamilifu wake, yanatimia hivi kwamba dhati ya Mtume^{saw} machoni mwa Mwenyezi Mungu ni dhati tukufu ambaye rehema zisizo na mipaka za Mwenyezi Mungu huwa zinadumu kumteremkia, au tuseme maonyesho yasiyo ya mipaka ya sifa za Mwenyezi Mungu yamdhihirikia yeye^{saw} kila saa. Hivyo, yule mtu atakayempenda yeye^{saw} na kumtakia baraka na rehema na usalama, basi kama malipo ya mahaba yake ya dhati, Mwenyezi Mungu Ataendelea kumpa hadhi yake katika baraka hizo zote. Mtu huyo atakapokwishapata chochote kwa sababu ya Mtume^{saw} akitambua kuwa baraka zisizo na mwisho zaweza kupatikana kutoka kwake, hapo itazalika moyoni mwake jazba ya kujipatia baraka nyingine zaidi, basi atamsalia kwa jazba kubwa zaidi na mahaba mengi zaidi ya dhati, naye atanza kuteremkiwa na baraka nyingi zaidi.

Pili, kuhusu Kurani Tukufu, Hadhrat Masihi Mau'udi^{as} amesema kwamba Kurani Tukufu pia imedai ya kuwa

nawafungulia milango ya nuru isiyo na mipaka, ya baraka isiyo na mipaka na ya daraja zisizo na mipaka za kumkaribia Mungu, wenye kuniadini na kunifuata na wenye kumpenda Mtume^{saw}. Ndani ya Kurani Tukufu, Mwenyezi Mungu Anasema: **وَالَّذِينَ آمَنُوا مَعَهُ ۖ نُورُهُمْ يَسْعَىٰ بَيْنَ أَيْدِيهِمْ ۖ وَ** **بِأَيْمَانِهِمْ يَقُولُونَ رَبَّنَا أَتَيْنَاكَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ** (Sura At-Tahriim, 66:9) . Ndani ya aya hii imeelezwa kwamba wale watu wanaojaaliwa nuru duniani humu kwa fadhili ya Mwenyezi Mungu kwa kuifuata Islam na kumfuasa Mtume^{saw}, nuru hii jinsi inavyodumu pamoja nao duniani na kuwaongoza na kuwaangazia njia za ruhania, ndivyo ambavyo ndani ya akhera pia nuru hii haitatengana na mwaminio. Msifikirie kwamba kwa natija ya kuifuata Kurani Tukufu kikamilifu milango ya rehema zisizokoma hufunguliwa ndani ya dunia hii pekee, bali baada ya kifo pia rehema hizi haziwezi kuwekewa mipaka, wakati huo pia milango ya rehema itabaki kuwa wazi. Kwani, sehemu nyingine Akasema kuwa atakayekuwa kipofu katika dunia hii ndiye atakayekosa kuona huko Akhera pia. Hapa kwa mkabala wake pameelezwa madhumuni haya kwamba yule atakayekuwa na mwanga na nuru duniani humu, nuru hiyo itakwenda naye huko Akhera pia. Sio kwamba milango ya maendeleo ya ruhania itaendelea kuwa wazi duniani kwa mtu kama huyo, lakini itafungwa huko akhera; na huko kunakuwa ni wakati wa kula matunda baada ya mavuno, basi huko kutakuwa na wakati wa kula matunda, kule hakutakuwa na maendeleo zaidi.

Sivyo hivyo, bali Mwenyezi Mungu Ameiandalia roho ya binadamu njia kwamba ile nuru anayoipata kwa kuifuata Kurani Tukufu na kwa baraka za Mtume^{saw}, hiyo itaandamana naye baada ya mauti pia; huko pia Mwenyezi Mungu Ataendelea kumfungulia milango ya maendeleo na kudumu kuziangazia njia zake, na popote pale maendeleo ya ruhania hayataishia, kwani hamna kikomo cha umbali ulio baina ya mja na Mungu. Hivyo, daraja za ukaribu baina ya mja na Mungu zaweza kuwekewa mipaka. Ananena Hadhrat Masihi Mau^{as}:

“Katika aya hii, kauli hii kwamba watadumu kusema tutimizie nuru yetu inaashiria kwenye kuendelea daima mbele bila kukoma wakati wowote. Ndiyo kusema kwamba watakuwa na daraja la ukamilifu wa nuru, lakini kisha wataliona daraja la juu zaidi la nuru kamili, hapo ukamilifu wa kwanza watauona kuwa mpungufu, ndipo wataomba kupatiwa hilo daraja la pili la ukamilifu wa nuru. Na pindi watakapolipata hilo pia watadhihirikiwa na daraja la tatu la ukamilifu na hapo watauona ukamilifu wa hapo kabla kuwa si kitu na kwa hiyo watapenda kulipata hilo la tatu na kadhalika. Huo ndio upendo wa kudumu kupata maendeleo unaofahamika kutokana na neno ‘Tutimizie nuru yetu.’ Ilmuradi, mtu daima atasonga mbele wala hatarudi nyuma katu.”

(Hekima ya Mafundiho ya Kiislam uk. 146-147)

Basi, Kurani Tukufu ikadai hivyo na kuhakikisha pia kwa kitendo. Yaani, ndani ya Islam wakazaliwa maelfu na malaki ya waja watukufu wa Mwenyezi Mungu ambao kwa kupata mwanga toka kwa mapenzi ya Mtume^{saw}, ambao kwa kuchukua kimota cha huba ya Mwenyezi Mungu wakajipatia ile nuru ambayo kwayo wakapata maendeleo yasiyo na mwisho; na kile watakachopata huko Akhera walichoahidiwa, hata hatuwezi kukiwaza kama ilivyoielezwa ndani ya Hadithi kwamba neema hizo ni za namna za ajabu fika hata kwamba binadamu hawezi kuziwaza akiwa hapa duniani.

Maana ya nne, nilivyoishasema, ni kuwa na mwisho mwema, yaani kupata pepo na kupata makusudio ya maisha.

Mwenyezi Mungu Anasema: **أُولَئِكَ عَلَىٰ هُدًى مِّن رَّبِّهِمْ ۗ وَأُولَئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ** (Sura Al-Baqara, 2:6), yaani wale watu wayatekelezao mafundisho ya Kurani Tukufu, hawa wamekaa imara juu yake, nao wameimarika juu ya mwongozo uliokamilika ambao utunzi kamili wa Mola wao uliuteremsha. **وَأُولَئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ** — na hawa ndio wenye kupata ufaulu. Neno *Falaah* kwa Kiarabu lamaanisha ule ufaulu kamili fika ambao mbele yake ufaulu wowote mwingine hauwi ufaulu usiokuwa na kasoro, usiokuwa na dosari, ambao ndio ufaulu mkamilifu mno. Hivyo, Mwenyezi Mungu Amenena hapa kwamba wale wanaoimarika juu ya mwongozo wa Mola wao (Ambaye Akiwatunza katika zama za Mtume^{saw} Amewaleta kwenye daraja

mahususi ya juu na kuwajaalia vipawa na vipaji kamili), hawa ndio wanapata ufaulu kamili wa kweli na wanawatangulia watu wa nyimati zote za hapo zamani.

Hivyo, wakati huu nimeeleza kiasi fulani katika hotuba hii makusudio mawili yauhusuyo ujenzi wa Kaaba. Mosi, Mwenyezi Mungu Alitaka kuifanya Kaaba kuwa yenye baraka (*Mubarakan*). Kwa kutumwa Mtume^{saw}, Baitullah ikawa *mubarak* katika maana zote mbili. Pili, Mwenyezi Mungu Alitaka kupeleka sehemu hii mwongozo ulio Mwongozo kwa walimwengu wote, kwa sababu ya ukamilifu wa sheria pia, na kwa kuwanufaisha watu pia. Na ahadi hii vilevile ikatimia kwa njia ya Kurani Tukufu, waila kule Makka kulikuwa hamna sheria yoyote iwayo. Na sheria nyinginezo hazikutoa dai hili wala hazingeweza. Kurani Tukufu pekee ikatoa dai hili na kulithibitisha pia kwa kitendo. Na kwa fadhili ya Mwenyezi Mungu ndani ya Islam wakazaliwa maelfu na malaki ya waja watukufu ambao maisha yao ni dalili ya jambo hili kwamba yeyote aitiye Kurani Tukufu na kuifuata, ambayo Mwenyezi Mungu akaiita هُدًى لِلْعَالَمِينَ, mtu huyo anapata hadhi nyingi mno katika baraka za Mwenyezi Mungu, na mwisho wake huwa mwema. Na chochote kihitajikacho kwa nafsi ya binadamu kuifikisha kwenye ukamilifu na kutimiliza utakaso wake, kimo ndani ya Kurani Tukufu. Kwani waja hao wakazitekeleza amri za Kurani Tukufu, basi machoni mwa Mwenyezi Mugu uwepo wao ukawa wenye baraka na mkamilifu. Na ushuhuda wa kiamali wa

Makusudio 23 Adhimu ya Ujenzi wa Baitullah

Mwenyezi Mungu ndio huu kwamba kwa kweli hawa ndio watu waliomkaribia Munug na katika nyanja za ruhania kila saa hatua zao zinasogea mbele. Mwenyezi Mungu Atuingize na sisi pia katika kundi hili.

(Gazeti la Al-Fadhl, 14 Mei 1967)

⑤

**Baitullah
ni Chanzo cha Ishara Bayana
na Misaada ya Kimbingu
Itakayodumu Milele**

Hotuba ya Ijumaa, 12 Mei 1967,
Masjid Mubarak, Rabwah, Pakistan.

“Mwenyezi Mungu Alimwahidi Hadhrat Ibrahim^{as} ya kwamba Nyumba hii itakuwa ni chanzo cha ishara bayana na ishara za kimbingu na misaada ya kimbingu vitakavyodumu milele hata milele. Yaani, lengo la kuijenga lilikuwa ni kuleta umati wa Kiislamu ambao kupitia huo ishara za Mwenyezi Mungu zitaendelea kudhihiri duniani mpaka Kiama.”

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ¹⁰

تَحْمَدُهُ وَنُصَلِّي عَلَى رَسُولِهِ الْكَرِيمِ¹¹

Baada ya kutamka Shahada mbili, kusoma A‘udhu na Sura Al-Faatiha, Hudhurth alisoma aya hii:

فِيهِ آيَاتٌ بَيِّنَاتٌ مِّمَّا عَمُرَ إِبْرَاهِيمَ ۚ وَمَنْ دَخَلَهُ كَانَ آمِنًا ۗ وَلِلَّهِ عَلَى النَّاسِ حِجَابُ الْبَيْتِ مَنِ اسْتَطَاعَ إِلَيْهِ سَبِيلًا

(Aali ‘Imraan, 3:98)

Kisha akanena:

Mimi naendelea kueleza katika hotuba zangu makusudio yale 23 ambayo kwa kuyapata Mwenyezi Mungu Akaijengsha Kaaba juu ya misingi yake. Nami naendelea kuwaambia namna yalivyotimizwa makusudio haya kwa njia ya Mtume^{saw}. Kuhusiana na makusudio matatu nimeishawaambia marafiki zangu mawazo yangu.

Kusudio la nne la kujenga Kaaba, au yaweza kusemwa kwamba ahadi ya nne ya Mwenyezi Mungu kwa Hadhrat Ibrahimu^{as} ilikuwa ni فِيهِ آيَاتٌ بَيِّنَاتٌ . Nilisema kuwa ndani ya sentensi hii Mwenyezi Mungu Alimwahidi Hadhrat Ibrahimu^{as} ya kwamba Nyumba hii itakuwa ni chanzo cha ishara bayana na ishara za kimbingu na misaada ya kimbingu vitakavyodumu milele hata milele. Yaani, lengo la kuijenga lilikuwa ni kuleta umati wa Kiislamu ambao kupitia huo ishara za Mwenyezi Mungu zitaendelea kudhihiri duniani mpaka Kiama.

¹⁰ Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema na Mwingi Ukarimu.

¹¹ Twamhimidia Yeye na kumsalia Mtume Wake mhashamu.

Kurani Tukufu imedai kwamba kwa kuifuata Kurani tu, mlango huu umefunguliwa hadi Kiama, na kwamba ndani ya kila kaumu na kila zama wataendelea kuzaliwa watu watakaojipatia hadhi katika baraka zake, na Mwenyezi Mungu Atadumu kudhihirisha ishara zake kuwapitia hawa.

Manabii wa zamani pia walijaaliwa Ishara bayana, lakini hizo ishara bayana zilihusiana na kaumu zao na zama zao pekee, sio na wanadamu wote wala na zama zote. Lakini ndani ya aya hizi imeelezwa kuwa haya ni makusudio yahusianayo na wanadamu wote, mataifa yote na zama zote. Ndiyo sababu madhumuni haya yameanzia na اللّٰكۡسِ katika إِنَّ أَوَّلَ بَيْتٍ وُضِعَ لِلنَّاسِ – Nyumba ya kwanza iliyowekwa kwa ajili ya wanadamu wote.

Basi, ijapokuwa nyimati za awali pia zilipewa ishara bayana; lakini zile ishara bayana zihusianazo na kila kaumu na kila zama, alijaaliwa Mtume Muhammad^{saw} pekee. Mwenyezi Mungu Analonga ndani ya Kurani Tukufu: (Sura Al-‘Ankabuut, 29:50). Ndani ya aya hii tukufu madhumuni haya yameelezwa kwamba kwa nguvu takatifu ya Mtume Muhammad^{saw}, watu wataadumu kujaaliwa elimu timilifu na maarifa kamili, na kwa sababu ya maarifa kamili hofu ya Mola wao itakuwemo ndani mwa nyoyo zao na kimatokeo watazalishiwa nyoyoni mwao mapenzi kamili ya Mola wao, nao watakuwa wenye kumheshimu Mola wao. Hivyo, kwa kuwa watu

kama hao wataendelea kuzaliwa, basi zile ishara bayana zihusianazo fika na Kurani Tukufu, bali yaweza kusemwa Kurani Tukufu imeundwa kutokana na ishara bayana, nazo zitadumu kutokeza vifuani mwao na dunia itaendelea kung'arika na nuru ya Kurani Tukufu. Lakini watazaliwa katika umati wa Kiislamu pia watakaokuwa dhalimu na watajifungia milango ya baraka za Kurani Tukufu, bila shaka ishara bayana hazitadhihirika kwa njia ya hawa. Lakini **أَوْثُوا الْعِلْمَ** , yaani wale watu watakaojaaliwa elimu kamilifu, hawa wataadumu kuzaliwa ndani ya umati wa Kiislamu na mlango wa ishara bayana utabaki wazi kwa umati wa Kiislamu.

Haya siyo madai tu, bali historia ya Islam ni shahidi juu ya jambo hili kwamba Mwenyezi Mungu Ameijaza tele ardhi na mbignu na kila zama ishara za kuthibitisha ukweli wa Islam na Mtume Muhammad^{saw}. Hadhrat Masihi Mau'udi^{as} amesema:

“Alama ya pili ya dini ya kweli ni kwamba isiwe dini iliyokufa, bali zile baraka na adhama ambazo mbegu zake zilipandwa mwanzoni, baraka hizo zote na adhama zidumu mpaka mwisho wa dunia kwa ustawi wa binadamu, ili ishara za hivi sasa zikizisadikisha ishara za zamani, zisifanye nuru ya ukweli huo kudhaniwa kuwa ilikuwa ni kisa tu. Hivyo, naendelea kuandika tangu muda mrefu kwamba ule Unabii alioidai Seyidna wa Maulana Muhammad Mustafaa^{saw} na zile dalili za ishara za

Makusudio 23 Adhimu ya Ujenzi wa Baitullah

kimbingu alizotoa yeye, hizo zote zipo mpaka sasa na wanazipata wamfuatao ili wapate kufikia daraja ya maarifa na kumwona Mungu mmoja kwa moja.”

(Tablighe Risaalat, J. 6, uk. 14 na Tangazo la 14 Januari 1897)

Kadhalika Hadhrat Masihi Mau‘udi^{as} amesema ndani ya *Tasdiikun Nabii*:

“Muujiza wa nne wa Kurani Tukufu ni athari zake za ruhania zinazoendelea kuhifadhiwa ndani mwake kwa kudumu. Yaani, waifuatao hufikia daraja za kukubaliwa na Mungu na wanapata heshima ya maongezi na Mungu. Mwenyezi Mungu Anasikiliza dua zao na kuwajibu kwa huba na rehema na kuwaambia baadhi ya siri za ghaibu kama awaambiavyo manabii, na Anawapambanua baina ya mahuluku wengine kwa ishara za msaada wake na nusura yake. Hii pia ni alama itakayodumu ndani ya umati wa Muhammad^{saw} na kudhihiri daima dawamu, na hata sasa pia ipo na inathibitika.” (uk. 23)

Tena ndani ya *Kitabul Bariyyah*, Hadhrat Masihi Mau‘udi^{as} anasema:

“Kadiri zilivyodhihirika ndani ya Islam ishara za kimbingu za Mawalii wa umati huu na kuendelea kudhihirika kusaidia Islam na kushuhudia ukweli wa Mtume^{saw}, hamna mfano wake asilani katika

dini zingine. Ni Islam pekee inayoendelea kuzidi kustawi siku zote kupitia ishara za kimbingu. Nuru zake na baraka zake zisizohesabika zimetuonyesha Mwenyezi Mungu kwa kumleta karibu nasi. Fahamuni kwa yakini kuwa Islam katika zama zozote haiabiki, kwa sababu ya ishara zake za kimbingu.”

(Kitabul Bariyyah, uk. 67, chapa ya kwanza)

Baadaye, sehemu hiyo hiyo Hadhrat Masihi Mau'udi^{as} amejiweka mbele ya dunia. Kupitia Masihi Mau'udi^{as}, Mwenyezi Mungu Amedhihirisha malaki ya ishara bayana. Na dhati ya Masihi Mau'udi^{as}, kila saa ya maisha yake, ilishuhudia waziwazi ukweli wa Islam. Ishara mpya mpya za kimbingu zilikuwa zinateremka kama mvua. Mwenye chuki alinyimwa kuziona ishara hizo. Mwenye lubu kidogo, mwenye ufahamu kiduchu, asiye na chuki, alikuwa hawezi kuzikataa ishara hizo. Ishara hizi bayana hazikuishia kwa Hadhrat Masihi Mau'udi^{as}, bali kwa kuhuisha dini, Islam imepata nguvu mpya, na ule mlango waliojifungia watu kwa ujahili wao, akathibitisha Hadhrat Masihi Mau'udi^{as} kuwa upo wazi, haukufungwa. Baada yake, mfululizo wa ishara unaendelea kupitia makhalifa wake. Maisha ya Hadhrat Khalifa wa Kwanza^{ra} yalikuwa ni maisha ya wale waliosemwa na Mwenyezi Mungu ndani ya aya iliyotajwa kuwa **أَوْتُوا الْعِلْمَ**. Ndivyo ilivyokuwa hali ya Hadhrat Muslih Mau'udi^{ra}. Dunia iliziona ishara mamia

na maelfu kumpitia yeye. Na mlango huu haukufungwa hata sasa. Siku chache zimepita, nilikuwa ninafanya *Istighfar* baada ya sala ya Alfajiri, hofu ya aina fulani ilikuwa imenitawala, nami nilikuwa naomba maghufira, mara nikahisi kwamba nimetawaliwa na nguvu fulani ya ghaibu na nikatamkishwa “**قِيَامِ دِينٍ**” – uimara wa dini – na kwa msukumo uliotikisisha mwili wangu mzima nikazinduka. Nikafahamishwa kuhusiana na hii kwamba ule mpango ninaoukilia kuuweka mbele ya Jumuiya kupitia hotuba zangu hizi, Mwenyezi Mungu Ataimarisha dini ya Kiislamu kwa njia hii na Ataandaa nyenzo za kuistawisha, inshallah.

Hivyo, kuna maelfu ya ishara ambazo Mwenyezi Mungu Ameanzisha kudhihiri mfululizo kupitia Ukhaliifa wa Masihi wa Muhammad^{saw}. Lakini kumbukeni kwamba kwa kuwa Khalifa huwa katika daraja ya kujipoteza ndani ya Mungu, hivyo mara nyingi hadhihirishi yale maneno Asemayo Mwenyezi Mungu kuonyesha upendo kwa mja wake, isipokuwa yale mambo yahusianayo na Jumuiya na huwa lazima kusemwa. Basi, naweza kusema kwa tajiriba yangu kwamba Mwenyezi Mungu Aliendelea kuwakataza kudhihirisha daraja yao ya ukaribu na Mungu. Nimefikia natija hii kwa uzoefu wangu, kauli fulani ya Hadhrat Masihi Mau‘udi^{as} na ushuhuda wa historia. Historia imehifadhi ishara bayana chache tu za Makhalifa Rashidiin waliopita. Mathalani, nifikirivyo ishara za Hadhrat Umar^{ra} hazikuelezwa zaidi ya tano. Yaani, katika matabiri au bishara alizopewa,

zimehifadhiwa chache tu katika historia, wala si nyingi. Lakini Hadhrat Masihi Mau'udi^{as} amesema kuwa Ma-Khalifa Rashidiin hao watukufu walipewa bishara maelfu na kufanyiwa maongezi na Mungu mara malefu.

Kauli ya Hadhrat Masihi Mau'udi ni haki na kweli, haiwezi kukanwa, lakini historia imenyamaa. Ndiyo kusema kwamba waja hao walikuwa hawadhihirishi mambo hayo hadharani, isipokuwa wakati ufaao, tena yale yaliyohusiana na nidhamu ya Jumuiya, na kuyaeleza yalio kuwa jambo la lazima. Mathalani, wakati fulani Hadhrat Khalifa wa Pili^{ra} alisema – ilipokuwa imechochewa fitina na ufisadi dhidi ya Jumuiya – ya kwamba yale mambo ninayojua, nikiwaambia, itakuwa vigumu kwenu kubaki hai. (sikumbuki maneno yenyewe, lakini yalikuwa na maana kama hii).

Naendelea kuwaambia kwamba ahadi ya **فِيهِ آيَاتٌ بَيِّنَاتٌ** aliyoahidiwa Hadhrat Ibrahimu^{as}, mwenye kuitimiza ndiye Muhammd^{saw}, Mtume wa Mungu, na historia ni shahidi juu yake. Kisha katika maisha ya Hadhrat Masihi Mau'udi^{as} dunia ikashuhudia malaki ya ishara, na baada yake kwa njia ya Makhalifa wake pia. Na kupitia waja wengine vilevile waliopo ndani ya Jumuya Ahmadiyya Mwenyezi Mungu huwa Anadhihirisha ishara. Na kwa baraka ya Hadhrat Masihi Mau'udi^{as} uhakika huu umekwishathibitika kwa waumini wake waziwazi ya kwamba mambo ya aina hii hayapaswi kudhihirishwa,

kwani yanasababisha majisifu, na pengine kunakuwa na hatari kwa mtu kukasirikiwa na Mwenyezi Mungu.

Basi, inathibitika kutoka ndani ya Kurani Tukufu na kwa mfano uliohifadhiwa katika historia, wa Mawalii wa umati, na jinsi Mwenyezi Mungu Alivyoendelea kuwatendea wapenzi wa Mtume^{saw} na wenye kujitoa katika njia Yake – na jambo hili haliwezi kukanushwa – kwamba ishara bayana zipo ndani ya mataifa yote na zama zote, nazo zinahusiana na Waislamu tu; dini zingine haziwezi kutoa dai hili wala haziwezi kulithibitisha.

Kusudio la tano la kujenga Kaaba lililoelezwa ni **مَقَامُ إِبْرَاهِيمَ**. Iliahidiwa kwamba kupitia daraja ya Ki-Ibrahimi^{as}, Jumuiya moja ya wapenzi wa Mungu itaendelea kazaliwa ambayo kwa kutengana na uhusiano wote wa kidunia na kwa kutoa dhabihu ya matamania yake yote itapta daraja ya kujipoteza ndani ya Mungu. Kwa kuwaza na kuwazua, itahakikika kwamba kwa sababu ya ishara bayana tu daraja ya Ibrahimi^{as} yaweza kupatikana, la sivyo, hapana. ‘Ishara bayana’ na daraja ya Ibrahimi^{as} zinao uhusiano wa keto. Na kwa kuwa ndani ya umati wa Muhammad^{saw} siku zote ipo bahari moja yenye mawimbi ya ishara bayana, hivyo ikawezekana ndani ya umati wa Muhammad^{saw} kupatikana maelfu na malaki ya watukufu wenye kupata daraja ya Ibrahimi^{as}. Kwa hakika daraja ya Ibrahimi^{as} ni kivuli cha daraja ya Muhammad^{saw}. Haiwezekani kufikia daraja ile kabisa

iliyo daraja ya Mtume^{saw}, lakini baada yake iliyo daraja ya pili ndiyo daraja ya Ibrahimu^{as}. Hadhrat Ibrahimu^{as} alipata sehemu ya ishara bayana kwa sura ya kivuli. Kurani Tukufu imedai kwamba miongoni mwa waniaminio watazaliwa wengi watakaojipatia daraja hii. Daraja hii ya **قُلُوبًا** – kijipoteza ndani ya huba ya Mungu – ni nini? Kuihusu amesema Hadhrat Masihi Mau‘udi^{as}:

“Ipo daraja moja ya mapenzi ya dhati ambayo waifuatao Kurani Tukufu kikamilifu wanaimarika juu yake. Na mapenzi ya Mungu hupenya ndani ya vena na mishipa yao hata yakawa ni uhakika wa uwepo wao, bali huwa uhai wa uhai wao. Huba ya ajabu kwa Mpendwa wa kweli hufurika nyoyoni mwao, na mahaba na shauku kubwa isiyo ya kawaida inazitawala nyoyo zao zilizotakata, inayowatenganisha na wengine. Na moto wa mapenzi ya Mungu unawaka namna ambavyo katika nyakati mahususi unashuhudiwa na kuhisiwa waziwazi na waja washiriki... Na alama kuu ya daraja yao kamili ni hii kwamba hawa wanamtanguliza Mpenzi wao wa kweli juu ya kila kitu kiwacho chochote. Wakipata mateso toka Kwake, huyaona ni neema, na kuichukulia adhabu kuwa sharubati tamu. Makali ya upanga wowote hayawezi kuwatenganisha na Mpendwa wao, na jaribio lolote kubwa fika haliwezi kuwazuia kumkumbuka Mpendwa wao. Wanamfahamu Yeye kuwa ni uhai wao, nao huona ladha ndani ya

upendo Wake, na wanaufikiria uwepo Wake ndio uwepo hasa, na wanafahamu kumkumbuka ni kusudio la maisha yao. Kupenda, humpenda Yeye; kuona raha, huona toka Kwake; katika ulimwengu mzima wanakuwa Naye, nao wanakuwa Wake; huishi kwa ajili Yake na hufa kwa ajili Yake. Wkikaa ulimwenguni, hawamo ulimwenguni. Ingawaje wawepo, hata hivyo hawajijui. Hawajali heshima, jina, wala uhai wao wala starehe yao, bali huwa wanajinyima vyote kwa ajili ya Mmoja; na ili kujipatia Mmoja, huwa wanatoa vyote. Huungua kwa moto usiojulikana, na hawawezi kueleza kwa nini wanaungua. Hao kufahamishwa na kufahamu huwa viziwi na mabubu. Hujiweka tayari kuvumilia kila msiba na fedheha, nao hupata ladha ndani yake.”

(Baraaahine Ahmadiyya, J. 4, uk. 450-451, maelezo ya maelezo ya pembeni Na. 3)

Kadhalika, Hadhrat Masihi Mau‘udi^{as} amechora hivi taswira ya Jumuiya hii takatifu na amesema sawa na ahadi ya Ibrahim^{as} kuafikiana na zile bishara ambazo Mwenyezi Mungu Akampa Mtume Muhammad^{saw} ya kwamba:

“Ni uzoefu wa malaki ya watakatifu kwamba kwa kuifuata Kurani Tukufu baraka za Mungu huutermkia moyo na mwungano wa ajabu hufanyika na Mola Mkarimu... Na mapenzi ya

Mungu yaliyolelewa ndani ya ladha ya kuungana na Mugu hutiliwa nyoyoni mwao. Kama hao wasagwe ndani ya kinu cha misiba na kukamuliwa ndani ya mtambo wa kusindika, ariki yao itakuwa huba ya Mungu, na si kitu kingine. Dunia haiwatambui, nao wako mbali kabisa na dunia na juu fika”.

(Surma Chashme Aria, maelezo ya pembeni, uk. 31)

Hii ndiyo daraja ya Ibrahimu^{as} aliyoahidiwa yeye. Bishara yake akaipata Mtume Muhammad^{saw} toka kwa Mola wake. Na Mwenyezi Mungu Aliye Mwenye kutoa ahadi za kweli Akaithibitisha kuwa ya kweli na Akaumba ndani ya umati wa Kiislamu malaki ya waja wake waliokuwa wenye kufikia daraja ya Ibrahimu^{as}.

Ahadi ya sita aliyoahidiwa Hadhrat Ibrahimu^{as} imeelezwa ndani ya kipande hiki cha aya hizo وَمَنْ دَخَلَهُ كَانَ أَوْيًا . Niliwaambia kwamba muradi wake ni kuwa atakayeingia Baitullah, yaani atakayetokeleza zile ibada zihusikanazo na Nyumba hii ya Mwenyezi Mungu, yeye mtu huyo ataingia katika hifadhi ya Mungu dhidi ya jahanamu ya dunia na ya Akhera na atasamehewa dhambi zote zilizopita, na atasalimika na moto wa jahanamu. وَمَنْ دَخَلَهُ كَانَ أَوْيًا , atakayeingia katika Nyumba hii atakingwa na moto (Aliouwasha Mwenyezi Mungu kwa wakanao). Hivyo, Ananena ndani ya Sura An-Naml 27:90 kwamba وَهُمْ مِنْ فِرْعَ يَوْمِيذِ أَوْيُونَ , yaani wenye kutenda matendo mema sawa na maagizo ya Kiislamu watapewa na Mwenyezi Mungu malipo mema na bora, na hao

watu watasalimika na hofu ya jahanamu katika saa ya kupigwa parapanda. Wakati ule Mwenyezi Mungu Atawatolea habari njema ya kuwa hamtapelekwa kwenye moto wa jahanamu, bali mtaongozwa kenye pepo, hivyo msiwe na hofu yoyote.

Kadhalika, sehemu nyingine Mwenyezi Mungu akanena *إِنَّ الْمُتَّقِينَ فِي جَنَّاتٍ وَعُيُونٍ* (Sura Al-Hijr 15:46-47). Wacha Mungu wataingia penye bustani na chemchem, nao wataambiwa ingieni humo kwa amani pasipo hofu wala hatari. Basi, hii ndiyo amani wanayojaaliwa wafuasi kamili kwa njia ya Kurani Tukufu.

Alisema *مَنْ دَخَلَهُ كَانَ آمِنًا* , maneno haya haya Mwenyezi Mungu alimwambia Mtume Mtukufu^{saw} na Akasema Tulikuahidi *لَتَدْخُلَنَّ الْمَسْجِدَ الْحَرَامَ إِنْ شَاءَ اللَّهُ آمِنِينَ* (Sura Al-Fat'h 48:28), yaani mtaingia Masjid Haraam kwa amani . Na ahadi hii ikatimia.

Kuna maelezo yake ya kidhahiri kwamba Mwenyezi Mungu Akaandaa sababu za ushindi wa Makka, na makafiri wa Makka (waliotumia maisha yao yote kuifuta Islam) wakasarenda bila vita kupiganwa, na malaika walioshuka toka mbinguni wakatilia nyoyoni mwao hofu sana, nao wakawa na moyo wa bua.

Lakini hii ina maana nyingine pia ya kwamba nyinyi ndinyi ule umati wenye kutimiza ile ahadi aliyoahidiwa Hadhrat Ibrahimu^{as} katika maneno haya *وَمَنْ دَخَلَهُ كَانَ آمِنًا* , atakayeingia humo ataingia ndani ya amani. Ahadi hii ikatimia kupitia ninyi. Nimeishaeleza bayana kwamba

ahadi hizi zote zinahusiana na wanadamu wote, mataifa yote na zama zote; hazihusikani na tafia fulani mahususi wala zama fulani maalum.

Hivyo, **مَنْ دَخَلَهُ كَانَ أُمَّتًا** yamaanisha kuwa mtu yeyote awaye atakayetekeleza ibada za hija, bila kujali anahusiana na taifa gani au zama zipi, atahifadhiwa na moto wa jahanamu. Ndani ya Hadithi, imesimuliwa na Hadhrat Abu Huraira^{ra} kwamba Nabii Mtukufu^{saw} alisema:

مَنْ سَخَّ فَلَمْ يَزِفْ وَلَمْ يَفْسُقْ غُفِرَ لَهُ مَا تَقَدَّمَ مِنْ ذَنْبِهِ

(kumbukeni kwamba kwa Kiarabu **يَزِفُ** , **يَزِفُ** na **يَفْسُقُ** , **يَفْسُقُ** yanatamkwa kwa njia zote mbili). Yaani yule atakayeepukana na maneno mabaya na machafu, yaani yule anayehiji na kuepukana na kusema maneno machafu wakati wa kuhiji – maana yeke ni kwamba undani wake umetakata kiasi hiki kwamba maneno machafu hayawezi kabisa kutamkwa na ulimi wake, sio maana yake kwamba katika miezi kumi na mmoja na siku kadha zilizobaki aendeleo kusema maneno machafu na ajiepushe tu nayo katika siku chache za hija, bali inamaanisha kwamba uchafu umekwishatoweka kifuni mwake kabisa hata kwamba neno chafu lisiweze kutamkwa na mdomo wake, na asiwe mwenye kuachana na njia ya haki na usuluhisho, yaani asivuke mipaka ya sheria, bali ailinde barabara na atimize haki ya utii – basi, yule atakayefanya hija ya Baitullah kwa nia halisi na vitendo halisi na kwa adabu njema, Mwenyezi Mungu Amemwahidi kwamba dhambi zake

zote zilizopita zitasamehewa, na aliyesamehewa dhambi zake zote za zamani, bila shaka ameokolewa katika moto wa jahanamu.

Kwa njia nyingine pia mtu anasalimika katika moto wa jahanamnu ndani ya dunia hii pia na huku akhera vilevile, nayo ni kwamba aingiaye katika **مَقَامِ إِبْرَاهِيمَ** , huiniga ndani ya amani.

Hadhrat Masihi Mau‘udi^{as} amenena:

“Mungu ana kudura za ajabu zisizokoma... Lakini wale tu wanafumbuliwa hizi kudura wanaokuwa Wake tu. Na wanazishuhudia ajabu hizi wale tu wanaojiletea ndani mwao mabadiliko matukufu na huangukia kizingitini pake, nao hutakata kama lile tone linalofanyika kuwa lulu, na kwa harara ya mapenzi na ukweli na usafi wakiyeyuka huanza kuturirika upande Wake, ndipo Yeye Huwasaidia katika shida zao na kwa njia ya ajabu Huwakinga na njama na hila za adui na kuwahifadhi na dhila, na Huwa Msimamizi na Mdhamini wao. Yeye Huwasaidia katika mishkili ambapo mtu yeyote hawezi kusaidia, na majeshi Yake huja kuwahami. Shukurani nyingi ilioje kwamba Mungu wenu ni Mkarimu na Mweza. Je mtamwacha Mpendwa kama Yeye? Je, kwa ajili ya nafsi yenu chafu mtavunja mipaka yake? Ni afadhali kwetu kufa kwa kupata radhi yake kuliko kuishi maisha machafu.”

(Ayyaamus Sulh, uk. 104)

Hii ndiyo amani anayojipatia yule ambaye akijifia hujivalia vazi la kutokuwepo na anaingia katika daraja ya Ibrahimu^{as}, hapo ndipo majeshi ya Mwenyezi Mungu huteremka toka mbinguni na kumhifadhi na adhabu za kila namna. Mwenyezi Mungu Haifanyi mioto miwili kuwatawala waja wake. Wapo waja wake wajipatiao daraja ya kutokuwepo kwa kuungua ndani ya moto wa mapenzi ya Mungu, hapo hufungiwa milango ya moto mwingine. Na wapo watu wake wengine wasiojali mapenzi Yake, wasiomshukuru kwa upendo Wake, wasio na shukurani kwa rehema zake, wanaompa kisogo na kuielekea dunia, na badala ya kumpenda Yeye wanaipenda dunia, badala ya kumfanya Yeye kuwa Mpendwa wao huwa wanayapenda mambo na mahusiano ya kidunia. Watu kama hawa hawateremkiwi na hifadhi ya Mungu, wala majeshi Yake hayashuki kwa kuwapa amani. Bali, watu hawa hufunguliwa milango ya jahanamu, na moto wa jahanamu huwa makazi yao.

Hivyo, waja wa Mungu hawaangukiwi na mioto miwili. Sasa ni juu yao waupende moto wa Mapenzi ya Mungu na kuchomelea mbali uchafu wao, nafsi yao, matamaniao yao, uwepo wao, mapenzi yao yote, mahusiano yote na mafungamano yote, au waitangulize huba ya dunia juu ya mapenzi ya Mungu na kujifungulia kwa mkono wao milango ya jahanamu.

Ahadi ya saba aliyoahidiwa Hadhrat Ibrahimu^{as} ilikuwa ni kwamba faradhi ya kuhiji haitakuwa kwa wazao wako

tu, bali hapa atatumwa Nabii ambaye sheria yake itakuwa kwa ajili ya mataifa yote. Na baada ya kuteremka sheria ile, kuhihiji itakuwa ni faradhi ya mataifa yote ya ulimwengu, na kwa njia hii Baitullah itafanywa kuwa mahali pa kurejea kwa halaiki na ulimwengu. Twaona kuwa kabla hajatumwa Hadhrat Mtume^{saw}, ahadi hii haikutimia. Pindi alipotumwa Mtume^{saw} na akateremkiwa na sheria ya Kurani, ndipo kwa njia ya sheria hii Mwenyezi Mungu Akafaradhisha hija kwa wanadamu wote. Mwenyezi Mungu Ananena ndani ya Sura Al-Baqara, 2:198 **الْحَجُّ أَشْهَرُ مَعْلُومَاتٍ فَمَنْ قَرَضَ فِيهِنَّ الْحَجَّ** yaani, Enyi wanadamu, kumbukeni kuwa miezi ya hija inajulikana. Basi, anayekusudia kuhiji katika miezi hiyo, yeye mtu huyo ndani ya siku za hija (kama ndani ya siku zingine pia) asisema maneno kuhusu nyege wala uasi, wala asitukane wala asibishane. Haya hayatakuwa halali kwake. Kisha Akasema, tendo lolote jema mtakalolifanya, Mungu Atalithamini. Yeye Hataona kuwa mnahusiana na watu weupe au watu weusi; bali hata mkihusiana na tafia lolote, wakazi wa sehemu yoyote ya ardhi, mtakapoitikia mwito wa Mwenyezi Mungu wa kuhiji mkiona ni ibada ya lazima na mtakapotimiza sharti zote zihusianazo na hija na mtahiji kwa kujua faradhi hii kuwa ni faradhi, na wakati wa kuhiji mtaangalia maagizo yote Aliyowaagizeni Mwenyezi Mungu kuhusiana na jambo hili, basi sikilizeni Enyi binadamu wote kwamba kitendo

chochote chema mtakachotenda, heshima yenu itaimarika machoni mwa Mwenyezi Mungu, Yeye Atatambua mema yenu. Chochote hakipo ghaibu machoni Mwake, na mtarithi neema zisizohesabika kwa sababu ya kuthaminiwa kwenu. Hadhrat Masihi Mau‘udi^{as} alisema kwamba hija sio tu jina la kutimiza ibada za dhahiri za hija, bali nyuma ya kila ibada ya Kiislamu kuna roho yake. Ibada ya dhahiri ni kama mwili, huo una roho yake; asiyeijali roho, bali aupenda mwili tu, yeye anamwabudu mfu. Yeye hatapata thawabu ya zile ibada ambazo hakuijali roho yake, bali Mola wake Atamtenda jinsi apasavyo kutendwa mwenye kuabudu kaputi. Hadhrat Masihi Mau‘udi^{as} amesema kuhusiana na hija:

“Jambo la hakika ni kwamba hatua ya mwisho ya anayesafiri kwenda kumlaki Mungu ni kwamba kwa kujitenga na nafsi yake ajipoteze ndani ya mapenzi na huba ya Mungu. Mwenye huba na mapenzi ya kweli huwa anatoa dhabihu ya uhai wake na ya moyo wake; na kuizunguka Baitullah ni alama ya kidhahiri ya dhabihu hii. Kama Baitullah moja ilivyo juu ya ardhi ndivyo ilivyo moja kama hii huko mbinguni. Mpaka mtu aizunguke ile, hii haipati kuzungukwa. Mwenye kuizunguka hii anavua mavazi yake yote na anakuwa na shuka tu mwilini, lakini kuizunguka ile (ya mbinguni) mtu anavua mavazi yote anakuwa rabana kwa ajili ya Mungu. Kuzunguka ni alama ya mwenye

kumpenda Mungu sana mno. Wampendao humzunguka, kana kwamba hawanayo matakwa yao yoyote, huwa wanajitolea dhabihu yao pembezoni mwake.”

(Mir'aatul Hakaaik, J. 3, Imekusanywa na Muhammad Afdhal
Changawii, uk. 26)

Hivyo, hii ndiyo hija ya kimbingu, maadamu mtu haihiji ile Baitullah, hija ya Baitullah ya ardhi pia haikubaliki. Basi, wenye kwenda kuhiji, wenye kunuia kuhiji, wanapaswa wasisahau nukta hii. Ibada za dhahiri tumezitekeleza, na kuhusu ibada za batini hukumu inatolewa na Mungu, kuhusu hizi hatuelewi zimepokelewa au hapana. Basi, baada ya ibada ya kidhahiri kwa nini yazalike majisifu, fahari, majivuno, maringo na kiburi? Hayo yanampeleka mtu mbali zaidi na Mola wake. Kama kuna sababu ya kutoa shukurani na ziimbwe nyimbo za kumhimidia Mungu, ni sawa. Lakini hii pia iwe jinsi alivyosema Hadhrat Masihi Mau'udi^{as} kwamba mja mpendwa wa Mugu anapokuwa katika sijida akilia kwa unyenyekevu mbele ya Mungu, wakati huo kama mtu mwingine apate kumwona, basi mja huyo anaona haya moyoni mwake jinsi anavyoona haya mtu yule anayepata kuonwa na mwingine akishughulikia uhusiano wa kidunia usio halali.

Basi, mambo haya ya mapenzi hayafai kudhihirishwa. Mambo ya mapenzi huwa siri baina ya mja na Mola wake. Kwa hiyo, Hadhrat Masihi Mau'udi^{as} ananena

Makusudio 23 Adhimu ya Ujenzi wa Baitullah

kwamba dunia haiwatambui, kwani hawa huwa mbali na dunia, na juu sana kuliko dunia. Lakini yule mtu anayetaka kuisogea dunia akimwacha Mwenyezi Mungu, na akiachana na daraja adhimu za juu na kuinama kwenye ardhi ili ajulikane duniani na asifiwe, basi mtu huyo akaikaribia dunia lakini akawa mbali na Mwenyezi Mungu na akapoteza daraja za juu za ruhania. Mwenyezi Mungu Amhifadhi kila mmoja kati yetu na jambo hilo. Na jinsi Mwenyezi Mungu Alivyompa Hadhrat Ibrahim^{as} ahadi zake, na Hadhrat Muhammad^{saw} Mtume wa Mungu alivyoutolea umati wake bishara, basi sawa na bishara hizo malaki ya waja watukufu wameishazaliwa na wanaendelea kuzaliwa na watazaliwa siku zijazo, Atujumishe sisi ndani ya kundi la watukufu hao na Atudumishe humo. Hatuhitaji kusifiwa na dunia, lakini Mungu Afanye hivi kwamba wema wetu wa moyoni hata kama ni sawa na punje ya haridali Aitambue, Atupatie badala ya wema huu, ulio sawa na punje ya haridali, mapenzi yake na upendo wake na Aturidhie. Amin.

(Gazeti la Al-Fadhl, Rabwah, 21 Mei 1967)

⑥

**Ahadi ya Mungu Kuimarisha
Umoja Baina ya Mataifa kwa
Kuwajibuisha Mataifa yote ya
Ulimwengu Kwenye Makao
Makuu ya Tauhidi**

Hotuba ya Ijumaa, 19 Mei 1967,
Masjid Mubarak, Rabwah, Pakistan.

“Jinsi mwanzoni Kaaba ilivyokuwa makao makuu ya ubinadamu ndivyo ilivyokusudiwa Nyumba hii ya Mungu kuwa makao makuu ya umoja wa binadamu katika zama kamilifu za mwisho, na Baitullah ikachaguliwa kwa kutumwa huko Mtume Muhammad^{saw}, Mkuu wa manabii wote, ili Nabii wa kuleta umoja wa kibinadamu na Kibla cha umoja wa kibinadmau vikusanyike vyote viwili mahali pamoja.”

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ¹²

تَحْمَدُهُ وَنُصَلِّي عَلَى رَسُولِهِ الْكَرِيمِ¹³

Baada ya kutamka Shahada mbili na kusoma A‘udhu na Sura Al-Faatiha, alisoma aya:

وَإِذْ جَعَلْنَا الْبَيْتَ مَثَابَةً لِّلنَّاسِ وَأَمْنًا وَاتَّخِذُوا مِن مَّقَامِ إِبْرَاهِيمَ مُصَلِّينَ

(Al-Baqara 2:126)

Kisha akanena:

Miongoni mwa makusudio 23 Aliyotaja Mwenyezi Mungu ndani ya zile aya za Kurani Tukufu, ambazo sehemu yake nimesoma hivi sasa pia, nimeishafafanua kuhusiana na makusudio saba hapo kabla ndani ya hotuba zangu, nami nilikwishaeleza namna makusudio haya yalivyotimia kwa kutumwa Mtume^{saw}.

Kusudio la nane lililotajwa hapa limeelezwa ndani ya neno مَثَابَةٌ. Nilisema kuwa hili ni kusudio la nane la kujenga upya Kaaba, nalo ni kwamba atainuliwa sehemu hii Mtume mmoja atakayeyafanya mataifa yote ya ulimwengu kuwa umati mmoja, na sheria moja itateremka ambayo kwa njia yake mataifa yote yaliyosambaratika yatakusanywa kwenye makao makuu ya Tauhidi na makao makuu ya utakaso. Kusudio hili nalo likatimia pia kupitia Nabii^{saw} kutumwa.

¹² Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema na Mwingi wa Ukarimu.

¹³ Twamhimidia Yeye na kumsalia Mtume Wake mhashamu.

Maana moja ya **مَغَابَةٌ** ni **مُجْتَمِعُ النَّاسِ بَعْدَ تَفَرُّقِهِمْ** (Al-Kamusul Muhit), mahali wanapojumuika watu baada ya kutawanyika na kufarakana panaitwa **مَغَابَةٌ**.

Maana yake ya pili ni **مَكَاثِمًا يُكْتَبُ فِيهِ الشَّوَابُ**, mahala wanapoandikiwa watu thawabu, malipo na jaza.

Hapa Mwenyezi Mungu Amesmea kwamba Tunakusudia kuifanya Baitullah hii, baada ya kumwinua Nabii Mtukufu^{saw}, kuwa kitovu ambapo mataifa yote ya dunia yaliyosambaratika yatajumuika, na hayatabakiwa na mahali popote pengine panapotarajiwa kupata thawabu kwa Mola wao.

Nilivyosema, ili kutimiza shabaha hii, Mwenyezi Mungu Alimtuma Mtume Muhammad^{saw} na kuteremsha sheria ya Kiislamu. Na kama Kaaba ilivyokuwa makao makuu ya ubinadamu mwanzoni – kwani katika zama za Nabii Adamu^{as} kulikuwa na Nabii mmoja tu, na kaumu ilikuwa moja tu na sheria nayo ilikuwa moja tu, binadamu walikuwa hawajapata kuenea duniani na hawakugawanyika katika mataifa, hivyo Kaaba ndiyo iliyokuwa kitovu cha ubinadamu kiruhania; baadaye wazao wa Adamu^{as} wakaanza kutapakaa duniani na wakajikalia ndani ya maeneo ya mbali sana, hivyo uhusiano uliokuwa baina yao ukakatika, na Mwenyezi Mungu Akaanza kutuma manabii na mitume mbalimbali kwa kaumu mbalimbali kwa ukuaji wao wa ruhanian, na hivyo hawakubaki kuwa kaumu moja bali wakatawanyika na kufarakana na wazao wa Adamu^{as}

wakagawanyika katika kaumu mbalimbali, basi jinsi mwanzoni Kaaba ilivyokuwa makao makuu ya ubinadamu ndivyo ilivyokusudiwa Nyumba hii ya Mungu kuwa makao makuu ya umoja wa binadamu katika zama kamilifu za mwisho, na Baitullah ikachaguliwa kwa kutumwa huko Mtume Muhammad^{saw}, Mkuu wa manabii wote, ili Nabii wa kuleta umoja wa kibinadamu na Kibla cha umoja wa kibinadmau vikusanyike vyote viwili mahali pamoja.

Hadhrat Masihi Mau'udi^{as} ametia mwanga juu ya maudhui haya kinaganaga. Hivi sasa nawasomea marafiki zangu madondoo mawili tu ya Hudhur^{as} yahusianayo na madhumuni haya. Hudhur^{as} alilonga:

“Mwanzoni wanadamu walikuwa wachache. Walikuwa haba sana hata kwamba hawakustahili kuitwa kaumu. Hivyo, Kitabu kimoja tu kiliwatosha. Kisha baadaye wanadamu walipoenea duniani na watu wa kila sehemu ya ardhi wakawa kaumu peke yake, na kwa sababu ya kukaa kwenye masafa ya mbali sana, kaumu moja ikawa haina habari ya kaumu nyingine, basi katika zama kama hizo hekima na masilahi ya Mwenyezi Mungu yalitaka kwamba kwa kila kaumu iwe na mitume na vitabu mbalimbali. Basi ikawa hivyo. Kisha binadamu walipozidi kujaza dunia na njia za mawasiliano zilipofunguliwa na nyenzo za watu wa nchi mbalimbali kuonana zilipopatikana, na

ikajulikana kwamba sehemu fulani fulani watu wanaishi, na Mwenyezi Mungu Akanuia kuwakusanya wote kama taifa moja na kuwajumuisha baada ya wao kusambaratika, ndipo Mungu Akatuma Kitabu kimoja kwa ajili ya nchi zote na ndani yake Akaamuru kwamba katika zama zozote Kitabu hiki kikifikia nchi mbalimbali, wakazi wake watawajibika kukipokea na kukiamini. Na kitabu kile ndicho Kurani Tukufu iliyokuja kuzifungamanisha nchi zote. Kabla haijaja Kurani, Vitabu vyote viliitwa *mukhtassul kaumi*, yaani kila kimoja kilikuwa kwa ajili ya kaumu moja tu... Lakini, baada ya hivyo vyote ikaja Kurani Tukufu iliyo Kitabu kwa dunia nzima, sio kwa ajili ya kaumu moja tu bali ni kwa kaumu zote. Kadhalika, Kurani Tukufu ilikuja kwa ajili ya umati mmoja uliotaka kuwa asteaste kaumu moja tu. Basi, sasa katika zama hizi njia zimepatikana zinazoyaelekeza mataifa mbalimbali kuwa na Umoja. Mawasiliano, yaliyo msingi wa kuwa kaumu moja, yamekuwa rahisi sana hata kwamba masafa ya miaka yanaweza kuabiriwa ndani ya siku chache. Na njia za kupelekeana ujumbe zimebuniwa kiasi hiki kwamba habari isiyokuwa imeweza kufika toka nchi ya mbali katika mwaka mmoja, sasa yaweza kuwasili ndani ya muda mfupi mno. Mapinduzi makubwa yanaendelea kutokea duniani na mkondo wa mto wa utamaduni umeelekea kwenye

janibu fulani inayofahamisha kwamba utashi wa Mwenyezi Mungu ni huu huu kwamba Ayafanye mataifa yote yaliyotawanyika duniani kuwa kaumu moja na kuwaunganisha waliokuwa wameachana tangu maelfu ya miaka.”

(Chashmae Ma'rifat, uk. 66-69)

Kadhalika Hadhrat Masihi Mau'udi^{as} akasema sehemu nyingine:

“Kwa kuwa zama za Unabii wa Mtume^{saw} zarefuka hadi Kiama, naye ndiye Khatamun Nabiiyyina, hivyo Mungu hakutaka kwamba umoja wa Mataifa ukamilike ndani ya maisha ya Mtume^{saw}, kwani jambo hili lingedokeza kukoma kwa zama zake, yaani lingetia shaka kwamba zama zake zimeishia tu hapo, kwani jukumu lake la mwisho lilipata kutekelezeka katika zama hizo. Hivyo, Mwenyezi Mungu Akatuilisha ukamilifu wa jambo hili la mataifa yote kuwa kama taifa moja na kuwa juu ya dini moja, hadi sehemu ya mwisho ya zama za Mtume^{saw} zilizo zama za ukaribu wa Kiama, na kwa kulikamilisha Akamweka naibu kutoka ndani ya umati huu huu, aitwaye Masihi Mau'udi^{as} naye ndiye aitwaye Khatamul Khulafaa pia. Basi mwanzoni mwa zama za Muhammad^{saw} yupo Mtume^{saw} na mwisho wake yupo Masihi Mau'udi^{as} na iliwajibika kuwa silsila hii ya dunia isikatika mpaka huyo awe ameishazaliwa, kwani umoja wa

mataifa umeambatanishwa na zama za huyo naibu wa Unabii, na kwenye hii hii imeashiriwa ndani ya aya *هُوَ الَّذِي أَرْسَلَ رَسُولَهُ بِأْتِهْدَىٰ وَدِينِ الْحَقِّ لِيُظْهِرَهُ عَلَى الدِّينِ كُلِّهِ* (Sura As-Saff, 61:10) yaani, Mungu ndiye Yule Aliyemtuma mtume wake kwa mwongozo kamili na dini ya kweli ili kuishindisha juu ya kila aina ya dini, yaani, aipe ushindi juu ya dunia nzima. Na kwa kuwa ushindi ule juu ya dunia nzima haukudhihirika katika zama za uhai wa Mtume^{saw} – na haiyamkini bishara za Mungu zitanguke – kwa hiyo wataalamu wote waliotutangulia wameafikiana kwamba ushindi huu duniani kote utatokea katika wakati wa Masihi Mau'udi. Kwani, kwa ushindi juu ya dunia nzima hakuna budi mambo matatu yapatikane yasiyopatikana ndani ya zama zozote za hapo kabla:

(1) Mosi, njia rahisi ziwe zimefunguliwa kikamilifu kwa mataifa mbalimbali kuwasiliana na kuonana, na ziondoke shida za safari zisizovumilika.

(2) La pili lililo lazima kwa kufahamu kwamba dini fulani inazishinda dini nyigine zote kwa mazuri yake ni hili kwamba mataifa yote ya dunia yawe huru kujadiliana, na kila kaumu iweze kuweka mbele ya kaumu nyingine mambo yake mazuri, na pia kwa njia ya kuandika vitabu iweze kueleza mambo mema ya dini yao na dosari za dini nyingi. Na kwa mwereka wa kidini, kaumu zote zipate nafasi ya kujumuika ndani ya medani moja na

kushambuliana kwa kuhojiana kidini... na mwrereka huu usiwe baina ya kaumu moja mbili, bali uwe mwereka wa kaumu zote zile...

(3) La tatu lililo sharti kwa kuibainishia dunia kwamba dini fulani hususan inasaidiwa na Mungu kukabiliana na dini zote nyingine... ni hili kwamba kwa kukabiliana na dini zote za dunia, dini hii inazo ishara za kimbingu za kusaidiwa na Mungu namna ambavyo dini zingine hazinazo... na tokea kona hii ya dunia hadi kona ile ya mwisho kusipatikane dini yoyote iwezayo kushindana na dini hii ya kweli juu ya kwamba sehemu yoyote ya wakazi wa dunia isiwe pasipo kujua habari za mwito wa shindano hili.”

(Chashmae Ma'rifat, uk. 82-86)

Hadhrat Masihi Mau'udi^{as} anasema kwamba sasa hali zimezalika duniani kwamba mwereka ndani ya uwanja wa dini na ruhania baina ya dini zote za dunia umewezekana. Mataifa yote yakijumuisha wawakilishi wao mahali pamoja wanaweza kushindana na dini zingine. Na kwa kuwa Hadhrat Masihi Mau'udi^{as} aliziita dini za dunia nzima zije katika medani ya dini, basi mashindano haya yakaanza katika zama zake. Katika Mkutano wa Mwaka uliopita mimi nami niliitupia dunia miito kadha kwa ajili ya uamuzi. Na Mwenyezi Mungu Akinijaalia kwenda matembezini Ulaya nanuia kurudia miito yangu, kwa kutolewa uamuzi, katika nchi zile

zinazohusiana na ulimwengu wa Kikristo, na kuwatupia mwito wa kushindana na Islam katika mazingira ya amani na suluhu kwamba kama wanayafikiria madhehebu yao kuwa ya kweli wahakikishe ukweli wao. Nami natarajia kwamba kama wakijitokeza uwanjani kwa ajili ya uamuzi, Mwenyezi Mungu Atazalisha sababu za wao kukubali kushindwa kwao mbele ya dunia, inshallah.

Hivyo, kusudio la nane ni kuyaunganisha pamoja mataifa ya dunia na kuleta umoja baina yao. Na Mwenyezi Mungu Ameahidi kutimiza kusudio hili kupitia Nabii Mtukufu^{saw}. Na kama alivyonena Hadhrat Masihi Mau'udi^{as}, kupata shabaha hii kwahusiana na Jumuiya Ahmadiyya, kwa hiyo Jumuiya Ahmadiyya inayo majukumu mazito ambayo mimi na nyinyi nyote twapaswa kuyazingatia.

Basi, kusudio la nane limeelezwa katika neno **مَثَابَةٌ**. Na ni dhahiri kwamba kusudio hili halikupatikana kwa yeyote mwingine minghairi ya Mtume^{saw}, wala lisingeweza kupatikana, kwani nabii yeyote mwingine hakupewa sheria isipokuwa tu iliyokuwa kwa kaumu mahususi na kwa zama maalum. Ni Mtume^{saw} pekee aliyepewa na Mwenyezi Mungu sheria yenye kutimiza mahitaji yote ya binadamu na inayohusiana na kila kaumu ya dunia na zama zote mpaka Kiama. Na zile ahadi Mwenyezi Mungu Alizomuahidi Mtume Muhammd^{saw} zilitimia katika nyakati zake. Na ahadi hii ndiyo ambayo

kuhusiana nayo anasema Hadhrat Masihi Mau'udi^{as} kwamba wakati wake wa kutimia ni zama za Masihi Mau'udi^{as} na kuitimiza ni jukumu la Jumuiya Ahmadiyya. Mwenyezi Mungu Aijaalie Jumuiya uwezo wake.

Kusudio la tisa lililotajwa ndani ya aya hizi limeelezwa katika neno **أَمَّا** . Katika **مَثَابَةٌ** ilitajwa kuimarika kwa mahusiano ya matifa yote, juu ya misingi madhubuti. Na hakuna budi kwa uthabiti wa uhusiano wa udugu baina ya mataifa kwamba zizalishwe sababu na njia za utuvu wa moyo katika kuimarisha uraufu baina ya mataifa na mahusiano baina yao. Ahadi yenyewe ilikuwa ni kwamba ahadi ya **مَثَابَةٌ** pia itatimia na jambo lililo la lazima kwa ajili yake kwamba mazingira ya amani baina ya mataifa yazalishwe, ahadi hii pia itatimia. Na kupitia Mtume Muhammad^{saw} dunia itajaaliwa sheria ambamo mafundisho yatatolewa kuimarisha amani baina ya mataifa.

Na iliahidiwa kwamba dunia inaweza kupata amani ya kweli kwa kutekeleza mafundisho yale tu atakayoitolea dunia Khatamun Nabiiyyina atakayedhihiri ndani ya Makka. Kwani ndani ya sheria hii ya mwisho zitawekwa njia za kukuza barabara nguvu na vipawa vya asili, na akili ya binadamu itapata utulivu kwa yale maagizo na moyo wa mtu utatulia.

Mafundisho kuhusiana na amani duniani yaliyomo ndani ya Kurani Tukufu yameelezwa kwa mapana na marefu. Hivi sasa sinuii kuingia katika maelezo hayo.

Kuhusu jambo hili limefafanuliwa kwa utondoti ndani ya vitabu ‘Uahmadiyya, Yaani Islam ya kweli’ na ‘Nidhame Nau’ (Nidhamu Mpya) vya Hadhrat Muslih Mau‘udi^{ra}. Katika vitabu hivyo, Hadhrat Muslih Mau‘udi^{ra} ameeleza kwamba kwa kuimarisha amani duniani, mambo matano yameelezwa ndani ya Kurani Tukufu. Mpaka dunia itekeleze hayo, mfumo wowote wa Mataifa yote hautafaulu. Kwanza Shirikisho la Mataifa (1919-1946) lilishindwa, sasa – tuonavyo – Umoja wa Mataifa pia unaelekea kwenye kushindwa. Sababu yake kubwa, au yafaa kusema kwamba sababu yake ni moja tu, nayo ni kwamba watu hawa hawakuzingatia mafundisho yaliyotolewa na Kurani Tukufu kwa kuimarisha amani ya mataifa wala hawakuyashika. Kwa kuyapuzilia mbali wanaendelea kula mwande. Hadhrat Muslih Mau‘udi^{ra} ameeleza kinaganaga jambo hili ndani ya vitabu vyake kwamba badala ya kufanya mapatano ya aina moja baina ya mataifa yote, dunia inafanya mapatano ya aina mbili. Mapatano ya aina moja huhusiana na mataifa yote, na ya aina nyingine ni ambayo mataifa makubwa makubwa yanafanya baina yao. Na kwa kuwa miguu yao inakuwa katika boti mbili, hivyo wanashindwa. Katika Umoja wa Mataifa, mapatano yaliyofanywa, ndani mwake makubaliano mengine yakaunganishwa. Ilitakiwa kwamba mapatano haya yangekuwa halisi baina ya mataifa, lakini wakakubali kuingiza humo kura ya turufu, yaani Umoja wa Mataifa ukayapa baadhi ya

mataifa fadhila hii kwamba pasipo rai zao baadhi ya mambo hayataweza kuamuliwa. Hakika yenyewe ni kwamba jinsi ambavyo ile kanuni inayohusikana na watu wote, humo haiwezi kutofautishwa baina ya tajiri na maskini, mwenye nguvu na mnyonge, wala haipaswi kufanya hivyo ikiwa serikali ya kikanuni iwe inaimarishwa nchini, ndivyo hivyo ilivyolazimu kwamba katika mapatano baina ya mataifa, taifa lolote liwalo lisitangulizwe juu ya taifa jingine; kama litatangulizwa, kanuni hiyo ya kimataifa itashindwa kabisa.

Kurani Tukufu ilifundisha msilitanguliza tafia lolote juu ya taifa jingine. Watu hawa walifikiri kwamba tu wenye nguvu, twaweza kufanya tependavyo kwa nguvu yetu. Wakayapa baadhi ya mataifa haki za kura ya turufu, au yakajichukulia yenyewe baadhi ya mataifa haki hizo. Na hii hii ndiyo sababu kubwa ya kushindwa kwa Umoja wa Mataifa kwamba hawakufanya mapatano ya aina moja wakati wa kukubaliana, ambayo yangukuwa tu kwa mataifa yote, bali wakatia ndani mwake mapatano yaliyohusiana na baadhi tu ya mataifa, hayakuhusiana na mataifa yote ya dunia nzima.

Agizo la pili lililotoa Kurani Tukufu (kuhusu kuimarisha amani baina ya mataifa) lilikuwa ni hili kwamba pindi linapotokea tu tatizo, wakati uo huo anzeni kulitatua. Lakini leo desturi ya dunia, kwa kuangalia manufaa yao, imekuwa ni kwamba wanaendelea kulirefusha ili waweza kujifaidisha. Kwa njia hii amani haiwezi

kuimarika. Kisha agizo la tatu lilikuwa ni kwamba katika mapatano baina ya mataifa, chuki kwa nchi au taifa fulani, ni kitu chenye kudhuru bali ni cha kuangamiza. Lakini mapatano ya Mataifa yaliyokuja mbele ya dunia kwa sura ya Umoja wa Mataifa, juu ya hayo mapatano mataifa yaliyokuwa wanachama wake bali yakawa ni nguvu yake, yakaanza kufanya mapatano mbalimbali, na yakaanza kuyapendelea mataifa yaliyokuwa na uhusiano mzuri nayo.

Basi, Kurani Tukufu imesema kwamba amani baina ya mataifa yote yanaweza kuimarishwa hapo tu ambapo kusiwepo kupendelea taifa hili au lile, na taifa lolote lisilhami taifa lingine kwa njia isiyo halali.

Jambo la nne inalopinga Kurani, lakini dunia hii dhalimu inalipenda, ni hili kwamba ugomvi ukitokea, hapo baadhi ya mataifa badala ya kusuluhisha, yanapendekeza kuyaadhibu mataifa fulani kwa sababu ya chuki, na kila nafasi ikipatikana yanaanza kuyavunja na kugawanya. Wakagawanya Ujerumani katika sehemu mbili, ndivyo ilivyo ikawa hali ya Vietnam. Hayo yakafanyika ilhali Umoja wa Mataifa ulikuwepo pamoja na madai yake kwamba huu ni Shirika la kuimarisha amani.

Kurani Tukufu inanena kwamba mkiwa katika kivuli changu mtaweza kuimarisha amani duniani; mkiondoka kivuli changu, harara ya jua la kishetani itawasumbueni na haitawapa nafasi ya kupata utulivu.

Na fundisho la tano lililotolewa na Kurani Tukufu lilikuwa ni kwamba kama inakusudiwa kuimarisha amani baina ya mataifa, basi kila taifa litapaswa kutoa dhabihu. Lakini hivi sasa hali yenyewe ni kwamba baadhi ya mataifa yanatoa dhabihu na mengine yanakataa. Basi, mafundisho ya Kurani Tukufu ndiyo ambayo kwa kuyatekeleza amani baina ya mataifa yanaweza kuimarika.

Hadhrat Muslih Mau'udi^{ra} ndani ya kitabu 'Ahmadiyyat Yaani Hakiki Islam' ameandika natija hii ya mazungumzo yote ya kwamba:

“Kasoro hizo tano zikiondolewa mbali, ule Umoja wa Mataifa uliosemwa na Kurani Tukufu unapatikana, na kwa hakika Umoja kama huu waweza kunufaisha, sio ule Umoja unaokaa kutafuta ukarimu wa watu kwa kuimarika.”

(Ahmadiyyat Yaani Hakiki Islam, uk. 230)

Kama nilivyosema, Mwenyezi Mungu Aliahidi kwamba mataifa yote ya ulimwengu yatafungamanishwa pamoja, na Umoja wa mataifa yote yataimarishwa.

Kisha akasema kwamba kwa kuimarisha Umoja baina ya mataifa hakuna budi kudhaminiwa amani baina ya mataifa, na akadai kuwa Kurani Tukufu inatoa dhamana ya amani baina ya mataifa. Mkitekeleza amri za sheria hii, magomvi ya dunia nzima pia yakizuka yataamuliwa sawa na kanuni ya uadilifu na amani haitavurugika. Basi,

Kurani Tukufu imetoa mafundisho kwa utondoti yawezayo kuimarisha amani duniani. Kwa kuwa kupata shabaha ya *مَثَابَةٌ* ni jukumu la Jumuiya Ahmadiyya, kwa hiyo na jukumu hili pia ni la Jumuiya Ahmadiyya kwamba ieneze mafundisho haya sana mno duniani iliyoyatoa Kurani Tukufu kuimarisha amani duniani baina ya mataifa. Kwani, kama dunia ikibaki gizani, basi siku ya Kiama watu wanaweza kusema, ‘Ee Mungu, hatukuwa na elimu hii, na wale uliowatwisha mabegani mwao jukumu hili kwamba watuelimisha, hawakutufikishia elimu hii. Kwa hiyo sisi hatuna kosa, hivyo Uwaghadhibikie wale waliokosea. Mwenyezi Mungu Atulinde na ghaidhi Yake.

Kusudio la kumi la ujenzi wa Baitullah lilielezwa kuwa *الْمُحَمَّدُ وَالْمَقَامُ إِبْرَاهِيمَ مُصَلًّى*, ambamo mlielezwa kwamba kwa njia ya Makka, kwa njia ya Baitullah na kupitia Mtume mwenye shani kuu atakayeinuliwa ndani yake, mataifa ya ulimwengu yatapata utambuzi wa daraja ya ‘*Ubudiyat* – ibada ya kweli – na msingi wa ibada ya kweli itawekwa hapa inayobubujika kutoka katika chemchem ya udunifu, utiifu na unyenyekevu. Na kwa njia hii, katika mataifa mbalimbali vivuli vya Mtume Muhammad^{saw} vitazalika na katika kila maeneo ya ardhi makao makuu ya kueneza Islam yataimarika ambako adhama na jalali ya Mwenyezi Mungu itakiriwa na kudhihirishwa kwa maombi yenye unyenyekevu. Na kwa unyenyekevu huu na udunifu utakaofanywa kwa kujipatia furaha na radhi

ya Mungu tu, mataifa haya yatajaliwa baraka za kimbungu na yatastahili kusamehewa.

Basi, Alisema kwamba kwa njia ya Makka kupitia sheria hii itakayoteremka hapa umati utazalika utakaosali ukizingatia maana zake na sharti zake zote, ambao utasimama imara katika daraja ya ‘*ubudiyat* – ibada ya kweli.

Kwa hakika hili pia lahusiana na makusudio mawili ya kwanza, kwani ahadi ya nane ilikuwa kwamba mataifa yote yatafanywa umati mmoja wa Kiislamu – yatafanywa kuwa kaumu moja. Na hii haiwezekani mpaka iwe imeimarika amani ya ulimwengu. Hivyo, kwanza Aliahidi kisha Akaitimiza kwa sura ya sheria ya Kurani Tukufu kwamba mafundisho kamili ya kuimarisha amani baina ya mataifa ya ulimwengu alipewa binadamu. Na sasa katika kusudio la kumi Mwenyezi Mungu Anasema kuwa mafundisho haya hayatekelezeki mpaka umati wa Muhammad^{saw}, yaani umati ulioahidiwa, uwe wenye kushika udunifu na unyenyekevu. Kwa hiyo Akasema *اتَّخِذُوا مِنْ مَّقَامِ إِبْرَاهِيمَ مُصَلِّينَ*, bila hii hamwezi kuimarisha duniani amani kwa mataifa yote. Hivyo, hapa pameahidiwa kwamba kwa njia ya Nabii Mtukufu^{saw} utazalika umati utakaokaa imara kwenye daraja ya ibada ya kweli. Hadhrat Masihi Mau‘udi^{as} anasema watiifu kamili wa Kurani Tukufu waitambua daraja yao ya ‘*ubudiyat* na wanaoimarika juu yake ndio ambao:

“Kwa kushuhudia Ukuu wa Mwenyezi Mungu wanadumu dawamu katika hali ya udunifu na kutokuwepo na unyenyekevu, na wanafahamu uhakika wao wa asili ni dhila, umaskini, ufukara na kujaa dosari na makosa. Na sifa zote bora walizojaaliwa wanazona ni kama mwanga wa muda unaoangukia ukutu, ambao hauhusiani na ukuta hata kidogo na huwa wenye kutoweka kama libasi ya kuazima. Basi, hawa wanajua kila heri na uzuri vimo ndani ya Mungu tu na wanatambua chemchem ya mema yote ni Dhat Huyu Kamilifu. Na kwa kushuhudia kikamilifu Sifa za Mungu, nyoyo zao hujaa yakini ya kweli kwamba sisi si chochote, hata kwamba hujisahau uwepo wao na matakwa yao na utashi wao, na mto uliofurika wa adhama ya Mungu unazizingira nyoyo zao namna ambavyo ‘kutokuwepo’ kwao kunawaangukia kwa namna maelfu nao hutakatika na kuepukana fika na ushirikina uliofichamana.”

(Baraahine Ahmadiyya, J. 4, uk. 453, maelezo ya maelezo ya pembeni)

Sehemu nyingine alisema Hadhrat Masihi Mau‘udi^{as}:

“Sehemu za sala zinalo dhihirisho la adabu, unyenyekevu na udunifu ndani yake. Katika hali ya kusimama, mwenye kusali husimama kufunga mikono kifuani jinsi mtumwa asimamavyo kwa adabu mbele ya Bwana wake na mfalme. Katika *rukuu*‘ , mtu anainama

kwa kujinyenyekeza. Unyenyekevu mkuu ndio ndani ya sijida idhihirishayo unyenyekevu wa hali ya juu kabisa.

(Mir'aatul Hakaik, J. 3, Majmu'ah Fataawa Ahmadiyya, chapa ya 1325
Hijri, mkusanyaji: Muhammad Fadhl Changawii, uk. 15)

Mwenyezi Mungu Amesema hapa kwamba kwa fadhili Yetu Tutaendelea kuleta jumuiya moja miongoni mwa wafuasi wa Nabii Mtukufu^{saw} itakayoshikamana imara na unyenyekevu, udunifu, upole utii na adabu. Na kwa sababu ya udhalilifu huu na unyenyekevu Mwenyezi Mungu Ataandaa sababu za kuimarisha amani, zilizoelezwa katika neno **أَمْثًا** ambalo maelezo yake yametolewa kwa kirefu na Kurani Tukufu.

Yapasa kukumbuka kwamba ibada ya kweli inastawi kwa mchanganyiko wa (1) mapenzi, kujitolea na (2) udunifu na unyenyekevu. Lakini wakati fulani jiha ya mapenzi inatokeza zaidi na pengine jiha ya udunifu na unyenyekevu. Pindi uzuri na hisani ya Mwenyezi Mungu inapojidhihirisha kwa adhama kubwa, moyo wa mtu hujaa mapenzi ya Mola wake na kama ashiki mkubwa anasema labeka kwa kila mwito wake na humzunguka pembezoni mwake, na akitengana na uwepo wake anapotea ndani mwake na anajiwa na mauti juu ya uwepo wake na hujaaliwa uzima mpya kutoka kwa Mola wake, lakini dunia haimtambui, naye pia haijali kitu.

Lakini, pindi linapomdhihirikia onyesho la utukufu na jalali ya Mwenyezi Mungu, hapo moyo wake hujaa kicho na tarajio. Baada ya utukufu na jalali ya Mungu,

haubaki ukuu wake na heshima yake naye hujivalia libasi ya unyenyekevu na huufanya udhalilifu kuwa tabia yake na kwa vumbi la unyenyekevu anaonekana mwenye mavumbi. Yeye huchagua njia za unyenyekevu na huinama mbele ya Mola wake kwa udhalilifu na mwenye hofu moyoni akitetemeka na kukicha na hukiri adhama na jalali ya Mola wake. Kila chembe ya mwili wake na kila jiha ya roho yake hutikisika kwa kumcha Mola wake. Na onyesho hili la utukufu na jalali lamwimarisha katika yakini ya kweli hata kwamba mbele ya utukufu Wake mahuluku wote huwa maiti na si chochote; hautarajiwi kutoka kwao wema wowote, wala wenyewe hawanao uwezo wake. Kama ni kurajua, yaweza tu kwa Mungu Mwenye jalali na heshima. Hapo pamwe na hofu, matarajio pia huzalika ndani ya kifua chake safi. Huambatisha matarajio yake yote na Mola wake na humtegemea Yeye pekee, na hugonga mlango Wake tu kwa kupata mahitaji yake. Moyo wake huwa unjaa yakini kwamba chochote kitakachopatikana, kitapatikana kutoka kwenye Mlango Wake, iwe ni gidamu ya kiatu au heshima za ulimwengu mzima.

Yule mtu ambaye linamdhihirikia onyesho hili la adhama na jalali hahitaji kukusanya kashfi na ruya zake na kuzipamba na matukio ya kupokelewa dua zake na kwenda nyumba hadi nyumba kuomba apewe heshima ya kidunia na taadhima na staha na asifiwe, na awe anajitafutia heshima machoni mwa dunia. Atajipatiaje kitu toka kwa mfu? Na maiti atampatiaje kitu? Yule

Makusudio 23 Adhimu ya Ujenzi wa Baitullah

ambaye hofu ya adhama na jalali Yake na Ambaye matarajio ya rehema Yake isiyo na mipaka yamemfanya kuwa darweshi wa kujikalia kizingiti fulani, yeye mtu huyo anapitisha siku za maisha yake akishinda kweye kizingiti hicho baina ya matarajio na kicho, ndipo Mola wake Huwa Anamridhia na kumkalisha mapajani Mwake, naye hupata pepo za dunia na Akhera. Mungu Amewaridhia waja hawa nao wamemridhia Yeye.

Bishara ya kupatikana umati mmoja kupitia Mtume Muhammad^{saw} alipatiwa Hadhrat Ibrahim^{as}. Naapa kwamba Yeye Akatimiza ahadi Yake. Hakuna Mwabudiwa ila Mwenyezi Mungu na Muhammad^{saw} ni Mtume wake.

(Gazeti la Al-Fadhil, Rabwah, 28 Mei 1967)

⑦

BAITULLAH
Makao Makuu ya Kupata Utakaso
wa Kiroho na Kimwili
na Uenezeji Wake

Hotuba ya Ijumaa, 26 Mei 1967,
Masjid Mubarak, Rabwah, Pakistan.

“Kaaba au Baitullah ni nukta ya katikati, nasi tumefundishwa kwamba mtalazimika kuanzisha matawi yake pia. Yaani kwa kuiiga kwa kupata makusudio hayo, kwa kuzalisha utakaso na usafi wa aina hiyo mtatakiwa kufungua Makao Makuu kama haya katika maeneo mbalimbali yatatakayokuwa ni vivuli vya Baitullah, na shabaha yake ya kuviimarisha itakuwa ni shabaha ile ile ya kuimarisha Baitullah.”

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ¹⁴

تَحْمَدُهُ وَنُصَلِّي عَلَى رَسُولِهِ الْكَرِيمِ¹⁵

Baada ya kutamka Shahada mbili na A‘udhu na usomaji wa Sura Al-Faatiha, alisema:

Katika hotuba zilizopita nilitaja makusudio kumi ya kujenga Baitullah, na kueleza maoni yangu juu ya hayo. Aya nilizoendelea kusoma katika hotuba hizo, kuhusu hizo niliwaambia kwamba ndani yake makusudio 23 yametajwa. Nimeishaeleza kuhusiana na makusudio kumi hapo kabla.

Kusudio la kumi na moja au shabaha ya kumi na moja ya kujenga Baitullah ilielezwa ndani ya neno طَهَّرًا , yaani mfanye mpango wa kuitakasa, msimamie utakaso wake na kuiweka safi. Mwenyezi Mungu Anataka kuifanya kuwa Makao Makuu ya usafi wa kudhahiri na utakaso wa kibatini. Shabaha hii pia ikatimia kwa kutumwa kwa Mtume Muhammad^{saw}. Mwenyezi Mungu Ananena ndani ya Sura Al-Baqara 2:151-152 kwamba popote mkiwepo, jambo lolote mkilifanya sawa na agizo la sheria ya Kiislamu, mzingatie kuwa mmeumbwa kwa makusudio na shabaha mahususi, na mmetwishwa jukumu la kutekeleza makusudio haya na kuimarisha sheria ya Kiislamu duniani kote na baina ya mataifa yote ya ulimwengu na kuibakiza hai. Mwenyezi Mungu Anasema kuwa Mimi Nawaelekezeni kwenye jambo hili

¹⁴ Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwingi wa Ukarimu.

¹⁵ Twahimidia Yeye na kumsalia Mtume Wake mhashamu.

kwamba saa zote muyaweke mbele ya macho yenu makusudio yahusianayo na Baitullah. Hii ni kwa sababu Mimi Nataka kuwatimizieni neema Yangu, **وَلَا تَعْبُرُوا عَنِّي عَلَيْكُمْ** . Ili kuwatimizieni neema, Nimeweka makusudio haya mbele yenu. Kama mkijibidiisha kutimiza makusudio haya sawa na Tulivyoagiza na kuzitekeleza amri Zetu kwa nia halisi, hapo neema Zetu mtakazopata zitakuwa kwa njia na namna ambayo kuzihusu hizo itaweza kusemwa kuwa mmetimiziwa neema. Na baada ya **لَا تَعْبُرُوا عَنِّي عَلَيْكُمْ** , Mwenyezi Mungu Amesema (ndani ya aya 152) kwamba Mtume mmoja mmepelekewa anayewafundisheni kujitakasa.

Kwa kuwa kitabia lilikuwa linazuka swali kwamba Ee Mungu tumeishajua makusudio, lakini bado njia za sisi kujibidiisha hatujabainishiwa, na kama zingebainishwa, tungsahilishiwa, kwa hiyo ndani ya aya nyingine (aya 152) Ametuambia kwamba njia awaambiaye mpendwa Wangu, Mtume wa Mungu, Muhammad^{saw} ndiyo njia iongozayo kwenye utakaso, na ambayo kwa kuikanyaga mwaweza kupata makusudio yote ya kujenga Baitullah. Akasema: **يَتْلُوا عَلَيْكُمْ آيَاتِنَا وَيُرَكِّبُكُمْ**, yaani kupitia Mtume^{saw} huyu, Tumewapatieni njia za utakaso wenu, kwani yeye anawasomeeni aya na kuwafundisheni Kitabu na kueleza hekima zake.

Hivyo, ile shabaha iliyokuwa imeelezwa ndani ya neno **كَلِمًا** na ambayo imeashiriwa kwayo ndani ya maneno haya, mwenye kuitimiza ndiye Nabii Mtukufu^{saw}. Kurani Tukufu yenyewe imedai kwamba yeye^{saw} ndiye atimizaye

shabaha hii. Kwani, sehemu hii Msikiti Mtakatifu, kuweka makusudio mbele ya macho, kutimiza neema na kuzitakasa nafsi na njia zake zote, mambo yote haya yamejumuishwa ndani ya aya hizi mbili.

Ndani ya aya hizi za Sura Al-Baqara utakaso wa kawaida umetajwa, lakini mkazo zaidi ni juu ya utakaso wa ruhania na wa kidini. Mwenyezi Mungu Anasema ndani ya Sura Al-Maa'ida 5:7 kwamba kama mwenye janaba, basi ogeni. Ndani yake imefundishwa kwamba katika Islam hakuna budi kuitakasa miili na kuisafisha pia. Kwa hiyo, Nabii Mtukufu^{saw} ametoa mafundisho kuangalia usafi wa mwili, usafi wa mavazi, usafi wa nyumba, usafi wa mazingira, usafi wa misikiti na kuitakasa, usafi wa ulimi, usafi wa masikio na usafi wa macho. Sitaki kushughulikia wakati huu maelezo ya mafundisho haya, wala haiwezekani kuingia katika maelezo haya. Kwa vyovyote twafikia natija hii (ambayo hawezi kuikana mtu yeyote) kwamba kiasi ulichokazaniwa ndani ya sheria ya Kurani usafi na utakaso wa dhahiri na batini, katika dini yoyote ya hapo kabla hayakusisitizwa mambo haya, hata sehemu yake ya mia, pengine hata sehemu ya elfu. Basi, kusudio lililokuwa limeelezwa katika طهرا , kwa kulitimiza alitumwa Nabii Mtukufu^{saw}, naye akalifanya kusudio hili liwezekane kutimizwa na umati wa Kiislamu. Kwani, yeye akatuongoza kwenye kila njia kubwa ya kuleta usafi na kila mafundisho yaliyohusiana na utakaso na usafi akatubainishia vizuri fika, na kuturahisishia njia za

kutekeleza maagizo. Hakuna nabii yeyote wa hapo kabla aliyewahi kufanya kazi kubwa kama hii katika nyanja hizi. Basi, kusudio lenyewe ni utakaso na usafi, na Mtume Muhammad^{saw} akawa njia ya kuupata. Na kulitekeleza kusudio hili ni jukumu la umati wa Kiislamu, na miongoni mwa Waislamu, katika zama hizi, ni jukumu la wafuasi wa Jumuiya hii ambao walihuishwa upya kupitia Hadhrat Masih Mau'udi^{as} kwa ajili ya Mungu na Mtume^{saw} wake. Ndani ya aya hii pia Mwenyezi Mungu Anasema kwamba Hatuwatakieni taabu na ugumu; shabaha Yetu ni kuwatakaseni na kuwatimizieni hisani Yetu. Kama pamoja na mafundisho ya utakaso wa kiroho yasingetolewa mafunzo ya usafi na utakaso wa kimwili, basi neema na hisani ya Mwenyezi Mungu isingekamilika. Lakini **وَلِيُتَمِّمَ بِعِنتِهِ عَلَيْكُمْ** , Yeye Akapenda kutimiza hisani yake na kukamilisha neema Yake, basi Akatoa mafundiho haya ili Asibakize ndani mwenu uchafu wowote na kuwatakaseni na kuwasafisheni kikamilifu kitimilifu.

Kadhalika Kurani Tukufu ikasema kuhusiana na maji kwamba haya yana manufaa mengi, mojawapo ni kuwa mnajisafisha nayo na kufua nguo, kukosha vyombo, kunadhifisha mitaa yenu, kusafisha nyumba zenu na kuoga. Maelfu ya utakaso mnapata kwa maji, **مَاءٌ لِيُطَهِّرَكُمْ بِهِ** (Sura Al-Anfaal 8:122). Hivyo, Kurani Tukufu imejaa mafundisho ya usafi na utakaso wa kidhahiri na kibatini, na ni Nabii Mtukufu^{saw} tu ambaye kupitia yeye kusudio hili la kujenga Baitullah linapatikana.

Kusudio la kumi na mbili la ujenzi wa Nyumba ya Mungu lilielezwa ndani ya لِبَاطِنِينَ . Ndani ya neno hili iliashiriwa kwamba wawakilishi wa mataifa ya ulimwengu watajikusanya hapa mara kwa mara ili wapate mafunzo ya utakaso na usafi, na kisha baada ya kurejea kwenye maeneo yao wazagaze mafundisho haya. Shabaha hii pia ilitimia kikweli kwa njia ya Mtume Muhammad^{saw}. Kwa lengo hili, Kurani Tukufu iliamuru katika Sura At-Tauba 9:122 kwamba:

وَمَا كَانَ الْمُؤْمِنُونَ لِيَنفِرُوا كَآفَّةً ؕ فَلَوْلَا فَزَعٌ مِّنَ كُلِّ فِرْقَةٍ وَنُهُم طَآئِفَةٌ لِّيَتَتَقَّوْا فِي الدِّينِ وَلِيُنذِرُوا قَوْمَهُمْ
إِذَا رَجَعُوا إِلَيْهِمْ لَعَلَّهُمْ يَحْذَرُونَ ﴿١٢٢﴾

Yaani, haiwezekani kwa waaminio kwamba wote wajumuike katika makao makuu ya Islam, kwani Islam inahusiana na mataifa yote ya ulimwengu. Mataifa ya ulimwengu hayawezi kujumuika wakati wowote katika makao makuu ya Islam, lakini hakuna budi kwamba uhusiano madhubuti wa mataifa ya ulimwengu uimarike pia na Makao Makuu. Kwa hiyo, Mwenyezi Mungu Anasema kuwa Twawafunzeni kwamba kwa sababu haiyumkiniki kuwa wote wakusanyike hapa, basi kwa nini halitoki kundi katika kila taifa miongoni mwao kujielimisha vema dini na baada ya kurudi wangeokoa taifa lao katika ukosefu wa dini na kuwaokoa wasipotee njia, kwa kuwaonya na kuwaogofya.

Hivyo, Kurani Tukufu imeuamrisha umati wa Kiislamu ambao unayo mataifa yote ndani mwake na umeenea duniani kote kwamba kundi moja la wajumbe wa kila

taifa na kila nchi wanapaswa kudumu kufika Makao Makuu ili kujifunza dini na kujua mahitaji ya wakati na kupata elimu kwamba katika zama hizi Islam inahitaji dhabihu za aina gani na wapate kuelewa kuwa Imam wa zama anawaita kwenye mambo yepi na mipango ipi na ili wazitambue hekima zake, na wakirejea kwao wawahabarishe ndugu zao kwamba wakati huu Islam inashambuliwa kutoka upande fulani fulani, nanyi mjitayarishe kujibu. Mbinu fulani za udanganyifu dhidi ya Islam zinatumiwa, kwa hiyo kwa kuihifadhi Islam na kuibakiza hai na kuistawisha na kuiimarisha, mpango huu unawekwa mbele ya Jumuiya. Basi, kwa kutoa mifano ya dhabihu hizi na kwa kujitolea mjiweke tayari kiakili na mjaribu kupitana kwa kitendo nyinyi kwa nyinyi. Sawa na amri hii ya Mwenyezi Mungu, wajumbe wa makabila walikuwa wanaendelea kujumuika Madina kwa Mtume^{saw} katika zama za Nabii Mtukufu^{saw}. Wakajifunza elimu ya dini na elimu ya Kurani, na kukumbuka kwa ghaibu baadhi ya sehemu za Kurani Tukufu, na kujipatia تَفَقَّهُ فِي الدِّينِ – ujuzi wa undani wa dini – kisha wakarudi kwa kaumu yao na kuandaa njia za kuhuisha dini. Waliokuwa wanafika Madina, walikuwa wanatoa dhabihu ya nyakati zao kwa kujifunza dini pia na kuwafundisha wengine pia, na wale waliokuwa wanajifunza kwao pia wakajitolea nyakati zao. Kama wasingalifanya hivyo, japo wangepaidika wenyewe kufika Madina, lakini wengine wasingalinufaika kwao. Lakini shabaha ya kweli ya

mkakati huu ilikuwa ni hii tu kwamba watu toka nje waje katika Makao Makuu, wakajifunze dini na kujielimisha kuhusu mahitaji ya Islam, kisha warudi kuwaambia mambo haya ndugu zao wengine.

Hivyo basi, kusudio la tawafu – طَوَافٍ – halipatikani mpaka liwepo kundi hili na watu wazungukao na watoao dhabihu ya nyakati zao. Ndani yake imefahamishwa kwamba Islam imeishatoa mafundisho ya utakaso na usafi, na Mwenyezi Mungu Ameishaumba umati wa watu wanojumuika katika Makao Makuu kwa ajili ya Mungu na Mtume^{saw} wake wakijitolea dhabihu ya nyakati zao, na baada ya kurudi wanawafundisha ndugu zao elimu ya Kurani kwa ajili ya ridhaa ya Mungu na Mtume^{saw} wake. Wanawapa elimu ya dini na kuwaambia tadbiri zile zinazotekelezwa kuihifadhi Islam au kuieneza na kuzalisha nyoyoni mwao ubashasha kwa kutoa dhabihu katika njia ya Mungu.

Amri hii yakaelewa sana mataifa na makabila. Imesimuliwa na Ibnī Abbas^{ra} ndani ya Tafsiri Ibnī Kathīir, J. 5, uk. 88, Sura At-Tauba, chini ya aya وَمَا كَانَ الْمُؤْمِنُونَ ya kwamba:

كَانَ يَنْطَلِقُ مِنْ كُلِّ مَسْجِدٍ مِنَ الْعَرَبِ عِصَابَةً فَأَيُّ تَوَنُّنٍ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فَيَسْأَلُونَهُ حَتَّى يُرِيدُونَ مِنْ أَمْرِ دِينِهِمْ وَيَتَفَقَّهُونَ فِي دِينِهِمْ

(Tafsir Ibnī Kathīir, J. 5, uk. 88, Sura At-Tauba, Aya: wamaa kanal-Mu'minuna)

Yaani, kutoka miongoni mwa kila kabila la Waarabu, jama'at moja ilikuwa inahudhuria mbele ya Nabii Mtukufu^{saw}, nao walikuwa wanamuuliza yale mambo wasiyokuwa wakiyajua. Walikuwa wanapata busara na kuelewa hekima za masiala, kuimarika juu ya dini na kupata ujuzi wa undani wa dini, kisha baada ya kurudi wakawafunza wengine mambo haya. Katika historia yetu kwa marefu na mapana zimeelezwa habari za makundi ya wajumbe waliokuwa wakimfikia Nabii Mtukufu^{saw} huko Madina, wakakaa huko. Baada ya kundi moja likaja la pili, kisha la tatu, tena kundi lingine. Kulikuwa na mlolongo na ndani ya mlolongo huu kulikuwa na njia za dini kubaki. Mathalani, historia inatuambia kuwa safari moja wajumbe kumi na wanne wakaja toka Bahareni. Kadhalika toka Hadhramaut (Yemeni) wajumbe themanini waliwasili na kundi moja la wajumbe 70-80 wa Banu Tamim lilikuja kujifunza dini. Makundi haya ya wajumbe **بَقُوا بِالْمَدِينَةِ مُدَّةً يَتَعَلَّمُونَ الْقُرْآنَ** , **وَالَّذِينَ ثُمَّ خَرَجُوا إِلَى قَوْمِهِمْ** wakakaa Madina kwa muda fulani wakijifunza Kurani na dini, kisha wakarejea kwa kaumu zao, na kuwafundisha dini.

Nimetoa mifano hii michache ili matawi ya Jumuiya yetu yatambue kwamba pengine baadhi ya matawi hayaleti mwakilshi hata mmoja kwa ajili ya mipango inayoanzishwa kuwatolea mafunzo ya dini. Kwa njia hii hatuwezi kufaulu; idadi ya kutosha ya watu watalazimika kufika hapa, ndipo tutaweza kuihudumia dini ya Kiislamu ipasavyo.

Kwa vyovyote, maelezo yake nitawaambia nikiisha maliza kuyaeleza makusudio hayo kama nilivyoahidi, na nitaanza kuyaeleza majukumu yetu kuhusiana na ahadi hizo, kwani majukumu yote haya ndiyo waliyotwishwa Waislamu, na hususan wakati huu sisi Waahmadiyya tumetwishwa.

Kusudio la kumi na tatu lilielezwa ndani ya **وَالْعَاكِفِينَ**, na ilisemwa kwamba kwa njia hii itaumbwa kaumu itakayojitolea wakfu maisha yake katika njia ya Mwenyezi Mungu, na katika kundi hili la wenye kujitoa wakfu watakuwepo wajumbe wa mataifa na nchi mbalimbali. Shabaha hii pia ikatimia kwa njia ya Mtume^{saw} tu. Kabla yake jambo hili lilikuwa haliwezekani, kwani wajumbe wa mataifa mbalimbali walikuwa hawawezi kufika hapo. Hawakujua Makka wala hawakuwa na upendo wake nyoyoni mwao. Nimewaambia kuwa Mtume Mtukufu^{saw} ametimiza makusudio haya. Mwenyezi Mungu Anasema **وَإِنَّكُمْ عَقْفُونَ فِي السَّبِيلِ** (Sura Al-Baqara, 2:188). Ndani mwake pia mmeashiriwa kwamba Twarjia kwamba mtakaa misikitini kwa ibada ya itikafu; kwa kutengana na mahusiano yote ya kidunia mpitisha kwa siku chache masaa 24 ya maisha yenu kwa ajili ya Mungu pekee, ili roho ya wakfu ipate kuhuishwa. Na kwa kuwa Mtume Mtukufu^{saw} amesema kwamba ardhi nzima imefanywa kwangu kuwa msikiti, hivyo **وَإِنَّكُمْ عَقْفُونَ فِي السَّبِيلِ** yamaanisha kwamba kwa ajili Yangu mtatakiwa kupitisha wakati fulani kama mwenye kujitoa wakfu. Kwani, kama

nilivyoashiria hapo kabla pia, Kaaba au Baitullah ni nukta ya katikati, nasi tumefundishwa kwamba mtalazimika kuwa na vivuli vyake pia. Yaani, kwa kuiiga, kwa kupata makusudio hayo, kwa kuzalisha utakaso na usafi wa aina hiyo, mtatakiwa kufungua Makao Makuu kama haya katika maeneo mbalimbali yatakayokuwa ni vivuli vya Baitullah, na shabaha yao ya kuimarisha itakuwa ni shabaha ile ile ya kuimarisha Baitullah. Mwenyezi Mungu Ametuambia hapa kwamba **وَأَنْتُمْ عَكْفُونَ** , **فِي الْمَسْجِدِ** , popote pale umati wa Kiislamu utakapoimarisha ‘kivuli’ cha Baitullah, mtatakiwa kukaa hapo kama mwenye kujitoa wakfu, la sivyo, kusudio hili halitatimia. Kuhusiana na jambo hili sitaki kujiingiza ndani ya maelezo yake zaidi. Lakini nikapata wazo kwamba ikiwa shabaha moja ya ujenzi wa Kaaba ni hii pia kwamba *wakifiin* wa mataifa, yaani waliojitolea wakfu, wa kila sehemu na makabila wajumuike katika Makao Makuu au katika ‘kivuli’ chake, na wakae huko, basi wakfu na hijra zalandana sana. Historia yatuambia kuwa si tu toka Makka, bali toka sehemu nyinginezo pia baadhi ya wajumbe wa makabila wakaziacha sehemu zao na kuhamia Madina na kisha wakakaa huko kwa kudumu. Hijra yao toka kaumu au nchi yao haikuwa kama hijra toka Makka, bali ilikuwa ya aina ile inayokuwa hijra ya mtu aliyejitoa wakfu, ambaye anakuja kwa ajili ya Mungu katika Makao Makuu kwa kuachana na jamaa zake, makazi yake na rasilimali yake, kisha anahudumia dini sehemu tofauti za dunia sawa na maagizo ya Makao

Makuu. Mathalan, huko Yemeni kulikuwa na kabila la Ash'ariyyiin, sahaba mmoja mashuhuri, mtawa sana wa kabila hili Hadhrat Abu Musa Ash'arii, akahamia Madina pamoja na wenzake themanini. Vivyo hivyo historia inataja makabila mengi yaliyohamia Madina kwa shabaha ya kunufaika na kukaa pamoja na Nabii Mtukufu^{saw}, kati yao mmojawapo alikuwa Hadhrat Abu Hurairah^{ra} pia.

Kusudio la kumi na nne lilielezwa ndani ya وَالرُّجْعُ السُّجُودِ na ilisemwa kwamba kwa njia hii mataifa ya ulimwengu yatapata utambuzi kikamilifu wa Dhati ya Mungu na Sifa Zake. Matokeo yake yatakuwa ni kwamba yatadhihirisha mifano ya kujitoa mhanga, ambayo dini yoyote duniani haitaweza kutoa mfano wake, na ambayo kwa kuiona, dunia itapigwa na bumbuazi.

Kusudio hili nalo likatimia kwa njia ya Nabii Mtukufu^{saw} kwa nguvu yake takatifu. Si tu katika zama zake, bali baadaye pia ndani ya kila karne waliendelea kuzaliwa waliotimiza kusudio hili. Katika utondoti wake sipendi kuingia wakati huu. Mwenyezi Mungu Akinijaalia nitatoa maelezo yake kwa marefu na mapana nitakapowaambia marafiki zangu majukumu yao, inshallah.

Kusudio la kumi na tano lilielezwa ndani ya بَلَدًا أَمِيًّا , na iliahidiwa kuwa Mwenyezi Mungu Ataikinga Nyumba hii na mashambulio ya kidhuluma ya dunia, na kila mbinu ya kuifutilia mbali itashindwa, bali washambulizi wataangamia na kutilifika. Ndani mwake mliashiriwa

kwamba Tumeihifadhi Makka kwa shabaha mahususi. Na Akasema, Makka italindwa ili kuibainishia dunia kwamba yule Nabii Tumtakaye kumtuma sehemu hii atakuwa chini ya ulinzi wetu, na ili dunia ipate kuelewa kwamba sheria Tunayotaka kuite remsha hapa nayo pia Tutaihifadhi Sisi.

Hivyo, Nabii Mtukufu^{saw} kuwa katika ulinzi wa Mungu na sheria iliyomteremkia Nabii huyu maasumu kuwa ndani ya ulinzi wa Mwenyezi Mungu kikamilifu, yote haya mawili yaliahidiwa ndani ya ahadi ya kuilinda Kaaba. Basi, Kurani Tukufu ilidai kwamba ile ahadi iliyofanywa, Mtume Muhammad^{saw} ndiye aliyeitimiza na ikasema وَاللَّهُ يُعِصُّكَ مِنَ النَّاسِ – na Mungu Atakulinda na watu. Aya hii inaanzia hivi يَا أَيُّهَا الرَّسُولُ بَلِّغْ مَا أُنزِلَ إِلَيْكَ مِنْ رَبِّكَ (Sura Al-Maa'ida 5:68), yaani mwongozo na mafundisho uliyoteremshiwa uyafikishe kwa watu bila hofu, kwa ushujaa pasipo kujali hatari, na kufikisha maji haya ya uzima hadi pembe za dunia. Lakini Twakuarifu kwamba dunia haitairidhia Tabligh hii wala haitaifurahia, bali itakula njama nyingi kukuua, kukuangamiza, kukutilifikisha na kuifutilia mbali Jumuiya yako, lakini usizijali njama zao kwa sababu Tumekuahidi kwamba u ndani ya ulinzi Wetu. Dunia ifanye ipendavyo, nguvu zote za dunia zikitaka kujumuika na zijumuike, haziwezi kukuhilikisha. Kwa hiyo, udumu kushughulikia kufanya Tabligh pasipo kuchelea bila kujali hatari. Kwani Sisi ndio Tutakulinda, na malaika zetu watashuka kutoka mbinguni na kukukinga na hilaki na kukuhifadhi.

Mwanzoni mwa aya hii imesisitizwa kufanya Tabligh, kisha mkatulizwa kwamba mtakapoeneza ujumbe, fitina zitazushwa dhidi yenu lakini hamtaangamia. Watu wa dunia wanawaudhi sana waja wa Mungu, lakini m ndani ya ulinzi wa Mungu, na Mungu Ameahidi ya kuwa nguvu yoyote iwayo haiwezi kuwahilikisha, haiwezi kuwatilifikisha. Kama umati wa Muhammad^{saw} usingepewa ahadi hii, usingeweza kutimiza faradhi ya *يَا أَيُّهَا الرَّسُولُ بَلِّغْ مَا أُنزِلَ إِلَيْكَ مِنْ رَبِّكَ*, kwani hapo wangukuwa na wasiwasi kwamba adui akituangamiza, njia ya kufanya Tabligh itakatika fika. Mwenyezi Mungu Akanena kwamba baadhi yenu wanaweza kuuawa na kuhilikishwa na baadhi yenu wanaweza kufungwa gerezani, mwaweza kuzuiwa kufanya Tabligh, baadhi yenu wanaweza kukatazwa kusema kuhusu dini na baadhi yenu wanaweza kuzuiwa kuandika kuhusu dini, lakini kwa ujumla umati wa Kiislamu upo chini ya ulinzi wa Mwenyezi Mungu, na hauwezi kusibiwa na msiba mkubwa ambao uufutilie mbali umati huu juu ya uso wa ardhi.

Mkitafakari, kulikuwa na wakati fulani ambapo kama Nabii Mtukufu^{saw} asingekuwa katika ulinzi wa Mungu, afkani mmoja angeweza kumuua yeye^{saw}; yaani alihitajika mtu mmoja pekee kwa kuifuta Islam. Kisha ukawadia wakati ambapo kama watu elfu tatu wangukuwa tayari kufa, kidhahiri wangeifuta Islam. Lakini Mungu Akanena kwamba Sitampa adui wa Islam kiasi cha watu au kiasi cha nguvu cha kuiumiza Islam vibaya sana.

Wakaja katika medani ya Badri kwa nguvu mara tatu, baadhi ya masahaba wakauawa pia lakini hawakuachwa wafutiliwe mbali. Kisha, maadamu Islam haikuimarika katika Makka na katika Bara Arabu, Kaisari na Kisra hawakuidhinishwa na Mungu kujaribu kuiangamiza Islam. Lakini baada ya Islam kuwa madhubuti Uarabuni, Kaisari na Kisra wakaruhusiwa kutumia nguvu wawezavyo dhidi ya Islam, nao wakafanya kila wawezalo dhidi ya Islam, lakini kila mara wakala mwande. Na muujiza mkubwa zaidi tunaona ni huu kwamba wakati wowote wapinzani hawakupewa nguvu kiasi cha kufutilia mblai umati wa Uislamu. Sehemu moja ya waaminio wakatoa dhabihu yao, na kutoka kwa wengine Akataka wajitolee dhabihu, nao wakavumilia katika njia yake masaibu makubwa, lakini umati wa Kiislamu kwa jumla ulikuwa katika ulinzi wa Mungu. Sasa, mathalani, katika zama zetu nguvu za kidajali zimepata uwezo kiasi hiki kwamba kama wangetaka au kama wakitaka, wanaweza kuwaua Waislamu wote wa dunia nzima, lakini Mwenyezi Mungu Aliyekuwa Ameonyesha miujiza ya namna fulani, sasa Ameonyesha muujiza huu kwamba Akaweka malaika kuwa walinzi juu ya akili za binadamu na kuwafahamisha kuwa zama hizi si za kutumia upanga kuifuta dini; pambano lapaswa kwa kuhojiana. Wanayo nguvu, lakini Mwenyezi Mungu Amewekeza upande mwingine wasijaribu kuwaangamiza kwa nguvu. Hivyo, leo kama dajali akitaka kutumia nguvu yake kumuua

kila Mwislamu, anao uwezo wake, lakini Mungu Akasema kuwa Nimewapeni nguvu lakini Sikuwapei ruhusa ya kuitumia dhidi ya Islam na Waislamu.

Jinsi Nabii Mtukufu^{saw} alivyoahidiwa ulinzi mahususi ndivyo hivyo umati wa Kiislamu ulivyotolewa ahadi ya ulindaji mahususi kwa sababu hiyo na kwa shabaha iyo hiyo. Na kwa kweli Mwenyezi Mungu Hakuwaruhusu wapinzani kufutilia mbali umati wa Kiislamu duniani. Angalieni hali zenu tu. Kulikuwa na wakati ambapo mtu mmoja alitosha kumuua Hadhrat Masihi Mau'udi^{as}. Hakuna Jumuiya yoyote iliyokuwa pamoja naye. Safari moja watu kumi na wawili tu walikuwa pamoja naye. Alipokuwa safarini Delhi, wapinzani wakivunja ukuta wa nje au mlango wakapata kuingia uani. Walipokuwa wanavunja milango ya ndani, haijulikani ilikuwaje kwamba wote wakakimbia na kuondoka. Kwa nini wakakimbia? Jawabu lake limo ndani ya aya hii kwamba yule mtu aliyeko katika ulinzi wa Mwenyezi Mungu, au kaumu ile iliyo chini ya ulinzi wa Mwenyezi Mungu, hila yoyote ya dunia, njama yoyote na nguvu yoyote iwayo ya dunia haiwezi kumwangamiza. Ahadi hii inaimarisha nyoyo na kuhamasisha kujitolea dhabihu.

Pili, ndani mwake mliashiriwa kwamba ile sheria atakayopewa Nabii huyu, nayo itahifadhiwa. Mwenyezi Mungu Anasema *إِنَّا نَحْنُ نَكْتُبُ الذِّكْرَ وَ إِنَّا لَهُ لَحَافِظُونَ* (Sura Al-Hijr 15:10) , yaani Sisi Tumeyateremsha mauidha haya na Kurani hii na ni juu Yetu kuziandaa njia za kuihifadhi.

Akaihifadhi Alvyotaka na Anaendelea kuihifadhi. Katika zama ambapo kulikuwa hamna karatasi kwa kuandika Kurani Tukufu kwa wingi ili kuihifadhi, hapo Mwenyezi Mungu Akazitayarisha malaki ya akili na kuzijaalia kipawa cha kuihifadhi Kurani Tukufu kwa ghaibu. Miongoni mwao walikuwepo maelfu waliokuwa na kipaji kizuri sana cha kukumbuka kiasi hiki kwamba walikuwa hawafanyi makosa ya hata kasra na fataha pia; lakini wote wakiwa pamoja walikuwa na kipaji cha kuhifadhi kiasi hiki kwamba kama mmojawapo akifanya makosa, papo hapo mwingine akamsahihisha, yaani kwa jumla mahafidhi wa Kurani walikuwa hawawezi kufanya makosa.

Kisha kwa kuhakikisha kwamba mahafidhi walikithiri hivyo kwa sababu ya matakwa ya Mungu, idadi ya mahafidhi ilianza kupungua pindi Kurani Tukufu ilipoanza kuchapishwa kwenye karatasi. Hii yathibitisha kwamba njia ile pia ililetwa na Mungu, tadbiri ya binadamu haikuwa ndani yake. Ili kuhifadhi maana za Kurani Tukufu, Mwenyezi Mungu Aliwaumba mawalii watawa mwanzoni mwa kila karne, katikati ya karne na mwishoni mwa karne pia, ambao walimkaribia sana Mwenyezi Mungu hata kwamba Mwenyezi Mungu Mwenyewe Alikuwa Anawafundisha elimu ya Kurani, Mwenyewe Alikuwa Mwalimu wao, nao walikuwa wanatimiza mahitaji ya nyakati zao, kufumbua masuala ya wakati huo na kutatua matatizo ya zama zao.

Kisha, sasa kwa njia ya Hadhrat Masihi Mau'udi^{as}, Mwenyezi Mungu Ameanzisha duniani mkakati mkubwa kwa kuishindisha Islam ulimwenguni na kutapakaza mwanga wa Islam. Na kwa fadhili yake tu Ametujaalia kujiunga na Jumuiya yake na kutupatia fursa ya kwamba tukipenda tuwe wenye kupata ridhaa ya Mwenyezi Mungu kwa kutoa dhabihu zile Anazotutakia Yeye kuzitoa. Mungu Atujaalie kwamba kila mmoja wetu awe amejiipatia radhi Yake.

Hivyo, Mwenyezi Mungu Alihifadhi Kurani Tukufu kilafudhi pia na kimaana vilevile. Akahifadhi katika hali hizo kwa njia ambayo labibu yeyote hawezi kukana kwamba kuhifadhi huku Kurani Tukufu siyo natija ya tadbiri yoyote ya kibinadmu. Hii ni natija tu ya fadhili ya Mwenyezi Mungu na ni kwa sababu ya ulinzi wake mahususi ambao Aliuahidi. Yu Mkweli wa ahadi zake na Mkweli wa kauli Yake, Akatimiza ahadi Yake.

Yapasa tuendelee kumwomba daima Mwenyezi Mungu kwamba Atuingize kati ya waja wake ambao Awatwishe jukumu la kuhifadhi Kurani Tukufu kimaana. Yaani tuwe kujipatia elimu sahihi ya Kurani, tusiwe kuzifuata tamaa za nafsi zetu, tusiwe kuitumia Kurani Tukufu kujipatia matilaba ya kidunia, bali tuwe wenye kujifunza elimu za kweli za Kurani kutoka kwa Mola wetu, na tuingie ndani ya wapendwa Wake ambao Mwenyezi Mungu Huwapatia fadhili yake na kuwapitia hao Yeye Anaondoa mapazia toka kwa elimu za lazima za Kitabu

Makusudio 23 Adhimu ya Ujenzi wa Baitullah

adhimu kilicho *Maknuun* – kilichofichika – na Asitujumishe pamoja na wale wasomao Kurani Tukufu midomoni lakini mioyo yao huwa mitupu, hamna nuru ya Kurani ndani yake.

(Gazeti la Al-Fadhl, Rabwah, 4 Juni 1967)

⑧

**Hazipotei Bure
Amali za Watoao Dhabihu
kwa Ridhaa ya
Mwenyezi Mungu**

Hotuba ya Ijumaa, 2 Juni 1967,
Masjid Mubarak, Rabwah, Pakistan.

“Kwa kushuhudia neema na baraka za Baitullah, dunia itafikia natija hii kuwa wale wanaotoa dhabihu sana kwa ridhaa ya Mwenyezi Mungu na wakiipa kisogo dunia wanakuwa Wake tu, amali zao hazipotei bure, bali hupata matunda matamu ya amali zao zilizokubaliwa, na hutoka natija bora sana za amali zao wazifanyazo kwa unyenyekevu na upendo.”

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ¹⁶

تَحْمَدُهُ وَنُصَلِّي عَلَى رَسُولِهِ الْكَرِيمِ¹⁷

Baada ya Shahada mbili, A'udhu na usomaji wa Sura Al-Faatiha, alisema:

Kusudio la kumi na sita la ujenzi wa Kaaba limetajwa ndani ya *وَأَرْزُقُ أَهْلَهُ مِنَ الْمَبْرُكَاتِ*, na imeelezwa kwamba kwa kushuhudia neema na baraka za Mwenyezi Mungu dunia itafikia natija hii kuwa wale wanaotoa dhabihu sana kwa ridhaa ya Mwenyezi Mungu nao wakiipa kisogo dunia wanakuwa Wake tu, amali zao hazipotei bure, bali hupata matunda matamu ya amali zao zilizokubaliwa, na hutoka natija bora sana za amali zao wazifanyazo kwa unyenyekevu na upendo.

Kurani Tukufu yenyewe imedai ya kuwa kusudio hili nalo limetimia kupitia Nabii Mtukufu^{saw} na sheria ya Kurani Tukufu, kama Asemavyo Mwenyezi Mungu ndani ya Sura Al-Qasas 28:58 ya kwamba:

وَقَالُوا إِنَّا تَتَّبِعُ الْهُدَىٰ مَعَكَ نَتَّخِظُكَ مِنَ الْغِيَابِ أَوْ لَمْ تُنْكِرْ لَهُمْ حَرَمًا أَوْنَا يُجِبِي الْبَيْتِ شَرْتُ كُلِّ شَيْءٍ
رِزْقًا مِّن لَّدُنَّا وَلَكِنَّ أَكْثَرَهُمْ لَا يَعْلَمُونَ ۝

Hapa Mwenyezi Mungu Anasema kwamba waambiwapo sheria ya Kurani Tukufu, mwongozo wa Kurani Tukufu na mafundisho yake, husema tukiufuata mwongozo ulioleta wewe tutanyakuliwa kutoka nchi yetu, dunia itakuwa adui yetu na itatupinga na itajiandaa kutuangamiza, nasi hatutajimudu kuwakabili watu wa

¹⁶ Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwingi wa Ukarimu.

¹⁷ Twamhimidia Yeye na kumsalia Mtume Wake mhashamu.

dunia; kwa nini tujiadalie sababu za kutuhilikisha kwa kuuamini mwongozo huu. Mwenyezi Mungu Anasema *أَوْ لَمْ نَكُنْ لَهُمْ حَرَمًا أَوْيًا*, je hawajui kwamba Sisi Tulimhusisha Nabii huyu na sheria hii kwa mahali patakatifu na kuifanya Baitullah kuwa alama moja ya jambo hili kwamba Nabii huyu na wenye kumwamini watakuwa katika ulinzi wa Mwenyezi Mungu; na sheria itakayomteremkia, jukumu la kuihifadhi pia litakuwa la Mwenyezi Mungu tu pekee.

Historia ya dunia inatoa ushahidi kwamba ile ahadi Aliyoifanya Mwenyezi Mungu kuihifadhi Kaaba takatifu Akaitimiza barabara. Washambulizi siku zote walihizika na kushindwa. Na dunia imeshuhudia pia na itadumu kushuhudia kuwa nguvu yoyote ya dunia, hila yoyote ya dunia, njama yoyote ya dunia haiwezi kumwangamiza Nabii Mtukufu^{saw} na kusudio lake, wala ughushi wowote hauwezi kujiingiza ndani ya sheria ya Kurani Tukufu.

Mwenyezi Mungu Amesema hapa kwamba je hawaoni kuwa Sisi Tumewapa mahali pa usalama na amani, ndani ya haram ya Kaaba pia, ndani ya haram ya umaasumu wa Nabii Mtukufu^{saw} pia na ndani ya haram ya sheria ya Kiislamu yaani Kurani Tukufu pia? Hivyo vyote ni vitu vilivyohifadhiwa, ni waja waliohifadhiwa, ni mahali palipolindwa. Kama mkiungana na patakatifu, basi mtakuja chini ya ulinzi wa Mwenyezi Mungu jinsi haram ilivyo katika ulinzi Wake, na jambo hili litakuwa ghalati kwamba *نُتَخَطَفُ مِنْ أَرْضِنَا*; hakuna nguvu yoyote itakayoweza kuwaangamizeni.

Tena Mwenyezi Mungu Alisema **يُجِبِّي إِلَيْهِ شُرَكَاتُ كُلِّ شَيْءٍ** , kwamba tumeambataisha na haram jambo hili pia kwamba matunda ya kila aina yanaletwa hapa. Yaani, kwa kuungana nayo, yanawezekana kutenda matendo mema ya kila aina pia. Mtu anapata uwezo wake pia toka kwa Mwenyezi Mungu, na matokeo yake bora pia yameahidiwa. Basi, mtu yeyote ambaye anayo nia halisi isiyo na ufisadi ndani mwake, huyo anapata matudna yake. Hivyo, hapa kwa kuunganisha **يُجِبِّي إِلَيْهِ شُرَكَاتُ كُلِّ شَيْءٍ** na haram, na kwa kufanya haram kuwa dalili ya kubatilisha msimamo wao wa **وَقَالُوا إِن تَتَّبِعِ الْهُدَىٰ مَعَنَا نَنخَضُكَ مِنَ الْأَرْضِ** , Mwenyezi Mungu Amebainisha uhakika huu kwamba matunda na malipo yaliyotajwa katika dua ya Hadhrat Ibrahimu^{as} yalihusiana kikweli na Nabii Mtukufu^{saw} na umati wake na uhusiano huu hata sasa upo na utadumu.

Matunda hayo (**مِنَ الشُّرَكَاتِ**), maelezo yake yametolewa ndani ya Sura Muhammad (47:16). Mwenyezi Mungu Anasema:

مَثَلُ الْجَنَّةِ الَّتِي وُعدَ الْمُتَّقُونَ ۖ فِيهَا أَنْهَارٌ مِنْ مَاءٍ غَيْرِ آسِنٍ ۖ وَأَنْهَارٌ مِنْ لَبَنٍ لَمْ يَتَغَيَّرَ طَعْمُهُ ۖ وَأَنْهَارٌ مِنْ حَمِيمٍ لَذِيٍّ لِلشُّرَبِينَ ۖ وَأَنْهَارٌ مِنْ عَسَلٍ مُصَفًّى ۖ وَلَهُمْ فِيهَا مِنْ كُلِّ الثَّمَرَاتِ وَمَغْفِرَةٌ مِّن رَّبِّهِمْ ۗ

Mwenyezi Mungu Ameeleza hapa kwamba wale wacha Mungu wanaotenda sawa na mwongozo unaoitwa **هُدًى** (mwanzoni mwa Sura Al-Baqara), imani yao imara na itikadi zao sahihi zinageuzwa kuwa sura ya Bustani, kwa sura ya miti kimajazi humu duniani, na kwa kweli huko Akhera zinachukua sura ya miti. Mwenyezi Mungu Amesema sehemu hii kwamba wale watu wanaotekeleza

agizo letu na kuwa wacha Mungu kweli, hao hupewa pepo ambamo mna miti ya kila aina na **فِيهَا أَنْهَرٌ مِنْ مَاءٍ غَيْرِ آسِنٍ**. Hao huwezeshwa kutenda matendo mema na hujaaliwa uchangamfu wa mtima, nao kwa kuonja utamu wake hawawi tayari kwa vyovyote kuyaacha matendo hayo. Basi Akasema kuwa amali hizi njema katika dunia hii na huko Akhera zitageuzwa kuwa mito yenye maji yasiyoharibika, yaani baada ya kuzoea utamu wa amali njema, mazoea haya ya kusikia utamu huu hayataachika. Kisha kwa sababu ya imani madhubuti watakapoanza kutenda matendo mema kikweli kwa ikhlasi ya moyo sawa na miongozo waliyoteremshiwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu, hapo watafunguliwa milango ya maendeleo zaidi ya kiruhania. Mambo yaliyokuwa siri hapo kabla, na yalikuwa ni siri ya kiruhania, siri hiyo itafichuliwa kwao na kinatija ruhania ya mwaminio itapata maendeleo. Na hali hii, **أَنْهَرٌ مِنْ لَدُنِّ لَمْ يَتَغَيَّرْ طَعْمُهُ**, itachukua sura ya maziwa yasiyohofiwa kugeuka utamu wake. Kisha kwa sababu ya elimu hizi za kiroho, yatazalika ndani mwao mapenzi makubwa ya kweli yaziunguzayo dhambi. Watajipatia mauti na kupotea ndani ya huba ya Mwenyezi Mungu, watadumu kulewa na mapenzi haya makali, na hali kama hizi zitageuzwa kuwa **أَنْهَرٌ مِنْ حَبْرِ لَدَّةٍ لِلشَّرِيبِينَ**¹⁸. Hapa Ameeleza pia kwamba asiye na tajiriba hii, atajuaje ladha yake? Na ndiyo sababu watu kama hawa hawaelekei kwenye huba ya

¹⁸ Sura Muhammad, 47:16

Mungu, kwani miba mingi ya majaribio imepandwa pembeni mwa mto huu. Lakini aionjaye mara moja huba ya Mwenyezi Mungu, huyo tu aweza kueleza kwamba ladha iliyopo ndani ya mahaba ya Mungu, haimo katika kitu kiwacho chochote kile. Kisha Akasema kwamba ajiangamizaye ndani ya huba ya Mwenyezi Mungu, mtu huyo amepangiwa kupata **أَنْهَرُ مِنْ عَسَلٍ مُّصَفًّى**. Yuaondokewa na maradhi yake yote, kisha maradhi yoyote hayawezi kumshambulia, hupata kupona kikamilifu fika, husalimika na mashambulizi ya shetani, kana kwamba amekuja mapajani mwa Mungu na hana hatari yoyote. Hii ndiyo hali itakayozalika kwa sura ya **أَنْهَرُ مِنْ عَسَلٍ مُّصَفًّى** duniani humu pia kwa namna fulani na huko Akhera vilevile kwa namna inayoafikiana na hali ya Akhera.

Kisha Mwenyezi Mungu Alisema **كُلِّ السَّبَاتِ** , kwamba matunda haya mtayapata kutoka katika Islam, yaani mtapewa matunda ya kila aina. Kutakuwa na miti ya aina zote. Itikadi zilizo sahihi zitageuka kuwa sura ya miti, kisha mtajaaliwa imani ile ambayo kwa sababu yake mkivumilia taabu ya kila aina kwa shauku na uchangamfu mtatenda matendo mema. Na amali hizo njema zitapewa sura ya mito ya maji ambayo kwayo bustani hizo zitastawi. Pasipo maji bustani haiwezi kustawi; pasipo amali njema mtu hawezi kuimarika katika itikadi sahihi. Zisipobaki amali njema, mtu hulazimika kubadilisha itikadi pia. Kwenye hii hii imeashiriwa ndani ya **وَعَدَ الْمُنْفِقُونَ** . Kwa hiyo, hatuwezi

kusema kwamba katika sheria ya Kurani uharibifu waweza kutokea, kwani ndani ya Kurani Tukufu hauwezi kutokea uharibifu. Lakini kwa sababu ya itikadi hii mtu alazimika kutenda. Hivyo, Akasema kwamba yeye mtu huyo atajaaliwa na Mwenyezi Mungu kutenda matendo mema, na atajaaliwa hivi kwamba *غَيْرِ اسِين* , hatakuwa na hatari kwamba shetani wakati wowote akimshawishi ampeleke upande mwingine.

Kisha atafichuliwa elimu na siri za ruhania, nazo zitageuka kuwa maziwa, ndipo kwa kufichiliwa kwa siri za ruhania mtimani mwake mtazalika mapenzi tele ya Mola wake, na mapenzi haya ya Mungu yatachukua sura ya *وَ أَنْهَرُ مِنْ خَيْرٍ لَدَّةً لِلشَّرِيبِينَ* na ndipo atasalimika na kila maradhi ya kiroho, yaani atajaaliwa *وَ أَنْهَرُ مِنْ عَسَلٍ مُصَفًّى* . Basi, haya ndiyo matunda yatolewayo na Islam, haya ndiyo matunda yatajwayo ndani ya aya hii kwamba Hadhrat Ibrahim^{as} aliomba dua kwa ajili yake *وَ أَرْزُقْ أَهْلَهُ مِنَ الشَّرَاةِ* .

وَ مَغْفِرَةً مِنْ رَبِّهِمْ , Mwenyezi Mungu Anasema kwamba msingeweza kupewa matunda haya kwa sababu tu ya amali zenu kama msingejaaliwa maghufira kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Hivyo, ahadi hii ya maghufira pia mmepewa ndani ya Islam tu. Hadhrat Masihi Mau'udi^{as} hakuashiria kwenye aya hii, lakini nilitafakari, na nyinyi mkifikiria kwa makini mtafikia natajia hii kwamba Masihi Mau'udi^{as} ameeleza muradi wa aya hii hii ndani ya dondoo hili nitakalowasomea sasa hivi. Hadhrat Masihi Mau'udi^{as} alisema:

“Sasa twapenda kudhihirisha kiasi fulani kwamba ni yepi matunda ya Islam. Basi, ibainike kuwa mtafutaji mkweli wa Mola wake aimarikapo kikamilifu katika Islam, na si kwa kujikalifisha au kujisingizia, bali kitabia kila nguvu katika njia za Mwenyezi Mungu ikitumika katika kazi Yake, hapo natija ya mwisho ya hali yake huwa hii kwamba maonyesho ya mwongozo wa Mwenyezi Mungu yakiondolea mbali mapazia yote yanaelekea kwake naye anateremkiwa na baraka za namna namna. Na yale maamrisho na zile itikadi zilizokuwa zimekubaliwa kiimani tu na kwa kusikia, sasa zinafunukiwa wazi wazi na kuhisika kwa njia ya kashfi sahihi na funuo za yakini fika, na mambo magumu ya sheria na dini na siri zilizofichika sana za *millati hanifiyya* hufichuliwa kwake na hutembezwa katika Ufalme wa Mungu ili ajipatie daraja kamili ya yakini na maarifa; na anajaaliwa baraka ndani ya ulimi wake na usemi wake, amali zake zote na kauli zake, kutikisika kwake na kutulia kwake; na anajaaliwa ushujaa, uimara na nguvu kinduni, na anapewa daraja ya juu sana ya kupanuliwa kifua. Na kwa kumwondolea ufinyu wa mapazia ya ubinadamu, na udunifu, ubahili, utelezi wa mara kwa mara, mtazamo finyu, utumwa wa nyege, khulka mbovu na kila aina ya giza la nafsi, anajazwa badala yake nuru ya khulka za Mungu. Ndipo yeye akibadilika kikamiifu

Makusudio 23 Adhimu ya Ujenzi wa Baitullah

anazaliwa upya na anasikia kwa Mungu na kuona kwa Mungu, na atikisika pamoja na Mungu na anatulia pamoja na Mungu, ghaidhi yake huwa ghaidhi ya Mungu, na huruma yake, huruma ya Mungu. Na katika daraja hii dua zake hukubaliwa kwa sababu ya uteule wake si kwa kumjaribu. Yeye huwa Hoja ya Mungu na Amani ya Mungu juu ya ardhi, na huko mbinguni uwepo wake unashangiliwa. Na atia bora fika anayotunukiwa ndiyo maongezi ya Mungu na mazungumzo Yake yasiyo na shaka wala wasiwasi, pasipo mavumbi yoyote, kama mwanga wa mwezi, huendelea kumteremkia mtimani mwake na yanayo ladha yenye kuathiri mno na kuleta utulivu na uraifu.”

(Aina Kamaalaate Islam, uk. 226-231)

Haya ndiyo matunda aliyoahidiwa Hadhrat Ibrahim^{as}, na haya ndiyo matunda uliyojaaliwa umati wa Muhammad^{saw} kwa wingi sana mpaka ozi lionalo lashikwa na mshangao.

Kusudio la kumi na saba limeelezwa ndani ya رَبَّنَا تَقَبَّلْ مِنَّا na imebainishwa kwamba amali si chochote mpaka ziwe zimekubaliwa, kwa hiyo daraja za juu sana za ruhania zaweza kupatikana kwa dua tu. Ndani mwake mliashiriwa kwamba Nabii mmoja mwenye adhama kubwa atainuliwa hapa na kwa baraka zake za ruhania utazaliwa umati mmoja utakaofahamu uhakika huu kwamba dhabihu za hali ya juu pia ni bure wala hazina

natija pasipo kuvuta fadhili ya Mwenyezi Mungu kwa njia ya dua zenye unyenyekevu. Hivyo, umati huu utafikia daraja ya juu ya maarifa kwa njia ya dua, na kwa sababu ya maombi tu utapata matunda bora ya amali zake.

Kurani Tukufu imetaja shabaha hizi tatu kwa uwazi sana. Nafikiri kwamba mwanga iliotia Islam juu ya dua na kukubaliwa kwake hakuna dini nyingine iwayo yoyote ile iliyouita. Hakuna dini yoyote inayoweza kutajwa kukabiliana na Islam kuhusu jambo hili.

Mwenyezi Mungu Anawataja waja wa Rahmani katika sehemu ya mwisho ya Sura Al-Furqaan kwamba waja wa Rahmani ni wale wanaotenda matendo kadhaa au wanajiepusha na matendo kadha na kadhalika. Rahman maana yake ni Yule Mtukufu (Allah) Anayemfanyia hisani mtu pasipo yeye kufanya amali yoyote na bila kuwa na haki. Amali zote za waja wa Rahmani zimetajwa mbele ambazo kidhahiri zahusiana na Urahimu.

Hivyo, katika sehemu hii yameelezwa madhumuni haya kwamba hata matendo mema mfanye kadiri mpendayo, lakini hamtapata malipo yake mpaka baraka ya Urahmani ujumuike na Urahimu. Ndiyo sababu madhumuni haya Alipoyamaliza, Akasema kwa maneno matukufu ¹⁹ قُلْ مَا يَعْزُبُ عَنْ رَبِّيَ لَوْلَا دُعَاؤُكُمْ ۚ فَقَدْ كَذَّبْتُمْ فَسَوْفَ يَكُونُ لِزَامًا ﴿٢٥﴾ (Sura Al-Furqaan 25:78) yaani, ni sawa kwamba hakuna budi kutenda matendo mema, na kuepukana na matendo

¹⁹ Sura Al-Furqaan 25:78

maovu pia kwamfaa binadamu, lakini kumbukeni kuwa Mungu Anawajaliye nyiye na mema yenu msipoomba dua! ²⁰ لَوْ دَعَاكَ . Naam, kama nyinyi mnamjali, basi kwa maombi ivuteni fadhili yake. Mtakapokuwa mmevuta fadhili yake kwa dua zenu, hapo amali zenu zitawanufaisheni. Hata hivyo dua pia haina maana mpaka pamoja na dua ukabalifu wa dua pia upatikane. Kwa dua kukubaliwa pia hutakiwa fadhili ya Mwenyezi Mungu, na kwa ajili yake pia hulazimika kuomba dua. Hivyo, twapaswa kudumu kuomba: Ee Mungu, tunatenda chochote au hatutendi, dua tuziombazo kwa kukubaliwa kwa amali zetu njema pia zaweza kukufikia hapo tu Uamuapo kukubali dua zetu. Basi, kwa dua kukubaliwa, tena inaombwa dua. Hivyo, Mwenyezi Mungu Amesema hapa kuwa Mungu Hawajalini, Hazijali amali zenu, Hazijali dhabihu zenu. Zile sadaka mzitoazo katika njia yake Anazijaliye! Je hazina Zake zi tupu hata kwamba azijali mali zenu? Nyinyi mwatekeleza maamrishi yake, mwajibidiisha mno na kujaribu katika njia yake, hata hivyo Hawajalini. Mwaweza kunufaika na hivyo vyote hapo tu mvutapo fadhili yake kwa kuomba dua. Mng'ao wa Urahmani unapojumuika na mng'ao wa Urahimu ndipo bidii zenu hakiri pia zaweza kufikia mbingu ya saba. Lakini kama mkidhani kuwa mwaweza kufika hata kwenye mbingu ya kwanza pasipo fadhili Yake, basi mmekosea. Bila

²⁰ Sura Al-Furqaan 25:78

fadhili yake mwaweza kufika mpaka chini sana ardhini, mapajani mwa shetani; lakini hamwezi kufika mapajani mwa Mungu Aliye Rahmani pasipo fadhili na rehema Yake. **فَقَدْ كَذَّبْتُمْ** : Mnaukataa uhakika huu. Miongoni mwenu wapo kidhahiri wacha Mungu sana na watawa, lakini wanajionea fahari juu ya amali zao na dua zao, ibada zao za usiku na huduma wanzawatolea watu wa dunia. Mwenyezi Mungu Hawajali kabisa mpaka waombe dua pamoja na sharti zake zote na mpaka Mwenyezi Mungu Akikubali dua yao azikubali amali zao kwa wingi wa Urahmani wake.

فَسَوْفَ يَكُونُ لِزَامًا : Matokeo ya kukadhibisha kwenu yataendelea kuambatana nanyi. Sasa angalieni siku hizi katika baadhi ya madhehebu ya Waislamu wapo baadhi yao wanaojitahidi sana, lakini wanajipatia matokeo gani ya bidii zao hizo? Tufahamavyo, hawapati ile natija inayokuwa ya amali kama hizo hizo za mcha Mungu, bali hata sawa na sehemu ya elfu ya amali hizo.

Hadhrat Masihi Mau'udi^{as} anasema ndani ya Braahine Ahmadiyya:

“Kwa hakika, hakuna budi kufikiria mambo haya mawili kuhusiana na dua. Yaani, kwanza kufikiria kwamba Mwenyezi Mungu Anao uwezo wa kila namna ya utunzaji, ulezi, rehema na kutoa malipo, na sifa zake hizi kamilifu hudumu kufanya kazi siku zote. Pili, kuzingatia kwamba binadamu havezi kupata kitu pasipo kujaaliwa na kusaidiwa

na Mungu. Hakuna shaka kwamba mambo haya mawili yanapogandamana mtimani mwa mtu pindi aombapo dua, yanageuza halani hali ya binadamu kiasi hiki kwamba mtu mwenye kiburi anaanguka ardhini akilia, na mkaidi mwenye mtima mgumu anatokwa na machozi. Huu ndio mtambo wa kutilia uhai ndani ya mfu aliyeghafilika. Kwa kuzingatia mambo haya mawili, kila moyo huvutwa kwenye kuomba dua. Ilmuradi, hii ndiyo njia ya kiruhania kwa roho ya binadmau kuelekea kwenye Mungu, na kujijua unyonge wake na kutambua msaada wa Mola. Kwa njia iyo hiyo binadamu hufikia ulimwengu wa kutojijua ambapo haibaki hata alama ya uwepo wake mchafu, bali yaonekana tu jalali ing'aayo ya Mwenye adhama, na Huyu Huyu ndiye Aonekanaye kuwa rehema yote na tegemeo la kila kiumbe na tiba ya kila taabu na chanzo cha kila baraka. Mwishowe kutokana na hii, yadhihirika hali fulani ya kujipoteza ndani ya Mungu, ambayo kwa sababu yake mtu haelekei kwenye mahuluku wala kwenye nafsi yake wala utashi wake, bali hujisahau kabisa ndani ya huba ya Mungu; na kwa kushuhudia Yule Dhati wa kweli, uwepo wake mwenyewe na wa vitu vingine vilivyoubwa unaonekana kana kwamba haupo.”

(Baraahine Ahmadiyya, J. 4, uk. 480-482, maelezo ya pembeni Na. 11)

Kusudio la kumi na nane lililoelezwa ni kwamba kwa sababu ya kuimarika Kaaba, dunia itapata maarifa ya Mungu Mwenye kusikia sana. Umati mmoja utazalishwa hapa utakaomtambulisha Mungu Asikiaye sana kwa dunia, na dunia haitathubutu kuukana uhakika huu, kwani washughulikao katika maombi kwa kujinyenyekeza na kwa bidii ndiyo wayashuhudia maonyesho ya sifa ya Mwenye kusikia sana. Mwenyezi Mungu Ananena ndani ya Sura Mu'min 40:61 **وَقَالَ رَبُّكُمْ ادْعُونِي أَسْتَجِبْ لَكُمْ إِنَّ الَّذِينَ يَسْتَكْبِرُونَ عَنْ عِبَادَتِي سَيَدْخُلُونَ جَهَنَّمَ دُخْرِينَ ۝** yaani, Mola wenu Anasema niombeni, Nitasikia dua yenu, lakini wanaotakabari na kukengeuka na ibada yangu ya kweli – yaani ibada ile ninayoikubali na kuhusiana nayo Nimeishasema mahali pengine ndani ya Kurani Tukufu kwamba pamoja na ibada zenu yalazimu ziwepo dua zenu pia – na wale wasiofikisha ibada yao kwenye darja hii ya ibada ya kweli hasa kwa sababu ya kiburi, Nitawapa adhabu ya jahanamu, nao wataingia ndani ya jahanamu ya ushinde, ya ghaidhi na ya hasira yangu. Kadhalika Mwenyezi Mungu Alisema ndani ya Sura Al-Baqara 2:187 ya kwamba **وَإِذَا سَأَلَكَ عِبَادِي عَنِّي فَإِنِّي قَرِيبٌ ۚ أُجِيبُهُمْ بِمَا سَأَلُونِي لَعَلَّهُمْ يَرْشُدُونَ ۝** دَعْوَةَ الدَّاعِ إِذَا دَعَانِ فَلْيَسْتَجِيبُوا لِي وَلْيُؤْمِنُوا بِي لَعَلَّهُمْ يَرْشُدُونَ ۝

Ewe Mtume, kama watumishi wangu wakuulize kunihusu Mimi kwamba kuna uhakikisho gani wa Uwepo wa Mwenyezi Mungu, na twawezaje kupata elimu ya sifaze, basi uwajibu kwamba Mungu Yu karibu nanyi, mgonge mlango wake, mtafunguliwa, na Mwombeni (Sawa na sharti alizoeleza), dua zenu zitakubaliwa, na kwa sababu ya kupokelewa dua mtapata kujua elimu ya Dhati Yake na ya sifa zake,

na baada ya maarifa na utambuzi wake nyoyo zenu zitajipoteza ndani ya huba Yake.

Hivyo, Mwenyezi Mungu Akasema kuwa yawapasa **وَلْيُؤْمِنُوا** **۞** kwamba waniamini – Dhati yangu na Sifa Zangu – ili wapate kuongoka. Hadhrat Masihi Mau‘udi^{as} kuhusiana na jambo hili anasema ndani ya Barakaatud Dua – Baraka za Dua:

“Na uhakika wa dua ni huu kwamba kunakuwepo na uhusiano wenye mvuto kati ya mja mwema na Mola Wake. Yaani, kwanza Urahimu wa Mwenyezi Mungu humvuta mja halafu kwa mivuto ya ukweli wa mja, Mwenyezi Mungu Humkurubia yeye. Na uhusiano huo katika hali ya kuomba dua ukifikia daraja maalum, huzalisha sifa za ajabu. Hivyo, wakati mtu akumbwapo na tatizo zito anaelekea kwa Mwenyezi Mungu kwa yakini kamili, matumaini kamili, mapenzi kamili, uaminifu kamili na hima kamili na huku akizinduka sana kabisa akiyachanilia mbali mapazia ya mghafala huendelea mbele zaidi na zaidi katika nyanja za fanaa (kujifia ndani ya huba ya Mwenyezi Mungu). Lo! mbele analikuta Baraza la Mwenyezi Mungu, na kwamba hakuna mshiriki yeyote pamoja Naye. Ndipo roho yake inaweka kichwa juu ya kizingiti hicho na nguvu ya kuvuta iliyowekwa ndani yake inayavuta kwake maelekezo ya Mwenyezi Mungu na hapo ndipo Mwenyezi Mungu Mwenye Shani Anaelekea

Makusudio 23 Adhimu ya Ujenzi wa Baitullah

kwa kuitimiza kazi hiyo, na athari ya dua hiyo Anazitilia sababu zote za asili ambazo kwazo zinazalika sababu zile zilizo muhimu kwa kupata makusudio haya.”

(Baraka za Dua, uk. 21; Kiurdu uk. 6)

Kusudio la kumi na tisa lililoelezwa ni kwamba si tu sifa ya *Samii*’, bali maonyesho ya sifa ya *‘Aliim* (Mjuzi sana) pia dunia itayashuhudia kupitia umati huu. Kukataliwa baadhi ya dua, au kutotimia baadhi ya dua kwa njia iliyoombwa hakutathibitisha kwamba Mungu wetu Mtukufu si *Samii*’ au kwamba hana uwezo wote au nguvu zote, bali kutathibitisha kuwa pamoja na kuwa na nguvu zote na uwezo wote Yu *‘Aliim* pia. Na ukubalifu wa dua una uhusiano wenye keto na sifa *‘Aliim*. Hadhrat Masihi Mau’udias anasema:

“Na ikumbukwe pia kuwa unyenyekevu pekee hautoshi katika kuomba dua, bali yahitajika pia Ucha Mungu, utakaso, uongofu, yakini kamili, mapenzi kamili, mwelekeo kamili, na kwamba yule mtu anayejiomba dua au anayeombewa dua kulipata kwake jambo hilo kusiwe pia kinyume na hekima ya Mwenyezi Mungu kwa sababu pengine ndani ya dua masharti yote hujumuika lakini kile kitu kilichoombwa huwa kinyume na hekima ya Mungu katika elimu ya Mwenyezi Mungu kwa ajili ya muombaji na kunakuwa hamna heri katika kuitimiza.”

(Baraka za Dua, uk. 26-27; Kiurdu uk. 10)

Sehemu hii, sharti alizotaja Hadhrat Masihi Mau'udi^{as} kwa maombi kukubaliwa, yaani Takwa, utakaso, yakini kamili, huba kamilifu na kadhalika, zahusiana na ukubalifu ule wa dua ulio kwa sababu ya utakaso wa mtu. Lakini ule ukubalifu wa dua unaokuwa kwa majaribio, sharti hizi hazihusiani nao. Hadhrat Masihi Mau'udi^{as} amezungumzia madhumuni hii kwa utondoti na amesema kwamba Mwenyezi Mungu [wakati mwingine] Anawaonyesha makahaba ruya za kweli ili kuwapatia njia ya mwongozo na kuwatilia moyoni mwao kwamba watoke katika uchafu huu na kukikimbilia chanzo na chemchem ya utakaso na wajaribu kujitakasa. Lakini dua inakataliwa ikiwa moyo wa mwenye kuomba dua haujang'arishwa na mwanga wa Takwa, au kifua chake hakina harufu nzuri ya utakaso, au ulimi wake haushiki njia ya kusema kweli, na mtima wake haujajaa yakini kamili na huba kamilifu, roho yake si yenye kuelekea kikamilifu kwa Mola wake, ama kitu kilichoombwa si chenye heri mbele ya Mjuzi wa Mambo ya ghaibu, kwa yule aliyeombewa kujaaliwa kitu hiki. Lakini katika sura ya mwisho, Mwenyezi Mungu Anampatia mtu malipo ya dua kama hii kwa njia nyingine, kama asemavyo Hadhrat Masihi Mau'udi^{as}:

“Je huu si uthibitisho wenye kutuliza kwamba kanuni moja ya kiruhania ya kudura ni kuwa kwa kuomba dua, Mungu Anaelekea sana kwa mwombaji, naye anapata utulivu, uraufu na ustawi wa kweli. Kama hatukupotoka katika kuomba

jambo fulani, twalipata hilo. Na kama twakosea katika maombi yetu – jinsi mtoto mkosefu anavyomwomba mamake kupewa nyoka au kipande cha moto – hapo Mungu Hutupatia kitu kilicho bora kwa ajili yetu, na hata hivyo anazidisha pia imani yetu kwa sura zote mbili. Kwani, kwa njia ya dua twapata elimu kabla ya tukio la jambo, na yakini yetu inazidi sana, kana kwamba tunapata kumwona Mungu wetu. Na kuna uhusiano baina ya dua na ukubalifu wake unaoendelea barabara tangu mwanzo na tangu binadamu kuzaliwa. Mwenyezi Mungu Anaponuia kufanya jambo, hapo Suna ya Mungu ni hii kwamba mja wake fulani mwenye ikhlasi huanza kushughulikia kuomba dua kwa kutotulia, kwa uchungu na majonzi na hutumia uwezo wake wote na maelekeo yake yote ili jambo hili lifanyike, ndipo dua za mtu huyu ajifiaye huvuta baraka za Mungu toka mbinguni na Mwenyezi Mungu Huzalisha njia mpya za kutendeka jambo hili.”

(Ayyaamus Sulh, uk. 10)

Hivyo, Mwenyezi Mungu Anatuambia ndani ya Kurani Tukufu mambo matatu ya msingi kuhusiana na maombi:

Mosi, mpaka tuvute fadhili ya Mwenyezi Mungu kwa dua, kwa dua iliyokubaliwa, hatuwezi kufurahia amali zetu, wala hatuwezi kusema kwamba Mwenyezi Mungu

Atazipokea dua hizi au hapana, kwani Mwenyezi Mungu Ameishatuambia kwa uwazi na kwa maneno ya kuogofya *قُلْ مَا يَعْبَأُ بِكُمْ رَبِّي لَوْلَا دُعَاؤُكُمْ* , Mola wangu Anawajaliye, Anayajaliye mema yenu, Anazijaliye amali zenu, msipoelekea Kwake mkimwomba dua?

Lakini, sisi twamjali Yeye. Kama tukitaka kuwa Yeye Aendelee kutudhihirishia maonyesho ya mahaba yake, basi hatuna budi kuvuta fadhili yake kwa njia ya dua, zile dua zitimizazo sharti zote za maombi. Tusipofanya hivyo, amali zetu hazina thamani hata sawa na thamani ya mguu wa nyenyere machoni mwa dunia.

Pili, Mwenyezi Mungu Amesema kuwa Islam imetupatia mafundisho ambayo tukiyazingatia, na kutekeleza maagizo ya Islam, twaweza kutarajia kwamba Mungu wetu Alie *Samii'* Atasikiliza dua zetu na kuzikubali na kutuandaalia rehema Yake.

Na jambo la tatu tuliloambiwa ni kuwa ingawaje Mwenyezi Mungu ni *As-Samii'* , lakini pia Yu *'Aliim*. Mtu anaweza kuidanganya dunia, anaweza kujivalia kidhahiri juba la utawa, anaweza kutangaza utawa wake kwa kujisingizia sana, lakini hawezi kumdanganya Mola wake. Hivyo, mbele ya Mungu, yule mtu tu anakubalika, na dua zake tu zinapokelewa ambaye mtimani mwake hamna ufisadi, uchafu na unajisi wa aina yoyote, hamna kiburi, majivuno, majisifu, majigambo, kujifikiria kuwa mkubwa na kuwahakirisha wengine, bali kwa mahaba makali ya kweli ya Mwenyezi Mungu yaiunguzayo

dhambi, makosa yake na dhunubu zake zote ziwe zimekwisha teketea naye yu mweye kuinama mbele ya Mola wake kwa moyo uliotakasika na kifua kilichotakatika na macho yatiririshayo machozi, ndipo dua yake hukubaliwa.

Lakini Mungu wetu (Mungu Apishe mbali) si jahili, hakuna kitu kililchofichika kwake. Yuajua yaliyomo vifuani kama Alivyonena ndani ya Kurani Tukufu. Anaelewa kama ilivyoelezwa ndani ya Kurani Tukufu kwamba nani yu mcha Mungu, na nani hapana. Hujua kwamba nani ndiye adui yetu na nani rafiki. Hutambua kuwa ndani na kitu gani mna hasara yetu. Hivyo, akiwa *'Alim*, Anakubali dua zetu. Yeye (Mungu Apishe mbali) si kama yule mama mjinga ambayo mtoto akiomba kaa la moto, pengine kwa kuudhika analiweka kaa la moto mbele yake na anaanguza mkono wa mtoto. Yeye Hupenda zaidi kuliko mama, Yuapenda zaidi kuliko baba. Anapoamua kupokea maombi, Hukubali dua zile namana zinavyotufaa.

Lakini kama kitu kilichoombwa hakitunafaishi hutukatalia, na badala yake kwa fadhili na huruma yake huleta rehema yake kwa sura nyingine. Yu Mola Apendaye sana, Mwenye mahaba mengi mno. Yatulazimu tupitishie siku za maisha yetu tukiwa waja wake wenye shukurani, na tudumu kuimarisha umoja na itifaki ndani ya Jumuiya, na tuzingatie uhakika huu kwamba mema yote na *'Uwali'* wote upo chini ya mguu

Makusudio 23 Adhimu ya Ujenzi wa Baitullah

wa Khilafat Rashida. Yule anayejifahamu kuwa kitu chochote akiwa nje ya Ukhalifa, hata kama dua zake zikubaliwe, ukabalifu huu hautakuwa kwa uhalisi wake, bali utakuwa kama majaribo na mtihani. Hivyo, yapasa kudumu kumcha Mola wetu.

(Gazeti la Al-Fadhl, Rabwah, 11 Juni 1967)

⑨

**Kuimarisha Umati wa Kiislamu
Kupitia
Mtume Mtukufu^{saw}**

Hotuba ya Ijumaa, 9 Juni 1967,
Masjid Mubarak, Rabwah, Pakistan.

Ilihidiwa kwamba kwa athari za kiruhania na nguvu takatifu ya Mwongozi Mau'udi^{saw} wa ulimwengu, roho zenye bahati njema zitakuwa kwa hakika Umati wa Kiislamu, na Waarabu watakaokuwa wa kwanza kuhubiriwa naye^{saw}, uchafu wao wote utaondolewa mbali, nao wakitukuka na kutakatika watajumuika Barazani mwa Muumba wa kweli na Mmiliki wa kweli wakiwa chini ya kivuli cha maombezi ya Mtume^{saw}, kisha watakuwa waongozi wa dunia na kuimarisha mfano wa Mtume^{saw} wa Mungu kote duniani.

Basi, sawa na dua za Hadhrat Ibrahimu^{as} na bishara zake zilizokuwamo ndani ya Vitabu vya zamani, Mwenyezi Mungu Akaimarisha Umati wa Kiislamu kupitia Mtume^{saw}.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ²¹

تَحْمَدُهُ وَنُصِّحَ عَلَى رَسُولِهِ الْكَرِيمِ²²

Baada ya Shahada mbili, A'udhu na usomaji wa Sura Al-Faatiha, Hudhur^{atba} akasoma aya zifuatazo za Sura Al-Baqara, 2:129-130

رَبَّنَا وَاجْعَلْنَا مُسْلِمِينَ لَكَ وَمِنْ ذُرِّيَّتِنَا أُمَّةً مُسْلِمَةً لَكَ وَأَرِنَا مَنَاسِكَنَا وَتُبْ عَلَيْنَا إِنَّكَ أَنْتَ التَّوَّابُ الرَّحِيمُ ﴿٢٠٠﴾ رَبَّنَا وَابْعَثْ فِيهِمْ رَسُولًا مِنْهُمْ يَتْلُو عَلَيْهِمْ آيَاتِكَ وَيُعَلِّمُهُمُ الْكِتَابَ وَالْحِكْمَةَ وَيُزَكِّيهِمْ إِنَّكَ أَنْتَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿٢٠١﴾

Kisha akasema:

Nimeishawaambia hapo kabla makusudio kumi na tisa yahasuyo ujenzi wa Kaaba. Kusudio la ishirini lilielezwa katika *وَمِنْ ذُرِّيَّتِنَا أُمَّةً مُسْلِمَةً لَكَ* na iliahidiwa kwamba kwa athari za kiruhania na nguvu takatikfu ya Mwongozi Mau'udi^{saw} wa ulimwengu, roho zenye bahati njema zitakuwa kwa hakika Umati wa Kiislamu, na Waarabu watakaokuwa wa kwanza kuhubiriwa naye^{saw}, uchafu wao wote utaondolewa mbali, nao wakitukuka na kutakatika watajumuika Barazani mwa Muumba wa kweli na Mmiliki wa kweli wakiwa chini ya kivuli cha maombezi ya Mtume^{saw}, kisha watakuwa waongozi wa dunia na kuimarisha mfano wa Mtume^{saw} wa Mungu kote duniani.

Basi, sawa na dua za Hadhrat Ibrahimu^{as} na bishara zake zilizokuwamo ndani ya Vitabu vya zamani,

²¹ Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwingi wa Ukarimu.

²² Twamhimidia Yeye na kumsalia Mtume Wake mhashamu.

Mwenyezi Mungu Akaimarisha Umati wa Kiislamu kupitia Mtume^{saw} kama Asemavyo Mwenyezi Mungu ndani ya Sura Al-Hajj 22:79 ya kwamba:

وَجَاهِدُوا فِي اللَّهِ حَقَّ جِهَادِهِ ۗ هُوَ اجْتَبَاكُمْ وَمَا جَعَلَ عَلَيْكُمْ فِي الدِّينِ مِنْ حَرَجٍ ۗ وَلَمَّا ابْتَهِمُوا بِهَيْبَتِهِ لُجُومًا
سَأَلْنَا الْمُسْلِمِينَ ۖ مَنْ قَبْلَ وَفِي هَذَا لِيَكُونَ الرَّسُولُ شَهِيدًا عَلَيْكُمْ وَتَكُونُوا شُهَدَاءَ عَلَى النَّاسِ ۚ فَأَقِيبُوا
الصَّلَاةَ وَآتُوا الزَّكَاةَ وَاعْتَصِمُوا بِاللَّهِ هُوَ مَوْلَاكُمْ ۖ فَنِعْمَ الْمَوْلَىٰ وَنِعْمَ النَّصِيرُ ﴿٧٩﴾

Hapa Mwenyezi Mungu Amesema kwamba jitahidini katika njia ya Mwenyezi Mungu kwa nguvu yote na uwezo wenu wote. Na fikisheni bidii na jitihada hii mpaka ukamilifu wake. حَقَّ جِهَادِهِ , timizeni haki yake, kwani Amewafanyeni wateule na kuwajaalieni utukufu na kuwapatieni dini kamili na kuwateremshieni maamrishi bora sana na kuwajaalieni zile nguvu na uwezo uliohitajika kuyatekeleza maamrishi haya, kwa hiyo utekelezaji wa amri hizi hauwatuishi mzigo wowote. Enyi wafuasi wa Ibrahimu^{as}, Mungu Amewaiteni jina *Al-Muslimiin*, umati *Muslima*. Kwa ajili yenu jina hili lilitumika ndani ya Vitabu vya zamani, na Kurani Tukufu pia inawaiteni jina *أُمَّةٌ مُسْلِمَةٌ، الْمُسْلِمِينَ*. Jina hili ni natija ya maombi aliyoyaomba Hadhrat Ibrahimu^{as} kwamba *Umati Muslima* uimarishwe duniani (kwa kuinuliwa kwa Mbora wa Mitume) na wazao wao pia wajumuike ndani ya *Umati Muslima*. Hivyo, dua ya وَمَنْ iliyokuwa ndani ya aya zile zihusianazo na makusudio ya Kaaba, Kurani Tukufu inadai katika Sura Al-Hajj kwamba imekubaliwa, na bishara zilizotolewa ndani ya Vitabu vya zamani wakati wa kutimia kwazo

zimewadia. Mtume^{saw} amekwishatumwa, umati wa Kiislamu umeishaimarika, na imeimarika kwa sababu nguvu za ruhania na khulka na vipawa na vipaji alivyojaaliwa binadamu, wakati wa kudhihirika kwake umekwisha fika. Sasa dunia itaona jinsi binadmau anavyotumia nguvu zake katika njia ya Mola wake, na jinsi anavyofikisha vipawa vyake mpaka ukamilifu wake.

Maana ya Islam ni kuweka mbele ya Mwenyezi Mungu, mbele ya Mola wako, shingo yako kwa kutoka dhabihu, kujiweka tayari wakati wote kuiridhia radhi ya Mungu kwa kuachana na matakwa yako na utashi wako. Yaani, kisibaki chocho chako, vyote vitolewe kwa Mungu, kisha kwa kujipatia uzima mpya zipitishwe siku za maisha kwa sura ya umati bora. Hadhrat Masihi Mau'udi^{as} ananena kuhusiana na madhumuni haya:

“Na maana ya kiistilahi ya Islam ndiyo iliyoashiriwa ndani ya aya hii, yaani:

بَلَىٰ مَنْ أَسْلَمَ وَجْهَهُ لِلَّهِ وَهُوَ مُحْسِنٌ فَلَهُ أَجْرٌ عِنْدَ رَبِّهِ وَلَا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ²³

Yaani, Mwislamu ndiye yule ajitoleaye dhati yake yote kwa Mwenyezi Mungu; yaani, ajitolee wakfu kwa Mwenyezi Mungu na kwa kufuata matakwa yake na kujipatia ridhaa Yake. Kisha, aimarike katika matendo mema kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na atumie nguvu zake zote za kiutendaji katika njia Yake. Yaani, kiitikadi na kimatendo awe

²³ Sura Al-Baqara, 2:113

wa Mwenyezi Mungu tu pekee. Kiitikadi, kwa njia hii kwamba ajifahamu kuwa yeye kikweli ni kitu kilichofanyizwa kwa ajili ya kumtambua Mwenyezi Mungu na kumtii na kumpenda na kupata radhi yake. Na kimatendo, kwa njia hii kwamba kwa ajili ya Mungu tu pekee atende mema ya kweli yahusianayo na kila nguvu na uwezo aliojaaliwa na Mungu, lakini kwa furaha na shauku na kwa moyo wote, kana kwamba anauona Uso wa Mwabudiwa wake wa kweli ndani ya kioo cha utiifu wake.”

(Aina Kmaalate Islam, uk. 58)

Kusudio la ishirini na moja lilelezwa ndani ya **أَرَأَيْتُمْ مَا كُنَّا**, na ilibainishwa kwamba Nabii yule aliyeahidiwa atateremkiwa na sheria itakayokuwa yenye kutimiza mahitaji yote ya kweli ya tabia ya asili ya binadamu, kila kipaji kitafaidika kwayo, na kila tabia ya asili itapata hisa yake sawa na uwezo wake, na ndani yake yatakuwepo, na yatadumu kuwepo, mafundisho kuafikiana na hali ya kila zama, sawa na hali ya kila kaumu na uwezo wa kila mmoja.

Neno **أَلْهَيْتُكَ** ni wingi wa **أَلْهَيْتُكَ** na **أَلْهَيْتُكَ**, na lamaanisha kujitenga na mambo ya kidunia, kuabudu na kila tendo lifanywalo kwa kujipatia ukaribu na Mungu.

Hapa Mwenyezi Mungu Hakusema **أَرَأَيْتُمْ مَا كُنَّا**, yaani tufundishe njia kamilifu za ibada, bali kasema **أَرَأَيْتُمْ مَا كُنَّا**, yaani Utufundishe zile njia kamilifu zilizoafikiana na hali zetu. Na zingatieni kwamba ni sheria ya Kiislamu pekee

ambambo mmewekwa nafasi hii ambayo haimo ndani ya sheria za hapo kabla. Pindi umati wa Kiislamu ulipokwisha imatika na sheria ya Kurani Tukufu ilipoishawashukia, ndipo dua ya Hadhrat Ibrahim^{as} ya اٰرْتَا مَنَّا سَكَّنَا ikakubaliwa. Basi, ndani ya اٰرْتَا مَنَّا سَكَّنَا imefundishwa dua hii kwamba katika kutimiza haki za Mungu na haki za watu, Utujaalie uwezo wa kuchagua amali bora zaidi kuafikiana na wakati na mahali. Kurani Tukufu imesisitiza sana kwamba mafundisho ya Kurani Tukufu huwa na jiha tofauti. Yaani, kila hukumu iliyotolewa na Kurani, ina jiha mbalimbali, hivyo ile jiha inayoafikiana na wakati na mahali na uwezo wenu, basi chagueni kutenda sawasawa na jiha hiyo. Hadhrat Masihi Mau'udi^{as} amesema kwamba baadhi ya watu wanajibidiisha katika mambo ya ibada zaidi sana ya uwezo wao; hufunga saumu kwa siku nyingi sana, au wanalala kidogo kabisa, ilhali miili yao haiwezi kuyavumilia matendo haya. Matokeo yake siyo kwamba wanamkurubia Mwenyezi Mungu, bali huwa wanarukuwa na akili au wanashikwa na baadhi ya maradhi, baadhi yao wanapatwa na kifua kikuu au magonjwa mengine.

Dua iliyofundihwa sehemu hii ni اٰرْتَا مَنَّا سَكَّنَا , yaani Utufundishe njia zifaazo za kutekeleza ibada zote zinazopaswa za kutimiza haki za Mungu na haki za watu, kuafikiana na kila kaumu sawa na kila zama, na tena kuafikiana na kila mtu wa kila kaumu na kila zama,

ili tuingwe na kila aina ya maradhi, udhaifu, utelezi na kuvunjika moyo, na tujipatie ukaribu Wako.

Kurani Tukufu imekazania kwa nguvu na kwa wingi kuchagua *ahsan*, yaani jiha iliyo bora sana, katika kutenda amali. Matalani, Alisema جَادِلْهُمْ بِأَلَّتِي هِيَ أَحْسَنُ (Sura An-Nahl 16:126), yaani wakati wa kubadilishana mawazo na mtu mwaweza kushika jiha kadhaa tofauti, basi mshike jiha iliyo bora zaidi katika hizo. Kuna mtu anayesikiliza akiambiwa kwa huba, msimtishe katu. Kuna wakati ambapo mpinzani anafikiri kwamba nikimchokoza ili alete ufisadi, hao watahasirika nasi tutafaidika, wakati huo ni faradhi ya Mwahmadiyya kuwa sawa na hukumu ya Kurani Tukufu ajitahidi sana kuimarisha amani na ashike njia bora iliyoamrisha ndani ya agizo جَادِلْهُمْ بِأَلَّتِي هِيَ أَحْسَنُ, ili amani isipate kuvunjika. Katika hukumu nyingi sana Mwenyezi Mungu Ameashiria kwenye jambo hili kwamba njia kadhaa zaweza kushikwa kutekeleza amri fulani, basi nyiye mjichagulie njia ile iliyo bora fika. Mwenyezi Mungu Ananena وَاتَّبِعُوا أَحْسَنَ مَا أُنزِلَ إِلَيْكُمْ (Sura Az-Zumar, 36:56) , yaani, Mola wenu anayetaka utunzaji wenu Ameteremsha kwa matakwa ya sifa yake hii, sheria yenye jiha tofauti. Na utunzaji wa kila mtu, kila mmoja na kila kaumu, unahitaji kwamba uweze kutekelezwa kwa jiha tofauti. Hivyo, kila jiha imejumuiika ndani yake. Sheria hii imeteremshwa kutoka kwa Mola Mkarimu, kwa hiyo imehifadhiwa mpaka Kiama. Shikeni njia iliyo bora zaidi. Tekelezeni kila hukumu kwa njia bora sana

inayoafikiana na hali yenu, ifaayo hali ya zama, ambayo isababishe nguvu zenu na vipawa vyenu kuweza kupata ukuaji na utunzaji sahihi.

Kadhalika, Mwenyezi Mungu Anasema katika aya nyingine **فَبَشِّرْ عِبَادِ الَّذِينَ يَسْتَبِعُونَ الْقَوْلَ فَيَتَّبِعُونَ أَحْسَنَهُ** , yaani, wape habari njema waja wangu wanaosikia (الْقَوْلَ) sheria hii bora **فَيَتَّبِعُونَ أَحْسَنَهُ** na wanaifuata iliyo bora zaidi kati ya hukumu wanazosomewa, kwamba **أُولَئِكَ الَّذِينَ هَدَى اللَّهُ** , yaani Mwenyezi Mungu Atawaandaalia njia za mwongozo wao, na machoni mwa Mwenyezi Mungu hao ndio **أُولُوا الْأَلْبَابِ** (Sura Az-Zumar 39:18-19) — watakaonekana ndio wenye lubu. Ndani yake imeelezwa kwamba Mwenyezi Mungu Amemwingiza mtu kama huyo ndani ya wenye lubu na kumjaalia akili ili aitumie katika kutekeleza hukumu za sheria ya Kiislamu, na aitumie akili yake na atambue hali na mahali. Mathalani, akibadilishana mawazo na mtu mwingine atambue saikolojia yake na aamue kwa busara yake kwamba nikiongea naye kwa njia fulani, maneno yangu yatamwathiri yeye.

Basi, sehemu hii waja wa Mungu kwa wazi sana wametolewa habari njema; hawakutolewa wale wanaosikia Kurani Tukufu lakini hawatumii akili yao na badala ya iliyo bora zaidi wanachagua jiha nyingine. Hivyo, Mwenyezi Mungu Hawatolei watu kama hao habari njema ndani ya Kurani Tukufu, yaani Hawapi habari njema ya mwisho wao mwema. Hivyo, hapa maana moja itakuwa kwamba waja wangu wale

wanaosikiliza *Al-Kaul* na katika hii wanaifuata iliyo bora fika, hao ndio ambao mwisho wao utakuwa mwema; wasiofanya hivyo, mwisho wao hautakuwa mwema.

Kusudio la ishirini na mbili lilielezwa ndani ya **ثُبَّ عَلَيْنَا** . Ndani mwake mmeashiriwa kwamba sheria ya mwisho itakayoteremka hapa, itakuwa na uhusiano wa keto na Mola *Tawwaab*, na wafuasi wake watatambua uhakika huu wa msingi kwamba pasipo toba na kuomba ghofira haiwezekani kupata maarifa ya Mungu na radhi Yake. Hivyo, watakapotoa dhabihu mara kwa mara katika njia Yake, hapo watajipatia nguvu toka Kwake kwa kuomba ghofira mara kwa mara, nao watakuwa pia wenye kurejea Kwake pamoja na kutubu; hawatazifahamu kwamba bidii na jitihada na dhabihu zao hazina kipengo au makosa ndani mwake.

Maana ya **قَبِلَ تَوْبَتَهُ مِنْهُ** , yaani Mwenyezi Mungu Amekubali toba ya mtu aliyetubu. Sehemu hii dua yenyewe ni **وَتُبَّ عَلَيْنَا** na imelezwa kwamba uhakika ule uliomo ndani mwa toba na *istighfaar*, umati huo utaitambua barabara maana yake ya kweli, nao watajaaliwa sheria itakayobainisha kwa uwazi mambo hayo. Ndani ya sheria na istilahi ya Kiislamu mambo manne yanakuwepo:

- (1) Kuachana na dhambi. Mathalan, yule aliyezoea kuongopa, yeye anafanya dhambi. Kuachana na kusema uongo huitwa toba. Hii ndiyo jiha yake moja.

- (2) Kujuta baada ya kufanya dhambi. Kila mtu hasemi uongo kila wakati. Lakini, mtu fulani kwa muda mrefu hakusema uongo, kwa mfano, hakusema uongo kwa miezi sita; ingawa aliacha dhambi (kwa miezi sita), lakini hii siyo toba, kwani zaidi ya kuachana na dhambi hakuna budi kujuta pia juu ya dhambi kwa kutubu.
- (3) Aazimie kwamba sitarudia dhambi hii; awe na nia imara ya kuachana na hii dhambi.
- (4) Kuna baadhi ya dhambi zinazoweza kurekebishwa. Mathalani, kama amejitwalia bila haki rupia 100 za mtu fulani, hapo toba haimaanishi kwamba ametubu tangu sasa kutwaa mali ya wengine bila haki, kwa majuto na kwa nia ya kutorudia dhambi hii, lakini juu ya kuwa na uwezo hamrudishii zile rupia 100 mwenye haki, ilhali si maskini kiasi cha kurudisha zile rupia mia, hapo pia toba yake sio toba kabisa.

Kwa kutekeleza mambo hayo manne yatulazimu tupate nguvu kutoka kwa Mwumbaji wetu. Kwani, kuiacha dhambi haiwezekani pasipo kupata uwezo toka kwa Mwenyezi Mungu. Kuzalika kwa hisia ya majuto baada ya kutenda dhambi haiwezekani bila kujaaliwa na Mungu. Ama azma, basi binadmu anawezaje kudai kwamba pasipo kupewa nguvu na Mwenyezi Mungu, bila kupata uwezo toka kwa Mwenyezi Mungu, naweza kuazimia, kufunga nia imara, kwamba sitatenda dhambi

tena. Hivyo, kwa ajili hii pia iko haja ya kupata uwezo toka kwa Mwenyezi Mungu; na kiasi anachoweza kujirekebisha, kwa ajili yake pia kunahitajikia kupata nguvu na uwezo kutoka kwa Mwenyezi Mungu.

Hivyo, nguvu hizi na uwezo huu wote unapatikana kwa njia ya *istighfaar*. Mja wa Mungu anamfahamu Mola wake kuwa chanzo cha nguvu zote na uwezo wote. Yeye hakuti nguvu yoyote wala uwezo ndani mwake wala hauoni. Hivyo, kabla hajaanza kufanya kila kazi, yeye hurejea kwa Mola wake na kuomba ghofira na husema kwa Mola wake: Ewe Mungu Uliye chemchem ya uwezo wote na chanzo cha nguvu zote, nijalie nguvu na uwezo kwamba niyaachilie mbali maovu na kuimarika kikweli katika mema. Basi, hii yamaanisha kwamba *istighfaar* inatangulia na toba inaifuata. Toba haiwezekani pasipo *istighfaar*. Hadhrat Masihi Mau'udi^{as} ametia mwanga mwingi sana juu ya madhumuni hii. Hadhrat Masihi Mau'udi^{as} anasema:

“*Istighfaar* na toba ni mambo mawili. Kwa sababu fulani *Istighfaar* inaitangulia toba, kwani *Istighfaar* ni msaada na uwezo anaopata mtu toka kwa Mungu, na toba ndiyo kuima imara juu ya miguu. Ni suna ya Mungu ya kuwa mtu atakapomwomba Mwenyezi Mungu msaada, Mwenyezi Mungu Atampa nguvu, na mtu ataima juu ya miguu yake na ndani mwake mtazalika nguvu ya kutenda mema, iitwayo **تَوْبُوا إِلَيْهِ**. Hivyo, utaratibu wa kiasili

ndio huu huu. Ilimuradi, ndani yake kuna njia waliyowekewa walio safarini kwenda kumlaki Mungu kwamba katika kila hali *Saalik* – amwendaye Mungu kumlaki – amwombe Mungu msaada. *Saalik* asipojaaliwa nguvu na Mwenyezi Mungu, ataweza kufanya nini? Uwezo wa kutubu hujaaliwa baada ya *istighfaar*. Kama hakuna *istighfaar*, basi kumbukeni kwamba nguvu ya toba inajifia. Kama mkifanya *istighfaar* hivyo, kisha mtatubu, basi natija itakuwa hii **يُبْتَعَلَمُ مَتَاعًا حَسَنًا إِلَىٰ أَجَلٍ مُّسَمًّى**.²⁴ Suna ya Mungu inaendelea hivi kwamba mkifanya *istighfaar* na toba, mtapata daraja za juu. Kwa kila mtu kuna duara ambalo ndani yake anapata daraja za maendeleo.”

(Malfuudhaat, J. 2, uk. 68-69, Al-Hakam, J. 6, Na. 26 la tarehe 24 Julai 1902, uk. 10)

Yeye^{as} amesema kwamba mkikaa ndani ya duara lenu jipatieni darja za juu za ruhania kiasi mnachoweza kwa njia ya *istighfaar* na toba.

Sehemu nyingine, Hadhrat Masihi Mau‘udi^{as} anasema:

“Kwa utondoti huu ni dhahiri kwamba maana ya kweli ya kuomba *istighfaar* ni kwamba *istighfaar* haiwi kwa sababu ya haki fulani kupotea, bali ni kwa utashi huu kwamba haki yoyote isipotee. Na tabia ya asili ya binadamu ikijiona dhaifu, kitabia

²⁴ Huud 11:4

inamwomba Mungu ajaaliwe uwezo... Na jambo hilo laashiria kwenye hii kwamba mtu hawezi kufikia daraja ya juu ya kutokuweza kufanya dhambi na daraja ya maombezi mpaka wakati wote aendelee kuomba dua kuzuia udhaifu wake na kuwaokoa wengine katika sumu ya dhambi, na kwa maombi ya unyenyekevu kuvuta uwezo toka kwa Mwenyezi Mungu, kisha anapenda kuwa wengine nao wapate hisa ya uwezo huu, ambao wanaunganika naye kiimani. Mtu maasumu anahitaji kuomba uwezo toka kwa Mungu kwani tabia ya asili ya binadmau haina sifa kamilifu ndani mwake binafsi, bali kila wakati hupata ukamilifu toka kwa Mungu; wala haina nguvu ndani mwake binafsi, bali hupata nguvu kila wakati toka kwa Mungu, wala haina nuru kamili ndani ya dhati yake, bali nuru inaiteremkia toka kwa Mungu. Ndani yake kuna siri hii kwamba tabia kamili ya asili hujaaliwa nguvu ya kuvuta tu ili iweze kuvuta kwake nguvu ya juu. Lakini, hazina ya nguvu ni Dhati ya Mungu pekee; katika hazina hii hii malaika pia hujipatia nguvu na mtu mkamilifu pia huvuta nguvu ya kutotenda dhambi na fadhili Yake kutoka katika chemchem hii ya nguvu kupitia mfereji wa ibada halisi... Hivyo, *istighfaar* ni nini? Hii ndiyo kama kifaa ambacho kupitia hicho nguvu huteremka. Siri yote ya Tauhidi hufungamana na kanuni hii kwamba sifa ya

kutoweza kutenda dhambi isichukuliwe kuwa ni milki ya kudumu ya binadamu; bali kwa kujipatia sifa hii, Mungu pekee Afahimwe kuwa ni chemchemi.

(Review of Religions, Kiurdu, J. 1, uk. 189-190)

Mtu anapokwisha pata ulinzi wa Mwenyezi Mungu, anapoisha pata nguvu toka kwa Mwenyezi Mungu, ndipo hupata uwezo wa toba, na ndipo toba yake hukubaliwa mbele ya Mwenyezi Mungu. Kwa hiyo anasema Hadhrat Masihi Mau'udi^{as}:

“Basi, amkeni, mkatubu na kumridhisha Bwana Wenu kwa matendo mema. Na kumbukeni kuwa adhabu ya makosa ya itikadi itatolewa baada ya kufa, na uamuzi juu ya kuwa Mhindu, Mkristo au Mwislamu utatolewa siku ya Kiama. Lakini, mtu anayepita kiasi katika dhuluma, uhalifu, ufasiki na upujufu, huadhibiwa hapa hapa, basi yeye hawezi katu kuikimbia adhabu ya Mungu. Hivyo, Mridhisheni haraka Mungu wenu, na kabla ya kuja siku ile... fanyeni suluhu na Mungu. Yu Mkarimu, kwa toba ya mara moja iliyojaa unyenyekevu mkubwa, Yeye huweza kusamehe madhambi ya miaka sabini. Msiseme kuwa toba haikubaliwi. Kumbukeni, kamwe hamwezi kusalimika kwa matendo yenu, bali daima fadhili ya Mungu ndiyo husalimisha siyo matendo. Ewe Mungu Mkarimu na Mrehelevu, tujalie sote fadhili

Makusudio 23 Adhimu ya Ujenzi wa Baitullah

zako, kwani tu watumishi wako na tumeangukia kizingiti chako. Amin.”

(Hotuba ya Lahore, uk. 38)

Leo, kwa sababu ya joto nimesumbuka, humu msikitini pia kuna joto kali. Ndugu wataudhika kwa hotuba ndefu, hivyo leo naishia hapa. Madhumuni iliyobaki nitaeleza katika hotuba ijayo kwa kuwezesha na Mungu na kwa fadhili Yake.

(Gazeti la Al-Fadhil, Rabwah, 18 Juni 1967)

**Makusudio Yote
ya Ujenzi wa Baitullah
Yalitimia kwa Kutumwa
kwa Mtume Mtukufu^{saw}**

Hotuba ya Ijumaa, 16 Juni 1967,
Masjid Mubarak, Rabwah, Pakistan.

“Mungu Anataka kuwa wazee wa kaumu pia na vilevile vijana wa kaumu, wanaume wa kaumu pia na kina mama wa kaumu vilevile waanze kufahamu hekima ya Mungu inayohusiana na msingi wa Kaaba ili mbele ya Mwenyezi Mungu wawe wenye lubu, na waweze kufahamu sauti yake na hukumu zake na hekima za hukumu, nao waingie ndani ya kundi la watakatifu wanaojaaliwa saa zote fadhili za Mwenyezi Mungu.”

Baada ya Shahada mbili, A'udhu na usomaji wa Sura Al-Faatiha, alisema:

Jana kutwa niliendelea kushikwa na maumivu makali ya kichwa, hata sasa nahisi udhaifu mwingi, lakini napenda kwamba hotuba nilizoanza kutoa mfululizo juu ya makusudio 23 (yaihusuyo Baitullah) niendeleo kutoa, na shabaha na kusudio la mwisho lililobaki nieleze kulihusu hili ndani ya hotuba ya leo.

Kusudio la ishirini na tatu la ujenzi wa Baitullah lilielezwa ndani ya رَبَّنَا وَابْعَثْ فِيهِمْ رَسُولًا مِنْهُمْ يَتْلُو عَلَيْهِمْ آيَاتِكَ وَيُعَلِّمُهُمُ الْكِتَابَ وَالْحِكْمَةَ وَيُزَكِّيهِمْ إِنَّكَ أَنْتَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿130﴾ (Sura Al-Baqara, 2:130). Na ilikuwa imeelezwa ndani ya aya hii kwamba Nabii mmoja atainuliwa atakayebaki hai hadi Kiama, na kwa baraka zake kwa sababu ya kutoa manufaa ya ruhania hatafikiwa na mauti, atajaaliwa kuishi milele hata milele; naye atapewa sheria ya kudumu, haitatanguka kwani hiyo itakuwa ni Al-Kitab (Sheria kamilifu timilifu); na utazalishwa umati utakaoimarika katika busara, utafahamishwa hekima na kupewa hoja na utahusiana na Mungu Aliye hai na Nabii aliye hai na Sheria iliyo hai.

Kusudio hili nalo lilitimia kwa kuinuliwa Nabii Mtukufu^{saw} kama Kurani Tukufu yenyewe ilivyodai,

²⁵ Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwingi wa Ukarimu.

²⁶ Twamhimidia Yeye na kumsalia Mtume Wake mhashamu.

nami nitatia mwanga juu yake hivi sasa. Hadhrat Masihi Mau'udi^{as} anasema:

“Tazameni, Ibrahimu^{as} pia aliomba dua moja kwamba awepo nabii mmoja kutoka katika wazao wake ndani ya Bara Arabu. Je dua hii ilikubaliwa wakati uo huo? Baada ya Ibrahimu^{as}, mtu yeyote hata hakuwaza kwamba dua hii ilileta athari gani. Lakini kwa sura ya kutumwa kwa Mtume^{saw} wa Mungu dua hii ilitimia, na tena kwa shani kubwa ilioje ilitimia.”

(Malfudhaat, J. 4, uk. 420; Al-Hakam, J. 7, Na. 8 la tarehe 28 Februari 1903, uk. 2)

Ndani ya aya hii tukufu, mambo matano yametajwa:

Mosi, kudhihiri kwa mja mkamilifu.

Pili, mfululizo usiokoma wa ishara bayana.

La tatu, kuteremka kwa sheria kamili na kudumu kwake mpaka Kiama.

La nne, kueleza hekima ya hukumu za sheria, na

La tano, imeelezwa kwamba kimatokeo jumuiya moja ya watukufu itaendelea kuzaliwa mpaka Kiama.

Ndani ya sehemu nyingi za Kurani Tukufu imedaiwa kwamba Nabii Mtukufu^{saw} ametumwa kama matokeo ya dua za Ibrahimu^{as}. Wakati huu ningependa kuweka

mbele ya marafiki zangu aya chache za Sura An-Naml 16:92-94. Mwenyezi Mungu Anasema:

إِنَّمَا أُمِرْتُ أَنْ أَعْبُدَ رَبَّ هَذِهِ الْبَلَدِ الَّذِي حَرَّمَهَا وَلَهُ كُلُّ شَيْءٍ وَأُمرْتُ أَنْ أَكُونَ مِنَ الْمُسْلِمِينَ ﴿٩٢﴾ وَأَنْ
اتْلُوا الْقُرْآنَ فَمِنْ أُمَّتِي إِنَّهَا لَمَهْتَدِي لِنَفْسِهِ ۗ وَمَنْ ضَلَّ فَقُلْ إِنَّمَا أَنَا مِنَ الْمُنذِرِينَ ﴿٩٣﴾ وَقُلِ الْحَمْدُ لِلَّهِ
سَيُرِيكُمْ آيَاتِهِ فَتَعْرِفُونَهَا ۗ وَمَا رَبُّكَ بِغَافِلٍ عَمَّا تَعْمَلُونَ ﴿٩٤﴾

Tuchunguzapo ile aya ya kwanza (yaani رَبَّنَا وَابْعَثْ فِيهِمْ رَسُولًا) na kuzingatia muktadha wake na kudhihirisha kiwakilishi nomino, twafahamu maana hii kwamba muradi wa dua رَبَّنَا وَابْعَثْ فِيهِمْ رَسُولًا مِنْهُمْ ya Ibrahimu^{as} na Ismaili^{as} ni huu kwamba: Ewe Mola wa Ibrahimu^{as} na Ismaili^{as} ambao kupitia hao Umejengesha upya Kaaba na kutangaza utukufu wa Nyumba Yako yenye heshima, Uinue kutoka miongoni mwa wakazi wa Nyumba hii tukufu, Roho mmoja adhimu na kumtunza yeye. Umfanye mchaguliwa na mteule, na kumjalila kilele cha ukaribu wako, na kwa kumpa sheria kamilifu timilifu umtume duniani akiwa Mtume Wako na Mwongozi akawaite binadamu kwenye Allah, Mola wa walimwengu na kuwaimarisha juu ya Tauhidi halisi. Mwenyezi Mungu Alikubali dua hii, na kwa kinywa cha Nabii Mtukufu^{saw} akatangazisha duniani:

إِنَّمَا أُمِرْتُ أَنْ أَعْبُدَ رَبَّ هَذِهِ الْبَلَدِ الَّذِي حَرَّمَهَا

Yaani, dua ya Ibrahimu^{as} na Ismaili^{as} ilipokelewa na Mola wa walimwengu, na Ameniamuru kwamba mimi kwa kufikisha kwenye upeo wa mwisho ibada ya Mola wa mji huu mtukufu, Baitullah hii, nikidhihiri kwa sura ya mja mkamilifu, niwaite binadamu waje kwa Mola wa

Kaaba, Mola wa mji mtukufu – kwa Yule Mwenye nguvu kamilifu (وَلَهُ كُلُّ شَيْءٍ) , na Mwenye Sifa zote njema, Ambaye Hufanya Apendavyo; nguvu yoyote ya dunia haiwezi kuthubutu mbele yake. Nami nimeamuriwa kwamba nikiingia katika kundi la *Al-Muslimuun*, niweke mbele ya dunia mfano kamili wa Mwislamu. Almuradi, huko Akawajalia Ibrahimu^{as} na wazao wake kuomba dua hii na Kurani Tukufu iliihifadhi, na huku Akatangazisha kwa kinywa cha Nabii Mtukufu ^{saw} kwamba nimeamuriwa kumwabudu Mola wa mji huu mtukufu, nami kama natija ya maombi ya Ibrahimu^{as} nimeima leo kwa kuongoza dunia.

Jambo la pili, la tatu na la nne, yaliyoelezwa hapa, haya yote yalikuwa yametajwa ndani ya *يَتْلُوا عَلَيْهِمْ آيَاتِكَ وَيُعَلِّمُهُمُ الْكِتَابَ وَالْحِكْمَةَ*, yaani atadhihiri mja mmoja mkamilifu, na pamoja na kudhihiri kwake dunia itanza kushuhudia mfululizo wa ishara bayana usiokoma. Yeye atatoa mafundiho ya *Al-Kitab* – Kitabu kamili – na hukumu zile atakazoeleza kutoka ndani ya Kitabu kamili, atafafanua pamoja nazo hekima zake pia. Tazameni, ndani ya *وَأَنْ أَتْلُوا الْقُرْآنَ* mambo haya matatu yameelezwa: Kueleza aya, kufundisha Kitabu na kutia mwanga juu ya hekima na sababu zake. Mambo haya matatu yaliyomo ndani ya dua hii yamo katika *أَنْ أَتْلُوا الْقُرْآنَ* , kwani katika lugha ya Kurani Tukufu, neno *Tilawat* latumika pia kueleza aya, kujifunza hizi na kuwafundisha hizi watu wengine na kupokea athari kutoka hizi na kuishi maisha sawa nazo, na pia hutumika kusoma Kitabu na hekima yake na

kuwasomea wengine na kukitekeleza na kutekelezesha. Ndani ya *Mufradaat Raghib*, maana ya neno *Tilawat* imeelezwa hivi:

الْتِلَاوَةُ تَخْتَصُّ بِاتِّبَاعِ كُتُبِ اللَّهِ الْمُنَزَّلَةِ تَارَةً بِالْقِرَاءَةِ وَتَارَةً بِالِازْتِسَامِ لَهَا فِيهَا مِنْ أَمْرِ وَعَنْهِي
وَوَتَرْتِيبٍ وَتَرْهِيْبٍ

Yaani, *Tilawat* ni neno mahususi kumaanisha kwamba vifuatwe Vitabu vya Allah viteremkavyo toka mbinguni. Na kuvifuata huku huwa kwa njia mbili: Kwa kiraa na kwa kutekeleza hukumu (kwa kukubali hukumu; kutekeleza maamrishi na makatazo yaliyomo humo pia huingia katika *Tilawat*), na kupokea athari ambazo kitabu kile kinataka kutia, yaani kuathirika na hekima zile zilizoelezwa, hii pia imo ndani ya maana ya *Tilawat*. Mwenyezi Mungu Anasema ndani ya Kurani Tukufu katika Sura Al-Anfaal 8:3 ya kwamba:

وَإِذَا أَنْزَلْنَا عَلَيْهِمْ آيَاتِنَا زَادَتْهُمْ إِيمَانًا

Yaani, waaminio ni wale ambao wasomewapo aya za Kimbingu, huzidi imani yao. Hapa nawaambia kwamba kuzihusu aya pia neno *Tilawat* limetumika katika lugha ya Kurani. Kadhalika kwa kusoma Kitabu na kuyatekeleza yaliyoelezwa ndani yake na kuweka mbele ya dunia mfano wetu pia neno *Tilawat* limetumika, kama Asemavyo Mwenyezi Mungu ndani ya Kurani Tukufu katika Sura Al-Ankabuut 26:46 *أَنْتُمْ مَا أَوْجَى إِلَيْكَ مِنَ الْكِتَابِ* kwamba soma kutoka katika Kitabu cha Mola wako wahyi ambao wewe unaendelea kuteremshiwa (wakati huo wahyi ulikwa unaendelea kuteremka). Yaani, uutekeleze

na uusome. (Mtu asomapo chochote, husoma kuwasikilizisha wengine pia, na vile vile kwa ajili yake mwenyewe. Na kwa kuwa Nabii Mtukufu^{saw} ndiye wa kwanza kuambiwa, hivyo maana yake ni kwamba wewe kwa kuutekeleza uwe mfano ufaao kufuatwa na watu hawa). Kuhusiana na Manabii^{as}, Kurani Tukufu daima imesema kuwa kila mmoja kati yao alidai na akatangaza kuwa mimi ndimi **أَوَّلُ الْمُسْلِمِينَ** , yaani mimi ndimi wa kwanza kutekeleza maamrisha na makatazo haya, naweka shingo yangu chini ya hukumu ya Mungu na kwa njia hii naweka mbele yenu mfano kama Kiongozi. Sisemi kuwa njia hii inafikisha kwa Mungu basi muifuate; mimi nasema kwamba njia hii yafikisha kwa Mungu, nami naifuata, nifuateni nyuma yangu ili nyinyi nanyi mumfikie Mungu. Hivyo, katika maana ya lugha yenyewe, sawa na *Mufradaat Raghīb*, kuifuata kielimu na kimatendo ndiyo imo ndani ya maana ya *Tilawat*: kufuata kielimu kwa kuwaambia wengine mambo ya hekima, na kufuata kimatendo ndiyo kwa kuishi maisha sawa na mambo haya. Ilimuradi, sehemu hii Mwenyezi Mungu Alimfanya Nabii Mtukufu^{saw} aseme kwa kinywa chake **وَأَنْ أَتْلُوَ الْقُرْآنَ** , Mwenyezi Mungu Ameniamuru kwamba niwasomeeni Kurani. Neno Kurani, imelitumia Kurani yenyewe kwa ajili ya aya. Ikasema **بَلْ هُوَ آيَاتٌ بَيِّنَاتٌ** (Sura Al-‘Ankabuut, 29:50) yaani hii – Kurani – ni aya zilizo bayana. Kwa hiyo, **أَنْ أَتْلُوَ الْقُرْآنَ** itamaanisha kwamba Mungu Ameniamuru kwamba niweke mbele yenu sheria kamili kwa sura ya Kitabu pia na vilevile kwa sura ya **أَوَّلُ**

السُّلَيْمِينَ . Kwani ilipoulizwa kuhusu khulka zake,^{saw}, akasema Hadhrat Aisha^{ra}: Someni Kurani (كَانَ خُلُقُهُ الْقُرْآنَ).

Basi, dua ilikuwa hii kwamba يَتْلُوا عَلَيْهِمُ آيَاتِكَ . Yule Nabii aendelee kuweka mbele ya dunia aya bayana. Nabii Mtukufu^{saw} alisema kuwa dua hiyo ilikubalika, nami kwa amri ya Mungu أَتَلُوا الْقُرْآنَ naziweka aya bayana za Kurani Tukufu mbele ya dunia.

Tena kulikuwa na dua hii يَعِيبُهُمُ الْكِتَابُ , na Nabii Mtukufu^{saw} aksema: أَتَلُوا الْقُرْآنَ , mimi naweka mbele ya dunia sheria kamili kwa sababu ya kukubaliwa kwa dua hiyo.

Kisha, ilikuwa dua hii kwamba yeye afundishe mambo ya hekima, na Nabii Mtukufu^{saw} akasema أَتَلُوا الْقُرْآنَ naweke mbele ya dunia Kurani Tukufu hii liyojaa hekima na ndiyo hekima kamili. Hivyo, kama natija ya ukabalifu wa dua hizi tatu, Mwenyezi Mungu Alitamkisha kinywani mwa Nabii Mtukufu^{saw} sentesi ya maneno mawili na kuashiria kwenye mambo yote matatu, na lugha pia inasadikisha maana hizi.

Jambo la nne lilikuwa ni يُرَكِّبُهُمْ , yeye atawatakasa. Kuhusiana na يُرَكِّبُهُمْ , Nabii Mtukufu^{saw} akasema ndani ya aya hizi, فَمِنَ اهْتَدَىٰ فَإِنَّمَا يَهْتَدِي لِنَفْسِهِ (Yunus 10:109) . Yaani, aliweka mbele ya dunia kilichozidi kuliko maana ya dua ya Ibrahimu^{as}. Ndani ya فَمِنَ اهْتَدَىٰ alitangaza kwamba nimewaleteeni njia zote zenye kutakasa nafsi, kwa hiyo dua ya يُرَكِّبُهُمْ imetimia. Lakini nawaambia kwamba utakaso wenu hautafanywa kwa kutumia nguvu. Hizi ni

‘nyenzo’ za kutakasa nafsi, nami naziweka hizi mbele yenu.

فَمِنْ اهْتَدَىٰ فَأَتَمَّا يَهْتَدَىٰ لِنَفْسِهِ

Sasa mtatakiwa kujitakasa nafsi zenu kwa kujitahidi wenyewe na kutoa dhabihu na kutoa uhai wenu katika njia ya Mungu kwa kudhihirisha uhalisi wa nia yenu. ‘Nyenzo’ nimekwishaleta mimi, lakini utakaso wa nafsi hautaingizwa ndani yenu kwa kutumia nguvu, bali upo uhuru wa dhamiri. Na zipo njia za kujitakasa; kwa kuzitumia hizi, kufaidika nazo, na kimatokeo kupata ukaribu wa Mwenyezi Mungu na kupatikana kwa usafi na utakaso, kwa ajili yake mtatakwa kujibidiisha; hakuna mwingine au nguvu ya juu itakayowatakaseni kwa kuwalazimisheni, wala haiwezi. Basi, فَمِنْ اهْتَدَىٰ فَأَتَمَّا يَهْتَدَىٰ لِنَفْسِهِ , ‘nyenzo’ za mwongozo zimefika tayari, njia za kujitakasa zimekuja. Yule mtu ambaye, akifaidika na njia hizi, anapata kujitafutia njia ya mwongozo, huyo anajinufaisha nafsi yake. (Yunus 10:109), وَ مَنْ صَلَّىٰ فَأَتَمَّا يَضِلُّ عَلَيْهَا , na yule asiyejinufaisha na njia za kujitakasa nafsi, wala haelekei kwenye njia za mwongozo, badala ya njia za mwongozo anazifuata njia za upotevu, na badala ya Mola wake Aliyemuumba anaelekea kwa shetani na kumfuata yeye, basi namuambia huyo kwamba hutatumiwa nguvu kukuzuia kupotea huku. (Sura An-Naml 16:93), اِنَّمَا اَنَا مِنَ الْمُنذِرِينَ , mimi ni mwonyaji miongoni mwa mitume waonyaji. Ni sawa kuwa mimi ni mkuu na mbora kuliko wote, nimetukuka kuliko wote, niko karibu zaidi na

Mwenyezi Mungu, lakini mimi ni mwonyaji tu. Mimi sitawalazimisheni. Kazi yangu si kuwaondoeni kwa nguvu katika njia za upotevu wala kuwaleteni kwenye njia za mwongozo kwa kutumia nguvu. **وَقُلِ الْحَمْدُ لِلَّهِ**, sema kwamba sifa zote njema ni za Mungu Aliyeleta ndani ya Islam ishara bayana na Kitabu na hekima na kuzalisha njia za utakaso. Na Akatuma Mtume^{saw} aliyeweka mbele ya dunia mfano kamili ambao kwa kuufuata mtu hupata huba ya Mola wake na kurithi neema zake. **الْحَمْدُ لِلَّهِ**, Yuastahiki sifa zote njema Yule Mungu Ambaye **سَيُرِيكُمْ آيَاتِهِ** Atadhihirisha tena ishara zake bayana na elimu za Kurani Tukufu katika zama za mwibuko wa Islam mara ya pili, na kufafanua hekima zake na kuzalisha sababu zitakazoirahisishia dunia kuzifuata njia za dini; na watu kwa kuchangamka watatoa dhabihu kwa ajili ya Mola wao, na katika wakati wa kukamilisha uenezi wa dini, yaani katika zama za mwibuko wa pili wa Islam, ulimwengu utakuja mapajani mwa Muhammad^{saw} Mtume wa Mungu, chini ya kivuli chake^{saw}. Wakati ule ahadi zile za Mwenyezi Mungu pia zitatimia alzoziahidi mwanzoni kwamba binadmu wote watafanywa kuwa umati mmoja mpendwa wa Allah.

Almuradi, ndani ya aya hii tukufu, yaani **رَبَّنَا وَابْعَثْ فِيهِمْ رَسُولًا** , mambo matano yalikuwa yameelezwa. Shabaha moja na dua ilikuwa kwamba miongoni mwao ainuliwe mtume mmoja ambaye awe na sifa hizi zilizoelezwa sehemu hii, na awe mfano mwema kamili ambaye kwa njia yake baraka za kiruhania zidumu kuendelea. Pili,

dunia ipate mfululizo usio na kikomo wa ishara bayana. La tatu, kuwe na sheria kamili isiyoweza kuingiliwa na pengo na uharibifu. La nne, akili ya binadamu itakayokuwa imefikia upeo na ukamilifu wake, wakati ule awaambie mambo ya hekima, kuwaeleza sababu, na kuwapa dalili ya kwamba hukumu hii inatolewa kwa sababu hii. Na la tano, kwa matokeo yake azalishe njia za kujitakasa nafsi.

Kwa hakika, utakaso wa nafsi hauwezekani pasipo ishara bayana na bila hukumu za sheria zilizofafanuliwa ambazo hekima zake zimeelezwa. Na kusudio hasa lilikuwa ni kwamba shabaha ya asili ya kuumbwa kwa umati wa Muhammad^{saw} na kuuimarisha ipate kutimia. Na yule mtu anayemfahamu Nabii Mtukufu^{saw} kuwa mfano mwema na kuufuata, yule mtu anayefaidika na ishara bayana, yule mtu anayejipatia elimu ya maamrishi ya sheria kamili na makatazo yake na kuelimika na hekima zake na kuyatekeleza, na kwa njia hii anapata utakaso wa nafsi, huyo ndiye mtu na hao ndio watu ambao kuhusiana nao ilinenwa mwanzoni mwa aya hizi kwamba **وَضَعَّ لِلنَّاسِ**, na Akasema **كُنْتُمْ خَيْرَ أُمَّةٍ** , **إِنَّ أَوَّلَ بَيْتٍ وُضِعَ لِلنَّاسِ** , **أَلْحَجَّتْ لِلنَّاسِ** . Hivyo, aya hizi zilianzia na **رَبَّنَا وَابْعَثْ فِيهِمْ رَسُولًا مِّنْهُمْ** . Pasipo haya, yale makusudio ishirini na mawili yaliyotajwa ndani ya aya hizi nilizoisha fafania kiasi fulani hapo kabla, hayawezi kupatikana. Na mpaka makusudio haya yapatikane, umati wa Kiislamu hauwezi kuwa umati bora. Kuhusiana na Kurani Tukufu kuwa Al-Kitab na kuhusu

Kurani Tukufu kueleza hekima za hukumu za sheria, ningependa kuwasomea ndugu madondoo mawili wakati huu. Hadhrat Masihi Mau'udi^{as} anasema:

“Leo, juu ya uso wa ardhi kuna Furkan Tukufu pekee kati ya Vitabu viliyofunuliwa, ambayo imethibitika kwa hoja madhubuti kwamba ni Neno la Mungu... ambayo itikadi zake zi kamili na imara ambazo hoja bayana zashuhudia ukweli wake, ambayo hukumu zake zimeimarika juu ya haki tupu... ambayo ina uzuri huu kwamba ... haitaki kutumia nguvu kuikubalisha itikadi yoyote. Bali itoapo fundisho lolote, huwa inatihitisha kwanza ukweli wake, na huhakikisha kila matilaba na dai kwa hoja na dalili bayana. Na ikieleza daili wazi juu ya ukweli wa kila fundisho hufikisha mpaka daraja ya yakini timilifu na maarifa kamili. Na uharibifu, uchafu, dosari na ufisadi vilivyomo ndani ya itikdadi, amali, kauli na matendo, huviondolea mbali hivyo vyote kwa daili bayana zing'aazo. Na hufundisha adabu zile zote zinazomlazimu binadamu kujua ili kuwa binadamu. Na huzuia kila ufisadi kwa nguvu zile zile ambazo kwazo ufisadi umepata kuenea siku hizi. Mafundisho yake ni manyofu, yenye nguvu na imara.”

(Baraahine Ahmadiya, J. 2, (Neno la mbele), uk. 91-92)

Kadhalika, anasema Hadhrat Masihi Mau'udi^{as}:

“Ndiyo yale yale maarifa mepesi yaliyoitwa hekima ndani ya Furkan Tukufu kama Alivyosema:

يُؤْتِي الْحِكْمَةَ مَنْ يَشَاءُ ۗ وَمَنْ يُؤْتَ الْحِكْمَةَ فَقَدْ أُوتِيَ خَيْرًا كَثِيرًا ۗ

Yaani, Mungu Humpa hekima Amtakaye. Na yule aliyejaaliwa hekima, amepewa heri nyingi. Ndiyo kusema kwamba hekima inayo heri nyingi, na aliyepata hekima, amepata heri nyingi. Hivyo, elimu na maarifa haya yanayoitwa hekima kwa maneno mengine, ndiyo kama bahari kwa sababu ya kuwa na heri nyingi, ambayo wanajaaliwa walifuatao Neno la Mungu, nao hutiliwa baraka ndani ya fikira na mtazamo wao hata kwamba kweli halisi za daraja ya juu kabisa zaendelea kuakisika ndani ya nafsi zao zenye sifa ya kioo, na kweli zilizokamilika zadumu kufichuliwa kwao.”

(Barahine Ahmadiyya, J. 4, maelezo juu ya maelezo ya pembeni Na. 3, uk. 445)

Almuradi, haya ndiyo makusudio 23 yahusianayo na kujenga upya Baitullah. Maelezo haya yalihatijika kutolewa kwa sababu siku moja Mwenyezi Mungu kwa nguvu sana Alinielekeza kwenye jambo hili kwamba kizazi cha sasa kinachoweza kuitwa ni kizazi cha tatu cha Uahmadiyya kinalazimika fika kupata ulezi sahihi kwa ajili ya ushindi wa Islam. Yaani, kama hawatalelewa barabara Waahmadiyya wenye umri mpaka wa miaka 25,

²⁷ Sura Al-Baqara, 2:270

au wasiopitisha miaka 15 wale waliojiunga na Uahmadiyya, vikwazo vingi vitazalika katika kupata makusudio haya ambayo kwa kuyapata Mwenyezi Mungu Alimtuma Hadhrat Masihi Mau'udi^{as} kwa sura ya جَرِيٌّ اللهُ فِي حَلِّ الْأَنْبِيَاءِ , na ambayo kwa kuyapata, Mwenyezi Mungu Aliimarisha Jumuiya Ahmadiyya. Kisha Mwenyezi Mungu Akanielekeza kwenye jambo hili kwamba njia zipaswazo kushikwa kwa kuwapatia hao ulezi zimeelezwa ndani ya aya hizi nilizoendelea kuzieleza katika hotuba zangu, na kwamba kama makusudio haya yakizingatiwa barabara na kutiliwa bidii kuyapata, basi kwa fadhili ya Mungu na rehema yake uzao wetu huu ukilelewa vizuri utaweza kutekeleza majukumu yao watakatotwishwa karibuni. Kwani niliekezwa kwenye jambo hili kwamba miaka 20-25 ijayo ni ya muhimu sana na ya kuleta mabadiliko makubwa kwa mwibuko wa pili wa Islam, na nyenzo nyingi za ushindi wa Islam zitazalika, na watu wengi wataingia katika Islam au wataelekea kwenye Islam. Wakati ule *murabbi* na *walimu* watahitajika kwa wingi huo huo. Walimu na *murabbi* hao Jumuiya italetu toka wapi ikiwa hatutafikiria jambo hili leo. Hivyo, zingatieni habari hii na wekeni mbele yenu makusudio yaliyoelezwa ndani ya aya hizi. Namna ya ulezi unaohitajika kwa kupata makusudio haya, wapatieni huo vijana wenu katika mwanga wa Neno Tukufu la Mwenyezi Mungu, ili wakati utakapowadia wawepo wengi sana wenye kujitolea wakfu kwa ajili ya Islam kama *murabbi* na *walimu* ili

litimie kusudio la binadmau wote kujumuishwa – **عَلَى دِينٍ وَاحِدٍ** – katika dini moja.

Nilipokuwa nikitoa hotuba hizi, mzee mmoja aliniandikia kwamba hotuba hizi unazoendelea kutoa zinahusiana na ufunuo mmoja wa Hadhrat Masihi Mau'udi^{as}, ulioandikwa ndani ya Tadhkira, uk. 80, nao ni huu:

“Yule mtu anayeufahamu msingi wa Kaaba kuwa suala la hekima ya Mungu, huyo ndiye mwenye lubu sana kwani anayo hadhi katika siri za ulimwengu wa malaika.”

Hivyo, nafahamu kwamba Mwenyezi Mungu Aliponielekeza kwenye jambo hili, basi Mungu Anataka kuwa wazee wa kaumu pia na vilevile vijana wa kaumu, wanaume wa kaumu pia na kina mama wa kaumu vilevile waanze kufahamu hekima ya Mungu inayohusiana na msingi wa Kaaba ili mbele ya Mwenyezi Mungu wawe wenye lubu, na waweze kufahamu sauti yake na hukumu zake na hekima za hukumu, nao waingie ndani ya kundi la watakatifu wanaojaaliwa saa zote fadhili za Mwenyezi Mungu. Ingawaje mpango au mkakati nitakaoweka mbele ya Jumuiya, shabaha yake hasa ni ulezi wa vijana ambao umri wao ni hadi miaka 25 kama wamezaliwa ndani ya Uahmadiyya, na kama ni wapya waliojiunga katika Uahmadiyya ni wenye miaka 15. Lakini kwa kuwalea vijana hawa, hakuna budi kuwalea wakubwa ili waweze

Makusudio 23 Adhimu ya Ujenzi wa Baitullah

kuwapatia ulezi wazao hawa. Hivyo, baada ya vijana nawaambia wanaume wote wa Jumuiya na kina dada wote wa Jumuiya wenye umri zaidi ya miaka 25, kwani siwezi peke yangu au wenzangu wachache kuwalea malaki ya vijana walio chini ya umri wa miaka 25 au kwa jiha nyingine wako chini ya miaka 15. Tutatakiwa kutakasa kila nyumba ili kila mmoja anayelelewa ndani ya kila nyumba apate kuwa askari wa Mungu na kujipatia ridhaa Yake. Sisi tutalazimika kutumia njia za kutakasa kila mtaa, kila kijiji na kila mji ili ndani ya mazingira yaliyotakasika kizazi kile kipate kuzaliwa ambao wawe wenye kutoa uhai wao, nyakati zao heshima zao, na kutoka dhabihu ya mali zao kwa ajili ya heshima na sifa njema ya Mtume Muhammad^{saw}.

Labda ningesema kwamba watu wazima wapaswa kwanza kupatiwa ulezi, ili kwa njia yao wadogo waweze kulelewa ambao karibuni watatakiwa kubeba majukumu makubwa fika. Kumbukeni, kama tukighafilika, tutashukiwa na ghadhabu ya Mungu, hapo tena watu wengine wataletwa watakaorithi ahadi za Mungu. Hivyo, jilindeni nafsi zenu na mjiweke tayari kutekeleza majukumu yenu nitakayowatuisheni sawa na matakwa ya Mungu, kwa njia ya mkakati fulani, ambayo nitaeleza maoni yangu kuhusiana nayo, inshallah, kwa kujaaliwa na Yeye.

(Gazeti la Al-Fadhl, Rabwah, 25 Juni 1967)